ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kwanza - Tarehe 15 Februari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kuanza kwa Mkutano)

DUA

Mhe. Spika: (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukuwe nafasi hii kuwakaribisha sana katika Mkutano wetu huu wa Tano katika Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 15 Februari 2017.

Napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla taarifa kuhusu Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika mkutano uliopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 23 Novemba 2016 mpaka tarehe 2 Disemba 2016.

Katika Mkutano wa nne wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Baraza hili lilipitisha Miswada minne ya Sheria ambayo ni:-

(1) Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutunga upya Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na masuala yanayohusiana na hayo.

(2) Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya mwaka 2005 kuweka Masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa mfuko na mambo yanayohusiana na hayo.

(3) Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa mali za serikali namba 9 ya mwaka 2005 na kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji wa

Mali za Umma na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.

(4) Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kuweka masharti bora ya kudhibiti na kusimamia fedha za umma na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo na kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali namba 12 ya mwaka 2005.

Kama inavyotakiwa chini ya kanuni ya 91 (3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012, naomba kutoa taarifa kwamba Miswada ifuatayo sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*)

Miswada yenyewe ni kama ifuatavyo:-

(1) Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutunga upya Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na masuala yanayohusiana na hayo.

(2) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya mwaka 2005 kuweka masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa mfuko na mambo yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsanteni. (*Makofi*).

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani nakala zote za Gazeti rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 3 Disemba mwaka 2016 naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na sasa namwita tena Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na Kutunga Sheria ya Kuanzisha

Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Panya Ali Abdalla (**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa idhini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 44

Kuibuka kwa Makundi ya Uhalifu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza**:-**

Kumekuwa na makundi ya vijana wanaotenda uhalifu nyakati za usiku kwa kutishia watu kwa mapanga, kuwaibia na kuwabaka hasa katika mitaa ya Kwamtipura, Kilimahewa, Darajabovu na Mtopepo.

Je, ni hatua gani zimechukuliwa kuyadhibiti makundi hayo maovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 44 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kuyadhibiti makundi ya vijana wanaotenda uhalifu hasa nyakati za usiku kwa kuwatishia watu kwa mapanga, kuwaibia na kuwabaka hasa katika mitaa ya Kwamtipura, Kilimahewa, Darajabovu na Mtopepo.

Mhe. Spika, hatua hizo ni kama zifuatazo:-

1. Kuimarisha Doria za Miguu na Gari kwa kushirikiana na vikundi vyengine vya Ulinzi na Usalama.

2. Kuimarisha vikundi vya Ulinzi shirikishi na kuona baadhi ya vikundi vilipunguza ari na kasi, hivyo kupelekea maeneo haya kurudia vitendo vya uhalifu.

3. Kuanzisha dhana ya Mabalozi wa Uhalifu kwa kuwatumia wahalifu wazoefu ambao kwa hiyari yao waliamua kuachana na kutenda vitendo vya kihalifu kwa kuwa karibu na Jeshi la Polisi kwa kutupatia taarifa mbali mbali za makundi yanayojihusisha na vitendo vya kihalifu na kuzifanyia kazi.

4. Kutoa elimu ya kutosha kwa Raia kwa kuwashajihisha kuwa tayari kushirikiana na Polisi na vyombo vyengine vya Usalama iwapo wataona watu wanaowatilia mashaka katika maeneo yao.

5. Kuzifanyia kazi taarifa za Kiintelijensia kuhusiana na matukio mbali mbali ya kihalifu yanayotaka kutokea au yaliyokwishatokea. Mhe. Spika, Katika kudhibiti vitendo hivyo viovu naomba kueleza matukio yaliyojitokeza na hatua zilizofikiwa na vyombo vya kisheria kama ifuatavyo:-

S/NO.	Aina Ya Kosa	Idadi Ya Kesi	Zilizopo Mahakamani	Zinazo Pelelezwa	Zilizo-po Kwa Dpp	Watuhumiwa MMe: ke
1.	Unyang'anyi	14	5	5	4	17: -
2.	Shambulio la hatari	7	-	4	3	14 : -
3.	Uzembe na Ukorofi	1	-	-	1	4 : -
4.	Kubaka	1	1	-	-	2 : -

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: (a) Mhe. Spika, je, serikali itatoa tamko gani baada ya haya yote kuyazungumza kwamba wamesimamiwa lakini bado

uhalifu ndani ya mitaa yetu unaendelea na hivi juzi tu msichana mmoja alifanyiwa vibaya na watu zaidi ya watatu.

(b) Kuna kesi ilitokea katika Jimbo la Mpendae lakini alifanyiwa kijana wangu wa Jang'ombe. Je, mpaka dakika hii imechukuliwa hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (a) Mhe. Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi serikali tayari imeshachukua hatua mbali mbali kuhakikisha inakabiliana na kadhia hii. Lakini pia serikali imekuwa ikiwaomba sana na kuwanasihi wananchi kujitokeza kwa hali na mali popote pale ambapo matukio kama haya yamekuwa yakitokea katika maeneo yetu. Wakati mwengine vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na vile vyombo mbali mbali vya serikali vimekuwa vikipata tabu, kwa sababu matukio yanatokea lakini baadhi ya wananchi wetu wanakuwa hawako rafiki katika kwenda kusaidia vyombo hivi vya ulinzi na usalama.

(b) Katika swali la pili ambalo amehusisha kijana wake wa Jang'ombe na hiyo kesi ya Mpendae niseme tu Mhe. Spika, tunachokifanyia kazi ni kile ambacho kimeripotiwa katika vyombo vya ulinzi na usalama. Tutalichukuwa hili, kama tutakuta taarifa hizi zipo katika kituo cha Polisi na katika vyombo vya ulinzi na usalama tutajitahidi kumpatia jibu kadiri iwezekanavyo Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Machano Othman Said: (a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri anaelewa kwamba baadhi ya Vituo vya Polisi vinageuka vijiwe vya raia hivyo kuwafanya raia nao kuogopa kupeleka kesi zao kwa kuwaona kwamba kesi zao zitavuja.

(b) Mhe. Waziri na serikali inaelewa kwamba usiku wa kuamkia leo moja wa madereva wa viongozi mawaziri kanyang'anywa simu na pesa baada ya kumshusha waziri kutoka mkutanoni jana usiku.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa maana Mhe. Machano Othman Said hakuuliza swali isipokuwa ametoa taarifa.

(a) Tunashukuru kwa lile la kusema kwamba dereva wa Waziri ama dereva wa kiongozi amepatwa na tukio lile tunashukuru kwamba ametupa taarifa lakini tutatizama katika vyombo vyetu kwamba taarifa hiyo imefika ili tujue namna gani tutaweza kuifanyia kazi.

(b) Suala la baadhi ya vituo vya Polisi kugeuka kuwa ni vijiwe na raia kukimbia tumekuwa tukiwasihi sana raia kwenda kutoa taarifa katika vituo vya Polisi. Lakini hili ambalo imekuwa ikisemekana baadhi ya Polisi wakitoa taarifa zisizo rasmi ama taarifa kwa raia ambao wamekwenda kutoa taarifa zile mitaani, wakati mwengine likitokea, wakati mwengine yamekuwa ni maneno ya watu ambao wameshindwa ama wanaogopa kwenda katika vituo vya Polisi. Lakini tunaomba sana watusaidie sana wananchi wote kwa ujumla endapo wanahisi taarifa zao zimekuwa zikivuja kuna vyombo vingi sana vya kutoa taarifa hizi. Sasa tunaomba wasichoke angalau taarifa inapofika katika ngazi moja iende katika ngazi ya pili ili tujue yule mtu ambaye atakuwa ama yule askari ambaye atakuwa amehusiana na kutoa taarifa ile naye sheria zile za kiaskari ama za kiintelijensia nazo zipate kufanya kazi.

Serikali haipo tayari kumvumilia askari yeyote ambaye atakuwa anachukua taarifa kwa dhamira ya kwenda kutoa taarifa nje na kushirikiana na wananchi badala ya kuisaidia serikali Mhe. Spika, nakushukuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, kwa kuwa utafiti uliofanyika inaonekana watumiaji wengi wa haya masuala ya kupora kunyang'anya na kujeruhi yanatokana na vijana wanaotumia madawa ya kulevya na Afisi yako Mhe. Naibu Waziri ndio inayohusina na masuala ya kupambana na Madawa ya kulevya.

Je, wizara yako imeandaa mikakati gani ya kutokomeza suala la utumiaji wa madawa ya kulevya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, inawezekana ikawa kweli vijana wengi ambao wanajihusisha na matukio mbali mbali wakawa wanatumia madawa ya kulevya. Lakini wakati mwengine inawezekana, ndio maana nikasema sio kwa asilimia zote na nikiri kwamba Tume ya Madawa ya Kulevya iko chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini mikakati gani ambayo tunayo.

Mikakati ya kwanza ambayo tunayo ipo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Madawa ya Kulevya iliomo katika Tume. Lakini jambo la pili suala la mikakati ya kupambana na suala zima la Madawa ya Kulevya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ishalitizama hilo kwa jicho la upana na kwa makini na yapo mengi ambayo tayari yameshakuwa tayari kwa dhamira ya kuanza kukabiliana nayo. Lakini Afisi yangu imeshakutana na vyombo mbali mbali vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha wanalidhibiti kwa kadiri itakavyowezekana suala zima la

kadhia ya Madawa ya Kulevya ndani ya Zanzibar yetu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa sasa aje Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza napenda nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya nyongeza na ya msingi kwa namna alivyoyajibu kwa ufasaha kabisa.

Aidha napenda niongezee jibu la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe nyote mtakumbuka kwamba viongozi wetu wakuu wamekuwa wakitoa maagizo na maelekezo mbali mbali juu ya kupambana na vitendo vyote vya uhalifu nchini. Ni hivi karibuni tu Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama alitoa agizo mahasusi la namna ya kupambana na vitendo hivi vya aina yote ya madawa ya kulevya, udhalilishaji wa kijinsia na aina yoyote ile ya uhalifu nchini.

Kwa msingi huo Mhe. Spika, ni kwamba viongozi wote wa vyombo hivi vya Ulinzi na Usalama wana wajibu mkubwa wa kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na itakuwa ni kipimo cha kazi Wakuu wetu wa vyombo vya ulinzi na usalama hususan Makamanda wa Polisi wa Wilaya, kitendo chochote ambacho kitahusiana na madawa ya kulevya unyanyasaji na uhalifu mwengine kitakachotokea katika Wilaya basi Mkuu wa Polisi wa Wilaya atawajibika kutokana na agizo hilo.

Hivyo nitoe wito kwa wakuu wetu hawa kuhakikisha katika Wilaya zao hakuna aina yoyote ya vitendo viovu vya madawa ya kulevya, hakuna aina yoyote ya unyanyasaji unatokea katika wilaya zao pamoja na uhalifu mwengine na kutokufanya hivyo, maana yake ni kusikiliza amri halali ya Mkuu wa Nchi, kwa hivyo kwa sasa Jeshi la Polisi na vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vitakuwa na uperesheni maalum ya kutekeleza wajibu wao kutokana na agizo hilo.

Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na wananchi wote washirikiane na Serikali katika kutoa taarifa za aina yoyote ya vitendo vya uhalifu, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais milango yake iko wazi, Ofisi zetu za Wakuu wa wilaya milango yake iko wazi, Masheha katika Shehia zao milango iko wazi na vituo vyote vya Polisi milango iko wazi kwa taarifa zozote ambazo

zinaonyesha uhalifu, ima madawa ya kulevya, ima udhalilishaji wa kijinsia au wa aina yoyote ya uhalifu ili hatua za haraka zikuchukuliwe, na wale watakaokuwa wazembe au watakaosaidia wahalifu katika kufanya kazi hiyo kwa hivyo sheria itachukua mkondo wake hatovumiliwa ikiwa kiongozi, ikiwa askari, ikiwa Mwanasheria, ikiwa mfanyabiashara yeyote yule atakayesaidia vitendo vya uhalifu sheria itachukua mkono wake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 1

Utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kupandisha mishahara ya kima cha chini:

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:-**

Kwa nia njema. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Moh'd Shein ameahidi kupandisha mishahara kwa wafanyakazi wa kima cha chini kwa aslimia 100 ili kuwawezesha wananchi wake kupata maisha bora.

(a) Je, Serikali inakusudia kupandisha mishahara kwa asilimia 100 kwa wafanyakazi wa kima cha chini pekee au inapandisha kwa wafanyakazi wote wa Serikali.

(b) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

(c) Je, upandishaji huo utawahusu pia wafanyakazi wa Mashirika ya Umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria ,Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, Kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarhan Said Mwakilishi wa Jimbo la Chake chake suala lake nambari 1 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mwakilishi kwamba ni kweli Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Ali Mohammed Shein ameahidi kupandishwa mishahara ya Wafanyakazi wa kima cha chini kwa asilimia 100 ili pamoja na mambo mengine kuwawezesha watumishi hawa kupata maisha bora.

Mhe. Spika, Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina lengo la kupandisha kima cha chini cha mshahara kwa asilimia mia moja . Hata hivyo ongezeko hili la mshahara la asilimia mia moja haliwezi kufanywa kwa mishahra ya Watumishi wengine kutokana na viwango walivyonavyo vya mishahara. Ili kuweka uwiano mzuri baina ya mishahara na kuzingatia uwezo wa Serikali, mishahara ya watumishi wengine itaongezwa kwa utaratibu maalumu utakaoandaliwa kitaalamu.

b) Mhe. Spika, Serikali imepanga kufanya marekebisho ya mishahara ya Watumishi wa Umma ifikapo mwezi wa April, 2017.

c) Mhe. Spika, Marekebisho hayo hayatawahusu watumishi wa Mashirika ya Umma kwa sababu viwango vya mishahara vinavyolipwa katika Serikali kuu vinatofautiana na viwango vinavyolipwa katika mashirika hayo. Tafauti hiyo inatokana na ushindani wa kibiashara uliopo miongoni mwa mashirika ya Umma, Uzalishaji na ukusanyaji wa Mapato kwa baaadhi ya Mashirika hayo. Aidha, Taasisi hizo zinasimamiwa na Sheria zao ambazo huzipa mamlaka Bodi za Wakurugenzi kupendekeza serikalini Maslahi ya Watumishi wa Taasisi zao.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Waziri naomba kuuliza Swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inategemea mapato yake sana kutokana na biashara ya utalii na tuliona kwa miaka ya nyuma hasa wakati wa 1997 na pia wakati wa *financial crisis* jinsi gani makusanyo ya mapato yalipungua katika bodi yetu ya ZRB. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba itakuwa ni jambo endelevu katika ongezeko la mishahara ili pale ambapo uchumi utaweza kudorora, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria ,Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kama nilivyosema awali kutokana na kile kipato ambacho wanapata mashirika haya ya Umma kwa sasa hivi tumeona kwamba bado hakuna haja Mashirika haya kuweza kupata hiyo asilimia iliyoongezwa.

Lakini hata hivyo pale ambapo hali itakapozidi kuwa nzuri zaidi basi na haya mashirika tutaangalia namna gani tunaweza kuyashughulikia.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Je, ni Shilingi ngapi zitatumika kwa ajili ya mabadiliko haya ya mshahara.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria ,Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kwa sasa hivi ni vigumu kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake ambalo linahitaji zaidi kupata data za kutosha, kwa hivyo nimwambie swali lake hilo nitamjibu kwa njia ya maandishi.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, nasimama kwa kanuni ya 37(1) ambayo inasema Waziri au Mjumbe yoyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu suali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba suali aliloulizwa Waziri moja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana swali nililouliza mimi langu la nyongeza na majibu niliyopewa halifanani, haliendani kabisa na suali nililouliza. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri angejibu suali langu kama nilivyouliza maana yake mimi sikuuliza suala kuhusiana na Mashirika ya Umma, wala neno la Shirika la Umma sijataja hasa nimezungumza masuala ya uchumi na jinsi gani Serikali itaweza kulipa mishahara pale ambapo uchumi utadorora

Mhe. Spika: Mhe. Simai samahani swali la msingi kwanza halikuwa lako ni swali ambalo uliuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Sarahani, maana yake pale mwanzo maelezo yako ulilitaguliza kama ni swali lako.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, swali nililouliza mimi sawa niliuliza swali kwa niaba ya Mhe. Suleiman Sarahani, swali langu la nyongeza lilikuwa ni la kwangu mwenyewe na uliniita Mhe. Spika, Mhe. Simai.

Mhe. Spika: Hamna tatizo tutafuatilia mpe Mheshimiwa swali lako ili akujibu kwa maandishi kwa sababu sasa hivi hatuwezi tena kumpa ili akujibu hivyo unavyotaka wewe ujibiwe atakujibu kwa maandishi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, nimesikia.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, awali ya yote nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kauli yake nzuri ambayo wananchi au wafanyakazi wote wana matumaini nae kwamba ni kiongozi bora na anakwenda katika utawala bora, kwa kuwa Mheshimiwa Rais kaongeza nyongeza mishahara kwa kima cha chini kwa asilimia mia moja. Lakini tunajua tu kwamba ili juhudi iongezeke panataka usimamizi mzuri kwa wafanyakazi wetu kuongeza nidhamu katika kazi.

Je, Serikali imejiandaa vipi kwa kuwa motisha ya asilimia mia moja aliyoongeza Rais inataka juhudi zaidi za kuongeza kasi na kuondoa kero kwa wafanyakazi na watumishi wa umma wa Serikali, Wizara ina mpango gani wa kutoa wito katika wafanyakazi wetu kwenda sambamba na hii adhma ya Rais kuongeza kipato au kuongeza mshahara ni kuongeza kazi katika maeneo yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria ,Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Serikali itapandisha kiwango hicho cha Mishahra kwa wale wote ambao wenye kipato cha chini kama nilivyoeleza awali, lakini hata hivyo kuongezeka kwa kipato hiki Serikali itaendelea kuhimiza kama ambavyo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein anavyohimiza kwamba tuache kufanya kazi kwa mazoea, tutakapoacha kufanya kazi kwa mazoea basi uzalishaji utaongezeka na mapato zaidi yataongezeka nchini kwetu na wafanyakazi wote tunaweza tukafarajika na hilo Ahsante sana.

Nam. 39

Kutofanya kazi ubao wa matokeo uwanja wa Amani

Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Haji Makame - Aliuliza**:-**

Bao la kuonyesha saa na matokeo ya mpira wa miguu kwa muda mrefu limekuwa halifanyi kazi katika Uwanja wa Amani kinyume na matarajio ya wapenzi wa mpira wa miguu na hivyo kuupunguzia hadhi Uwanja wetu wa Amani.

a) Sababu gani zilizopelekea kutofanya kazi ubao huo wa saa na matokeo ya mchezo.

b) Lini Wizara itarejesha tena huduma hizo katika Uwanja wa Amani.

c) Kama huduma hiyo imeshindikana kwanini Wizara hairejeshi utaratibu wa kuonyesha matokeo kwa njia ya kawaida (*manual*) kama ilivyokuwa zamani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu **:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake nambati 39 lenye kipengele a,b,na c kama ifuatavyo:-

a) Sababu za msingi zilizopelekea ubao wa saa na matokeo kutofanya kazi ni ukoserfu wa upatikanaji wa "*Spare*" vipuri vya kutengenezea ubao huo na saa.

Kampuni ambazo zimetengeneza ubao huo kwa sasa hazitengenezi tena vifaa au vipuri vya aina hiyo.

b) Mhe. Spika, huduma hiyo kwa hivi sasa imesharejea tena katika Uwanja wa Amani kutokana na umahiri wa mafundi wetu.

c) Huduma ya ubao wa matokeo imerejea katika hali ya kawaida lakini itaposhindikana kutokana na tatizo la mabadiliko ya teknologia tutaagiza ubao mwengine na sio kurejea katika kutumia unao wa zamani "manual".

Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame: Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja tu la nyongeza.

Mhe. Waziri tunashukuru sana hiyo kazi nzuri iliyofanywa na mafundi wetu kwa kurejesha huduma ile, lakini nataka nitoe *observation* moja tu. Mheshimiwa kabla ya swali langu, wakati wa michuano ya Kombe la Mapinduzi kuanzia mechi ya mwanzo mpaka fainali Mhe. Rais alipokuja kutoa kombe kwa mshindi ubao ule wa matokeo na saa ulikuwa ukifanya kazi, na juzi kwenye mashindano ya kombe la *African Football Confederation* ambazo timu zetu mbili timu ya Zimamoto ilicheza na timu ya Msumbiji, na timu ya KVZ

ilicheza na timu ya Burundi ubao ule umefanya kazi na saa. Je, kwa nini mechi zetu za ligi ya Zanzibar ubao ule haufanyi kazi?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, lengo la Serikali ni kuona kwamba wananchi wetu waliofika pale wanaona matangazo yale kupitia bao letu la saa, lakini napenda nimjibu Mhe. Muwakilishi kwamba kutokana na matatizo ambayo nimeyaeleza kwamba ubao huu vipuri vyake vimeshakuwa vya zamani na vipuri hivi havipo, matatizo yale wakati mwengine yanajitokeza bila ya kutarajia.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Muwakilishi kwamba tutaendelea kufanya juhudi za makusudi kuona kwamba ubao ule unafanya kazi wakati wa timu zetu za Zanzibar zinapokuwepo katika ligi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri nauomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Je, Mhe. Waziri unafahamu timu zetu za Zanzibar zinapocheza zinatozwa pesa ili kuwashwa ubao ule ni nini tamko la Serikali juu ya jambo hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, wakati timu zetu zinapocheza uwanja wa Amaan tunaelewa kwamba si wapenzi wengi tunaoingia katika kuona burudani zile, na matokeo yale pato linalopatikana katika uwanja huwa halisaidii katika kukidhi shughuli yoyote ile ya uwanja, lakini si kweli kwamba watu wanatozwa pesa kwa lengo ya zile mechi zao. Isipokuwa tu nataka nimfahamishe kwamba mapato yanayopatikana timu huwa zinagawiwa kwa mgao uliowekwa. Ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza naomba nishukuru sana Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo kwa timu zetu mbili kushinda kwa mara ya kwanza kwa mpigo katika mashindano ya Afrika, na pia niwapongeze vikosi vya SMZ, maana hizo timu zote ni timu za vikosi, Zima Moto na KVZ.

Sasa swali langu lipo hapa, Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu maswali alisema kutokana na tatizo la teknolojia na uchakavu. Lakini Mhe. Waziri anasema ni gharama, lipi tulijue la ukweli. Bao lile linakuwa halioneshwi kutokana na gharama kubwa za uwanja kwa ligi ya Zanzibar au ni kutokana na matatizo ya kiufundi. Hili hawaelewi kwamba bao lile linaweka saa, dakika na kila kitu ili kuweza kuondoa mzozo, linapokuwa halipo lile bao je, hatuoni kwamba tunasababisha migogoro katika mpira wa miguu Zanzibar na kurejesha nyuma maendeleo yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, bao letu lile pale lililotengenezwa limetengenezwa wakati panafanyika matengenezo ya Uwanja wa Amani takriban miaka mitano iliyopita. Lakini teknolojia iliyotumika pale vifaa vyake kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kwa sasa vifaa vile havipo ni umahiri tu wa mafundi wetu akina Chui kuweza kulirudisha bao lile na kufanya kazi kama kawaida.

Kwa hivyo kama anavyoijua *electronic*, kuna wakati zinajitokeza kwamba zinafanya kazi kuna wakati zinajitokeza zinafanya zinaleta matatizo. Tumehisi ni vyama bao lile tutumie wakati wa mambo yaliyokuwa yana umuhimu wake tuhakikishe kwamba yanafanya kazi, na pale ambapo mechi zetu zinachezwa si vibaya kuzionesha kwamba tunaweza kufanya hivyo. Lakini tatizo hasa ni la kiufundi linalotokana mule kwenye bodi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi naomba uniruhusu kwa dakika moja kabla ya kuuliza swali langu hili.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa tukiwa hai na sote tukiwa wazima, huu ni uwezo wake.

Vile vile nikushukuru wewe kwa dakika moja uliyonipa na niwashukuru wananchi wa Dimani kwa kutumia haki yao ya msingi ya kupiga kura na kuendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi na kukipa ushindi mkubwa, Chama ambacho kikubwa kuliko vyama vyote, na ni chama tishio. Pia niwashukuru ndugu zetu wa Tanzania Bara baada ya kuwaamini Madiwani karibu 24 kushinda kule kasoro kata moja tu, huu ndio muelekeo wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba uulize swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba serikali itoe jawabu.

Nam. 4

Kushuka kwa Kiwango cha Elimu Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Matokeo ya mtihani wa kidato cha sita yameonesha kuwa kiwango cha elimu Zanzibar kimeshuka vibaya sana.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea wanafunzi kufanya vibaya katika masomo yao, na ni kwa nini tatizo hili linaendelea kuwa sugu pamoja na ahadi nyingi za Serikali.

(b) Mitaala inayotumika katika Skuli za Maandalizi, msingi na Sekondari za Tanzania Bara na Zanzibar haimo katika masuala ya Muungano , Je, kuna uwiano gani kati ya mitaala inayotumika katika skuli hizo kwa Tanzania Baraza na mitaala ya Zanzibar na vipi mitaala hiyo inachangia kufeli kwa wanafunzi wetu.

(c) Je, Serikali itawasaidia vipi vijana waliofanya vibaya katika mitihani hiyo ili waweze kupata elimu ya kuweza kuwasaidia maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 4 lenye sehemu (a), (b) na (c).

Kwanza napenda kutoa maelezo yafuatayo:

Wizara inapenda kutofautiana na Mheshimiwa Mwakilishi kwa maelezo yake kuwa kiwango cha Elimu cha Zanzibar kwa hoja kwamba wanafunzi wa Zanzibar wamefanya vibaya mitihani ya Kidato cha Sita mwaka 2016. Matokeo ya Mtihani ya mwaka mmoja tu hayawezi kuchukuliwa ndio kigezo pekee cha kupima kushuka kwa kiwango cha Elimu katika nchi yetu.

Hata hivyo, napenda nikiri kuwa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita kwa mwaka 2016 kwa watahiniwa wa Zanzibar yalishuka kidogo ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 93.2 ukilinganisha na asilimia 97.6 mwaka 2015. Pia Idadi ya watahiniwa waliofaulu na kutunukiwa cheti cha daraja la kwanza hadi la tatu walikuwa ni 1,548 sawa na asilimia 85.7.

Natumai utakubaliana na Wizara kuwa kiwango hicho cha kufaulu sio cha chini kama baadhi ya watu wanavyodhania.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama hivi ifuatavyo:

a) Kushuka kwa kiwango cha kufaulu cha wanafunzi wetu kumechangiwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uhaba wa walimu hasa wa masomo ya Sayansi na Hesabati; upungufu wa vifaa vya kufundishia vikiwemo vifaa vya maabara na kemikali na wingi wa wanafunzi katika madarasa na kupelekea baadhi ya skuli kusoma kwa mikondo miwili ambapo kunaathiri ukamilishaji wa mtaala na kusomesha chini ya kiwango.

b) Mitaala ya Elimu ya Maandalizi na Msingi ni tofauti baina ya Skuli za Zanzibar na za Tanzania Bara, ingawa kuna mlingano wa baadhi ya malengo, falsafa na hata mada. Mtaala wetu umelenga zaidi kuwafundisha wanafunzi wetu wadogo kuelewa zaidi mazingira ya Zanzibar. Katika ngazi ya Elimu ya Sekondari mitaala ya masomo inayotumika ni ya aina moja na ndiyo sababu wanafunzi wetu wanafanya mtihani mmoja wa Taifa.

c) Wizara inawashauri vijana waliofanya vibaya kutovunjika moyo na matokeo waliyoyapata. Wajiendeleze na kurudia mitihani yao ya kidato cha sita kama wanafunzi wa faragha. Baadhi yao wana uwezo wa kujiunga na masomo ya Stashahada yanayotolewa katika Vyuo mbali mbali. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri anasema kwamba yupo tayari kutofautiana na mimi, na mimi niko tayari kutofautiana na yeye. Hesabu inaanza moja ndipo uende *step* ya pili hata ukienda huwezi kuanza na hatua mbili. Kwa hivyo amekiri Naibu Waziri kuwa viwango vya kufaulu sio vizuri, uhalisia ndio unavyoendelea katika takwimu zako ulivyozitaja kwa mfano ulioutaja wa daraja la kwanza mpaka la tatu. Hujaeleza ni masomo yepi waliyofaulu.

a) Je unaweza kueleza Baraza hili ni masomo gani kiwango walichofaulu.

b) Kwa kuwa umekiri kuwa tatizo la masomo ya sayansi na walimu na vifaa havipo, hivi juzi tu kulikuwa kuna walimu wa

sayansi karibu 70 na taarifa nilizonazo walifika mpaka Wizarani kwenu, mkachelewa kuwaajiri. Kuna ule msemo unaosema *"chelewa chelewa utakuta mtoto si wako"* wamechukuliwa na ndugu zetu wa Tanzania Bara. Je, lini mtakuwa tayari kuzungumza kwa mdomo baadaye tukafanya vitendo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza ningependa kujibu kwamba taratibu za ajira au uajiri una taratibu zake, na taratibu hizo ni lazima zikamilike ili mtu aweze kuajiriwa. Lakini hata hivyo ruhusa ya muhitimu yeyote inatolewa kuweza kuomba ajira katika sehemu yoyote ya dunia sio Tanzania Bara na pengine popote ruhusa hiyo ipo. Lakini tunachoweza kusema kama ni serikali kwamba baada ya taratibu kukamilika baadhi ya vijana hao tumeshaanza kuwaajiri na tumeshaanza kuwapangia kazi katika kipindi hichi ambacho sasa wanaendelea na kazi.

Mhe. Spika, ili kuona kwamba vijana hawa tunawaajiri mara moja wanapomaliza skuli, serikali imeturuhusu sasa kuwaajiri mara moja baada ya kumaliza masomo kuanzia mwaka huu.

Swali la (a) sikulifahamu, kwa hivyo naomba arejee tena, sikulisikia .

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba nizungumze kidogo kidogo.

(a) Mhe. Naibu Waziri umekiri kwa kuwa viwango vya kufaulu sio vizuri, uhalisia ndivyo unavyojieleza kuna takwimu ya daraja la kwanza hadi la tatu ulizozitaja. Je, ni masomo yepi waliyofaulu katika madaraja hayo ili Baraza liweze kujua ni masomo gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nimesema kwamba tunachokiri kwamba unapolinganisha mwaka huu na mwaka uliopita, mwaka huu kidogo kiwango kimeshuka, lakini kushuka kwenyewe sio katika kiwango kibaya, tumesema ni asilimia 93. Asilimia 93 ndugu Wawakilishi katika 100 hiyo ni mbaya? Bila shaka sio mbaya.

Nataka niseme pia tukirudi kwenye takwimu miaka iliyopita nyuma tulikuwa chini ya kiwango hichi isipokuwa mwaka 2015 tu ndipo tuliponyanyuka kidogo zaidi, kwa hivyo asilimia 93 si mbaya, kwa hiyo hakuna jambo baya lililotokea. Katika 100 tukapasisha 97 wakakosa 7 hicho si kitu kibaya, lazima tuelewe hivyo.

Suala la pili au sehemu ya pili tunachosema kwamba ni masomo gani kati ya sayansi na masomo ya *arts*, masomo gani yalifanyiwa vibaya zaidi. Hapa hatuna takwimu sahihi lakini tunachosema kwamba wanafunzi wa masomo ya sayansi wamefanya vizuri zaidi kuliko masomo ya *arts* katika kiwango cha *A level.* Kwa sasa tumejipanga zaidi na tunatarajia mwaka huu matokeo yatakuwa mazuri zaidi kutokana na ufuatiliaji. Kwa sababu mpaka sasa tumezifuatilia skuli zote tayari wameshasomesha mpaka asilimia 97 kumaliza *syllabus* na imebakia miezi mitatu zaidi. Kwa hivyo, tuna hakika mwaka huo matokeo yatakuwa mazuri zaidi. Ahsante.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Welezo kwa kunichagua lakini na kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kukiri kwamba leo tarehe 15/2/2017 kwamba wanafunzi hawakufanya vizuri.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba haoni kwamba kutofanya hivi vizuri kwa wanafunzi hasa kwa skuli za serikali, wakati skuli za binafsi zinafanya vizuri, na skuli za serikali ndizo skuli za watoto wa wakulima na wakwezi wanazozitumia. Je, haoni kwamba watoto wa kitajiri ndio watakaokuwa na elimu huko tunakoelekea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, hapa kuna mchanganyiko kidogo, hoja ya msingi ni matokeo ya mwaka jana ya kidatu cha sita, hiyo ndiyo ambayo tunazungumza. Mwakilishi anazungumzia kidatu cha pili na cha sita. Kwa hivyo nadhani hapa ni mambo tofauti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, taarifa. Mhe. Spika, kwa mujibu wa ...

Mhe. Spika: Samahani, taarifa kwa kifungu gani cha Kanuni.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kifungu ambacho amekinukuu Mhe. Simai ambacho nimekisahau. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa naomba ukae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillahi Rahmani Rahim*. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa mambo mengi yanayochangia watoto kufeli ni kuvuja kwa skuli, kukaa vibaya kutokana na madeski hakuna pamoja na hali mbaya wanayoipata, hata mafeni hakuna wanasoma kwa hali ngumu. Ni lini serikali

kupitia Wizara yake ya Elimu itahakikisha skuli zinaanza kupewa madeski ili wanafunzi wapate kusoma vizuri, kuingiziwa mafeni na mabati yasiyovuja.

b) Ni lini Wizara hiyo ya Elimu na Wizara nyengine zitaacha kutegemea sana Wawakilishi kuchangia katika masuala yao yanayohusu Wizara zao.

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa maswali yako yote hayahusiani na swali la msingi ambalo Mhe. Waziri ameulizwa hapa. Swali la msingi ni ufaulu, sasa haya mambo ya madawati sifikirii kama ...

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Kwa sababu kilichochangia kufeli ni kwa sababu hakuna madeski na kunavuja.

Mhe. Spika: Basi naomba ukae Mheshimiwa. Katibu, Wizara inayofuata.

Nam. 56

Msaada wa Mbegu kwa Wakulima wa Mpunga

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza:-

Kilimo ndio uti wa mgongo kwa Taifa letu. Hata hivyo kumekuwa na changamoto mbali mbali katika Kilimo kwenye majimbo yetu likiwemo Jimbo la Ziwani ambapo wananchi wengi wa jimbo hilo ikiwemo Shehia ya Ndagoni, Wesha na Michungwani wamekosa mavuno ya mpunga kwa msimu uliopita kutokana na mashamba yao kuingia maji ya chumvi.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapatia mbegu ya mpunga wananchi hao angalau kwa msimu unaofuata wa kilimo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 56 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili , Mifugo na Uvuvi ina mpango wa kuwapatia mbegu ya mpunga wakulima wote wa Zanzibar wakiwemo wa

Jimbo la Ziwani kwa kufahamu kwamba msimu wa mavuno 2015/2016 wakulima wengi waliharibikiwa na wengi wao hawakuvuna.

Wizara imeongeza uagiziaji wa mbegu kutoka tani 250 hadi 500 ili kukidhi haja ya wakulima kwa kuwauzia kwa bei ya ruzuku ambapo kilo moja inauzwa shilingi 200, tu wakati wizara inanunua kwa wastani wa shilingi 2,000 kwa kilo moja, ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri mara nyingi mpunga huu ambao kwamba ni mbegu ya wakulima wale hutoka, lakini kuna wajanja ambao huchukua na wakaweka majumbani mwao bila ya kufuata taratibu. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wale walioathirika kwenye kilimo kile wanapewa kipaumbele.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza nimuombe Mhe. Mwakilishi hili ni jambo letu sote tusaidiane kwa kuwaelimisha wananchi wetu kwamba wanapotoa mbegu basi wasiweke ndani au wasiutwange na wakafanya kwamba ni chakula wakala. Hii ni mbegu basi waitumie kama ni mbegu. Vile vile hawa ambao wamepata uharibifu basi tunawapa kipaumbele zaidi kuliko wale ambao wamevuna mavuno mazuri.

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Makame Ali: Kanuni ya 37 inasema kwamba Mhe. Waziri ana haki ya kulijibu swali alililoulizwa ama Waziri yeyote anayo haki ya kumuuliza Mhe. Mwakilishi.

Namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba kuna wajanja wale ambao kwamba wanakwenda kuchukua mpunga kule kwenye maduka ya kilimo na wakatumia majumbani mwao. Je, una hatua gani za kuwachukulia watu hawa wakati kule mabwana shamba wanawajua.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru na namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa majibu yake mazuri. Kwanza nataka nikiri tu kwamba ni kweli wapo watu ambao sio waaminifu na sio katika suala la kilimo tu, ni tatizo na ni janga la taifa kwamba watu wetu uadilifu umekuwa ni mdogo sana.

Tulichokifanya kupambana na tatizo hili tumetumia Jumuia za Wakulima kuweza kugawa mbegu. Kwa hivyo wanaorodheshwa watu Jumuia zao zinakaa, zinasema kwamba huyu ndiye anayefaa kupewa, anapewa hiyo mbegu kutokana na utaratibu huo ili kukimbia hilo tatizo la kutokuwa waaminifu.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri ukiachia jimbo la Ziwani hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la uingiaji wa maji ya chumvi katika maeneo mengi katika Kisiwa cha Pemba. Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuzuia ongezeko hili la uingiaji wa maji ya chumvi katika mashamba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, ni kweli tunakiri mabonde mengi ya mpunga hususan kwa Pemba yameingiwa na maji ya chumvi. Lakini hii tutambue kwamba ni kutokana na tabia ya nchi ambayo hii ipo nje ya uwezo wetu.

Vile vile tusiharibu mazingira kwa kukata miti ovyo na kuchimba yale mawe ambayo watu wanatumia kwa kujengea. Hata hivyo haya ambayo yameingia maji ya chumvi tuna uwezekano wa kubadilisha badala ya mpunga na tukasema wafuge samaki.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa nikaweza kumuuliza swali dogo la nyongeza.

(a) Mhe. Waziri umetwambia kwamba tayari kuna matayarisho ya mbegu ambayo zimeshawekwa kwa ajili ya wakulima ambao walipatwa na athari katika kipindi kilichopita. Lakini hujatwambia ni mbegu za aina gani ambazo zimetayarishwa kwa ajili ya kuwapa hao wakulima.

(b) Tunafahamu kwamba kuna mbegu za asili ambazo zilikuwa zinatumika, ambazo zilikuwa zinatoa mpunga mwingi na mzuri na wenye rutba ndani yake zikiwemo mbegu za mpunga wa ringa, supa, kibawa na nyenginezo. Je, kuna utaratibu gani wa kuweza kuziimarisha hizi mbegu ili wananchi wakaweza kuzitumia kama mwanzo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwanza nataka nikiri tu kwamba tuelewe kwanza juhudi za Serikali ilizofanya za kuweza kuwasaidia wakulima na huwa ninalirudia sana

kusema kwamba hii Serikali pekee inayotoa asilimia si chini ya 75 ya ruzuku kwa wakulima, hakuna duniani Serikali inayofanya hivyo.

La pili tumekuwa na utaratibu wa wakulima wetu kutokutunza mbegu zao, wanavuna wanakula kila kitu kwa hivyo wanaitegemea Serikali iwape mbegu. Mahitaji ya mbegu ya nchi yetu si chini ya tani 3500. Kwa bahati nzuri mara hii au kwa bahati mbaya mara hii kutokana na ukame watu wetu wamekosa mbegu kabisa kabisa, tumevuna kama asilimia 50 tu ya mazao. Ndio maana Serikali kutoka tani 250 tukaagizia tani 500 ili angalau tufidie wale ambao wamepungukiwa na mbegu. Mpaka sasa hivi kama taifa hatujakuwa na mbegu rasmi ambayo inatambulika kitaifa na ndio maana tunaendelea na utafiti ili kujua ni mbegu gani ambayo tutasema hii ni mbegu ya kitaifa ili itakapopungua mtu tunampa. Tunachokifanya tunatumia mbegu hizi tulizonazo kuweza kuzitumia. Wakulima wetu kila mmoja ana mbegu aina fulani anayoipenda yeye mwenyewe na hili ndio tatizo moja ambalo tunakutana nalo. Mwengine anapenda ringa, mwengine anapenda supa na kadhalika. Kwa utaratibu huo Serikali huwa inaagizia zile mbegu ambazo wamezifanyia *test* na kuona kwamba zinatoa mazao zaidi.

Kwa mfano sasa hivi tuna supa SSB ndio tunayoiona inakwenda vizuri ambayo tunailima hata kwenye kilimo chetu cha Shadidi na kadhalika. Kwa hivyo kwa wakulima tunawaomba zile mbegu ambazo wenyewe wanazipenda na Serikali haijaagizia basi waendelee na hizo mbegu zao, lakini kwa upande wa Serikali tunatoa zile mbegu ambazo tumefanyia majaribio na ambazo zinatoa mazao zaidi. Mimi ningeomba wakulima wakubali kutumia utaalamu badala ya kutumia mbegu za kubahatisha. Lakini nasema ni kweli kuna upungufu mkubwa wa mbegu kutokana na ukame uliotokea na wakulima wetu wamekuwa na mbegu aina mbali mbali, lakini mbegu ambayo tume- *introduce* Mhe. Spika, Makamu wa Pili wa Rais alishuhudia karibuni tulikwenda Cheju tukavuna mpunga kwa kutumia teknolojia ya Shadidi, ambayo ni maji kidogo, mbegu kidogo, mbolea kidogo na ardhi ndogo lakini mavuno makubwa sana. Ningeomba wakulima watumie teknolojia ili kuondokana na upungufu wa mbegu lakini vile vile na kuwa na mbegu bora.

Nam. 60

Ukosefu wa Maji katika Kijiji cha Kipandoni

Mhe. Asha Abdalla Mussa - Aliuliza:-

Serikali kupitia Kampuni ya Ras- el-Khaimah imechimba kisima na kujenga tangi la maji katika kijiji cha Kipandoni kwa lengo la kuwaondoshea wananchi kero kubwa ya maji safi na salama, lakini jitihada hizo bado hazijawanufaisha wananchi wa Kipandoni na Kiwengwa kwani wananchi hao wamefikia kununua maji dumu moja shs 500/-.

a) Je, Wizara haioni kuwa inawazidishia ukali wa maisha wananchi hao badala ya kuwapunguzia ukali wa maisha.

b) Je, mradi huu utamalizika lini ili wananchi hao waondokane na kadhia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwia Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa swali lake nambari 60 kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu inaelewa kwamba wananchi wa Kipandoni na Kiwengwa wana upungufu wa maji safi na salama na jitihada za kuwaondoshea tatizo hilo zimeanza kufanyika kwa kuchimba kisima na kujenga tangi. Aidha tayari imeshaandaa makisio ya mahitaji ya utekelezaji na kuingiza katika maombi ya fedha Serikalini.

b) Mradi huu utamalizika tu baada ya kupatikana fedha za utekelezaji wa shughuli hizo. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri umesema kwamba sasa hivi muna mpango kwamba mumeandaa bajeti na kupeleka Serikalini kwa ajili ya kutoa fedha kwa kumalizia mradi ule. Je, fedha hizo zinategemea kupatikana ndani ya kipindi hiki cha mwaka 2016/2017 au 2017/2018.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, matumaini yetu ni hivyo lakini kama nilivyosema katika jibu (b) pindi zikipatikana tunategemea zipatikane katika mwaka huu wa fedha *In Shaa Allah*, lakini pia kuna jitihada nyengine ambazo zinaendelea kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "B" kutafuta chanzo hicho tu pekee. Kwa hivyo ni matumaini yetu kwamba tunategemea tufanikiwe katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Spika, hatuna budi kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi kwa juhudi zake za kuwaondolea kero wananchi kwa kuwapatia maji safi na salama. Pamoja na juhudi hizo za Serikali naomba niulize kama ifuatavyo sasa.

Mhe. Spika, Serikali ilipata msaada au mkopo kutoka Ras-el-Khaimah na imechimba visima vingi lakini vingi vyao havifanyi kazi.

Je, Mhe. Waziri anaweza kutueleza kwamba ni visima vingapi vilichimbwa mradi ule wa Ras-el-Khaimah na vingapi vinafanya kazi, na je anajua kwamba miongoni ambavyo havifanyi ni visima vya Jimbo la Mfenesini kikiwemo kisima cha Chuini Ziwani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, visima ambavyo vimechimbwa na mfalme wa Ras-el-Khaimah ni visima 150 ambavyo walitupa kama msaada, lakini vile vile 17 tayari vishaendelezwa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali kutoka Hazina, na visima vyengine vitaendelea kuendelezwa najua vyengine vyote bado, lakini Serikali kila tunapopitisha bajeti tunapopata uwezo basi tunaendelea kuviendeleza kidogo kidogo mpaka hapo vitakapomalizika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi ningependa nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza lenye vifungu viwili.

(a) Mhe. Spika, na mimi kwenye jimbo langu hii kadhia au kero ya maji hasa imekuwa ni tatizo moja sugu na hadi kufika sisi viongozi kuanza kusemwa vibaya. Katika eneo la Mjonga tuna visima 3 vimechimbwa na Ras-el-Khaimah na visima hivi kwa bahati nzuri pia tayari tenki limeshajengwa pale la zege, na hivi sasa linageuka kuwa nyumba ya popo kwenda kukaa. Visima

hivi vilikuwa *line* za maji kupeleka maji katika eneo la Dunga Kiembeni ikiwezekana, Binguni pamoja na Tunguu.

(b) Sasa Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri je, katika mwaka wa fedha 2017 kwenda 18 je, huoni umuhimu wa kuhakikisha na taasisi yetu ya *ZAWA* kwamba kuondoa kadhia ya maji na kuhakikisha maeneo haya yanapatikana ya salama kwa ajili ya wananchi wetu, hasa ukizingatia kwamba Serikali imezingatia kujenga hospitali pale kubwa ya Binguni.

Katika eneo la Unguja Ukuu kuna tenki la maji ambalo linavuja na Mhe. Waziri alifanya ziara. Tenki hili maji yake yanategemewa kwa kisiwa cha Uzi pamoja na N'gambwa, Unguja Ukuu, Tindini, Kaebona na Kaepwani, Kikungwi kwa pamoja.

Ni lini hili tenki mtalibadilisha, maana gharama yake ni kubwa kuhakikisha watu wa Unguja Ukuu pamoja na kisiwa cha Uzi na N'gambwa na Kikungwi wanapata maji mazuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

(a) Mhe. Spika, ni kwamba Serikali inaona umuhimu mkubwa wa kutatua kero za maji si Jimbo la Tunguu pekee bali Zanzibar nzima kwa ujumla na ndio maana inafanya jitihada kila siku na yeye akiwa ni shahidi wa hili kuona namna gani tunaweza tukatatua kero ya maji majimboni.

(b) Kuna tenki la Unguja Ukuu la Mjonga kuna visima na tenki, ni jitihada zile zile za kuondosha kero za maji kwa wananchi wetu. Na lile tenki ambalo linavuja kama ambavyo nimewahi kusema na kutembelea kuona kwamba tunayo matenki ya namna hiyo si hapo tu Unguja Ukuu ni mengi, lakini namna ambavyo tunakuwa tunafanya lile ambalo linaweza kuzibika au kufanyiwa ukarabati tunafanya na kuhakikisha kwamba huduma ya maji haisiti tunapeleka maji *direct* kutoka kwenye visima. Lakini namna ya kuhakikisha kwamba lile lililokuwa halifai basi tunabadilisha au tunajenga jengine bora zaidi inaendelea na *In Shaa Allah* tutafika mpaka jimboni kwake.

Nam. 48

Kusita kwa Safari za Pemba – Tanga Baharini

Mhe. Ali Khamis Bakar – Aliuliza:-

Pamoja na lengo zuri la Serikali la kuwapunguzia wananchi shida ya usafiri wa baharini, mara nyingi tumeshuhudia kutokea kwa maafa ya kuzama majahazi na watu yakiwemo maafa yaliyotokea maeneo ya Kipumbwi Tanga ambapo kuna watu wameripotiwa kuzama na jahazi.

Kwa kuwa katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhan tumeshuhudia meli yetu ya MV. Maendeleo ikifanya safari ya kwenda Tanga, Pemba na Mkoani kama majaribio.

a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea meli hii isiendelee na safari zake (Pemba – Tanga) na kuwaondolea wananchi shida zao.

b) Je, Serikali ilipata hasara gani mpaka kuamua kusitisha safari hizo kwa kuzingatia taarifa kuwa meli hiyo itaanza na abiria 300 na mara ya pili abiria 500 pamoja na mizigo.

c) Je, hatuoni kutokuwepo safari hizo kunarudisha watu watumie usafiri usio wa uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe swali lake nambari 48 lenye kifungu a,b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Shirika la Meli pamoja na kuwa ni Shirika la Umma linalojihusisha na huduma kwa wananchi, vile vile limetakiwa kwa mujibu wa Sheria yetu Namba 3 ya mwaka 2013 kutoa huduma ambazo zitajiendesha kibiashara na zenye kuleta tija.

Katika mwezi wa Juni 2016 Shirika lilifanya safari *(voyages)* nne baina ya Unguja – Pemba – Tanga. Kati ya safari zote hizo zilizojumuisha usafirishaji wa abiria na mizigo, hakuna hata safari moja iliyoweza angalau kurejesha gharama za safari *(voyage costs).*

Kwa vigezo vya Shirika safari nane *(8 trips)* zilitosha kuangalia hali ya soko kama majaribio katika safari hizo. Kwa vile matokeo hayakuwa mazuri Shirika liliamua kusitisha safari zake za kawaida *(schedule voyages)* na hivi sasa linazingatia upatikanaji wa mizigo (ikiwemo saruji) ili kuweza kurejesha gharama na pindipo Shirika likithibitisha kuwepo kwa biashara hiyo, safari za Tanga zitaendelea.

b) Hasara iliyopatikana kwa safari hizo ni T.Shs 11,259,400. Hii imezingatia mapato halisi yaliyopatikana katika safari hizo ikilinganishwa na gharama zilizotumika *(voyage costs)*

c) Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi na mamlaka nyengine zinaendelea kuwashajiisha wananchi kuachana na matumizi yasiyo salama ya vyombo vya usafiri hali ambayo italiwezesha Shirika la Meli kuendelea na kutoa huduma za uhakika na salama baina ya Tanga na Kisiwa cha Pemba kwa vile safari hizo zitakuwa na tija kwa Shirika.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwaondoshea wananchi wake shida katika Taasisi zake na Wizara zake tofauti ambazo zimo katika nchi yetu. Lakini Mhe. Naibu Waziri nikiri kweli umesema kama meli yetu baada ya kufanya safari hii ilipata hasara lakini je, ni lini Serikali itatumia njia mbadala ili kuwaondoshea wananchi hawa shida hizi ambazo wanazipata katika safari yao ya Tanga - Pemba na Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, hivi sasa Serikali ipo katika mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba inaleta meli nyengine ambayo inafanana na ile Mapinduzi, na kwa hivyo nina imani kubwa sana ujio wa meli hii MV Maendeleo II itawezesha zile safari wanazosema za kwenda Tanga zitafanyika kwa sababu hii meli tuna hakika itakuwa na viwango bora na itakuwa inaweza kufanya ushindani na meli nyengine kama zile za *Azam Marine* zinavyokwenda Tanga ambayo ni meli mpya kabisa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Spika, na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri amesema Serikali inajiandaa kuwa kuweza kuleta meli nyengine ambayo itafanya kazi kwenda Tanga na Pemba. Je, Mhe.

Naibu Waziri pamoja na mikakati hiyo ambayo kuwa Serikali inajipanga ya kuweza kuleta meli hiyo ambayo itaweza kuwasaidia abiria wataokwenda Tanga na Pemba. Je ni lini hii meli ya Mapinduzi II ambayo ipo kwa ajili ya wananchi, ni lini itaanza ratiba ya kufanya safari ya Tanga - Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sote tunajua kwamba meli yetu MV Mapinduzi II ni meli kubwa na ya kisasa, na ukiangalia kwa utaratibu bandari ya Tanga maji yake ni ya kina kidogo, kwa hivyo ili kuipeleka Mapinduzi II Tanga inabidi ufanyike uchambuzi yakinifu. Hivi sasa tupo katika uchambuzi yakinifu kuhakikisha kwamba meli hii ya MV Mapinduzi inatekeleza agizo la Mhe. Rais la kufanya safari, ikiwezekana Comoro na Mombasa vile vile. Kwa hivyo atupe nafasi muda tufanye uchambuzi yakinifu baadae tutatoa maelezo kuhusu hizo hatua zitazochukuliwa katika kuhakisha kwamba MV Mapinduzi kama inawezekana inaenda Tanga, Mombasa na Comoro.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza ninashukuru kwa kukiri kwamba Wizara imeona kama liko tatizo la usafiri kati ya Pemba na Tanga kama swali la msingi alivyolijibu. Lakini kwa kuwa wananchi wa Pemba shida ya usafiri kutoka Tanga kuja Pemba ni kilio cha muda mrefu ambao wanatumia usafiri usio wa uhakika wa majahazi. Jambo hili linaipotezea Serikali nguvu kazi kubwa inayosababishwa kupotezwa roho za watu na mali zao. Na kwa kuwa kila inapotokea ajali serikali husema bila ya kufikia muafaka kulipatia suluhisho tatizo la usafiri wa baharini kati ya Pemba na Tanga.

Mimi narejea kuuliza, je, ni mikakati gani ya lazima ambayo serikali imejipangia kuhakikisha kwamba kilio hiki cha kumaliza shida ya wananchi wa Pemba wanaosafiri kutoka Tanga kuja pale Pemba kinamalizwa lini kilio hiki. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kama nilivyosema serikali imeanza kusikiliza kilio cha wananchi wa Pemba kutaka kwenda Tanga, ndio maana tukasema tuko katika mpango kabambe, na Mhe. Rais mwenyewe kasema kwamba tufanye juu chini tuhakikishe kwamba MV. Maendeleo II inaletwa Zanzibar kwa haraka sana. Kwa hiyo, kilio cha wananchi tunakijua, tumeanza kuileta Mapinduzi II ambayo ni mpya kabisa na imeanza kutatua tatizo hilo, na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu MV. Maendeleo II itakuja na kutatua tatizo hilo, na hivi sasa Azam wanatusaidia wamekuja na meli yao mpya ya *Sealink* II ambayo kila siku ya Jumamosi inakwenda Tanga. Kwa hiyo, nawaomba sana wananchi wastahamili kama

walivyostahamili mpaka ikaja MV. Mapinduzi basi na MV. Maendeleo II itakuja kwa kutekeleza ahadi zilizotolewa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM, nina hakika kabisa tumetoa ahadi na tutaitekeleza. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 109

Mazingira Hatarishi Kituo cha Afya

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein imepania kwa makusudi kuwapatia huduma za afya wananchi wake bila ya malipo kwa kuwasogezea huduma hizo karibu na wanakoishi. Na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mkopo wa Benki ya Dunia ambao ni dhima ya jasho la wananchi wa Tanzania ilitumia Tshs. 350 milioni kujenga kituo kikubwa hapo Mzambarautakao.

a) Je, Mhe. Waziri umeshawahi kutembelea Kituo cha Afya cha Mzambarautakao na kuona kilivyoathirika katika kipindi hicho kifupi mara baada ya kukabidhiwa.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kuathirika kwa majengo hayo ambayo kwa macho yana haiba nzuri.

(b) Je, utakubaliana na mimi wazo la kuondoa miti mikubwa ya jamii ya miembe na mikeshia ambayo ni hatarishi kwa majengo na wananchi wote ambao wanafika hapo kupata huduma.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako Tukufu swali lake Nam. 109 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Mwakilishi kwa jinsi ya tabia yake ya kuvitembelea vituo vya afya vilivyomo katika jimbo lake, na baadae kutuona na kutupa changamoto walizozibaini.

Mhe. Spika, mimi binafsi nimekitembelea kituo hiki na kuona athari zilizojitokeza ambazo ni kupasuka kwa baadhi ya kuta na sakafu za kituo hiki.

Kutokana na uchunguzi wa awali uliofanywa na wizara yangu imeonekana kupasuka pasuka huko imetokana na aina ya ardhi katika eneo hilo ambapo hata baadhi ya nyumba za majirani wa kituo hicho zinaonekana kuwa na athari hizo hizo. Hata hivyo, wizara yangu imekusudia kuendelea na utafiti zaidi kwa kuwatumia wataalamu ili kubaini chanzo cha athari hizo zilizojitokeza kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, suala la kuiondosha miti ikiwemo mikeshia na miembe iliyo karibu na jengo hilo tunalizingatia sana kwa kushauriana na wizara inayohusika ili kuona kama kuna haja ya kuiondosha kabisa miti hiyo au kuipunguza, kwani miti ni afya na uhai wa binadamu na viumbe wengine. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

(a) Pamoja na kwamba anasema miti ni mizuri kwa afya, lakini katika utafiti wangu nilipokwenda nimeona kwamba mizizi ya miti hii mikubwa ndio miongoni mwa athari iliyojitokeza pamoja na kwamba ardhi nayo inasababisha, lakini mizizi ya miti hii ndio sababu moja wapo. Kwa hivyo, ndio nikashauri kuwa miti hii ni vyema iondolewe au itafutwe miti mengine mbadala ambayo haitakuwa na nguvu kama hiyo.

b) Je, Mhe. Naibu Waziri anajua kwamba kituo hiki kwa vile amekitembelea muhudumu aliyepo pale ni mwanamke tena mzee, je yuko tayari aweze kupeleka muhudumu wa kiume pale kuweza kusaidia usafi wa mazingira ya kituo kile kilichopo cha Mzambarautakao. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama tulivyosema katika jibu la msingi kwamba miti ni uhai na miti ni afya. Naendelea kukuomba na kukushauri kwamba usubiri tutakaa na wataalamu wanaohusika na mambo ya miti, tutashauriana na suluhisho litapatikana kwamba ing'olewe kabisa miti ile au ipunguzwe kwa manufaa ya wananchi wa eneo lile. Kama tunavyojua kwamba pahali ukiondosha miti kabisa na mvua pia inakimbia. Miti pia ni muhimu na jengo letu pia ni muhimu, tutaangalia lipi la busara lifanyike ili kituo chetu kiendelee kutumika.

Mhe. Spika, kuhusu kuwepo kwa mfanyakazi yule ambaye kama ulivyoeleza kuwa ni mtu mzima, hilo wizara tumeshaliona na muda mfupi ujao tunaweza

tukafanya mabadiliko ya yule mama kuondoka na kuingia mwengine au kuongezewa mtu mwengine wa ziada. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri Hospitali ya Micheweni ni hospitali ya Wilaya, ulitembelea lini kuona eneo la wodi ya wazazi iliyoko Micheweni kuona kwamba kuna tatizo la mlango wa kuingilia kwenye wodi ya wazazi. Mlango ule je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako umeshautengeneza, na kama haujatengenezwa utatengenezwa lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Hospitali ya Micheweni mara ya mwisho nimetembelea Januari kwenye tarehe 14 au 15. Lakini na mlango ambao aliouzungumza pia nimeuona na nimeutolea maelezo na kuagiza wafanyakazi akiwemo Afisa Mdhamini ili ufanyiwe marekebisho. Juzi wakati yanatayarishwa majibu haya niliulizia na wakaniambia kwamba wako katika *final process* za kukamilisha ili upatikane uende ukawekwe katika sehemu husika.Ahsante.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa lengo lile lile la Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inaongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein kuwapelekea huduma za karibu wananchi wa nchi yetu, kuna kituo ambacho kimejengwa ndani ya jimbo langu zaidi ya miaka 12 sasa katika kijiji cha Kibokoni, kituo kile bado hakijafunguliwa. Je, ni lini wizara yako itathamini nguvu zile za wananchi waliojenga kituo kile cha afya kwa kuwafungulia ili wapate huduma ya karibu na wao wasipate usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kituo cha Kibokoni tumeshakiona na tatizo kubwa liliopo pale ni kwamba kama tatizo tunavyolifahamu ni *shortage of staff* tuliyonayo. Lakini wakati wowote kuanzia sasa tukipata ruhusa ya kuajiri wafanyakazi wa afya wa kada zote basi kituo kile tutakifungua na kianze kutoa huduma kwa wananchi kama lengo la serikali lilivyo. Mhe. Spika, hata hivyo naomba nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi kwamba watu wanaoishi karibu na kituo kile wanapata huduma vizuri katika hospitali ya Fidel Castro na vituo vyengine vya jirani. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa maswali umekwisha na kwa bahati hatuna tangazo lolote ambalo linahitaji kutolewa, lakini naomba mimi

nitoe moja tu na hili zaidi nilielekeze kwenye ile kamati ambayo inashughulikia masuala ya michezo; kwa maana ya mpira wa miguu na mpira wa pete, kwamba tumezungumza na Bunge la Jamhuri ya Muungano kutakuwa na mchezo wa kuadhimisha sherehe za Muungano. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mjiandae kwa kufanya mazoezi, tunategemea kwamba tunafanya mazoezi ili muda huo ukifika tuweze kwenda kukabiliana na wenzetu tukiwa katika hali nzuri. Baada ya tangazo hilo fupi sasa naomba tuendelee na shughuli zinazofuata.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 42 na 43, Mhe. Spika kama utaniruhusu niisome au ndio kanuni mpya hazijatoka…

Mhe. Spika: Nakuruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante.

Mhe. Spika, "Baada ya muda wa maswali kumalizika, Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kwa Baraza liakhirishe shughuli zake zinazoonesha katika orodha ya shughuli ya Baraza na lijadili jambo la dharura na muhimu kwa umma kwa ruhusa ya Spika".

Lakini nakuja kifungu cha 43 kinasema Kiongozi wa shughuli za serikali anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo serikali ina wajibu na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa...

Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba wala sio kwa nia mbaya kabisa tupo hapa kwa niaba ya wananchi, na wananchi ndio waliotutuma kuja kueleza matatizo yao ndio wametuchagua. Kadhia zilizotokea kuna mambo mawili, hivi karibuni Waziri wa Kilimo kwa nia njema kabisa amezungumza kuhusu suala la upungufu wa mchanga, na huku Waziri wa Ardhi anataka kufuta viwanja, ambapo tofali moja sasa hivi linauzwa shilingi 2600 baada ya kuwa kuna upungufu wa mchanga kutoka shilingi 700.

Hoja yangu na vile vile waziri anaagiza kuthubutu mpaka mchanga utoke Tanzania Bara, elimu haijatolewa kwa wananchi wetu vya kutosha. Tumeshuhudia tukipata maradhi ya kipindupindu vyombo vya habari

vinavyotangaza kuna hili na hili. Lakini itakuwaje gharama za ujenzi zimepanda kiasi kama hiki huku Waziri wa Ardhi anataka kuja kufuta viwanja, hili ni jambo ambalo tutarudisha nyuma wananchi wetu.

Kwa hiyo, Mhe. Spika nataka muongozo wa kiti chako katika mambo mawili haya, serikali ije na majibu sahihi kabla ya kikao hiki hakijamalizika au tujadili jambo hili la dharura kwa maslahi ya wananchi wetu. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nataka muongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku nimesikiliza huo muongozo ambao unaoutoa na ni kweli ni muhimu, lakini umuhimu wake zaidi ni kwamba wananchi waweze kupata elimu kutoka kwa serikali, waelimishwe. Kwa hiyo, mimi nitaishauri sana serikali ndani ya mkutano huu waweze kututayarishia kauli yao kuhusiana na masuala hayo ambayo umeyagusia kuhusu mchanga na viwanja, halafu baadae waje watutolee humu sote tutafaidika pamoja na wananchi na hiyo elimu ambayo itakuja kutolewa wakati huo na serikali. Kwa hiyo, mimi niitake serikali ili mje mtoe kauli hapa ndani ya mkutano huu mtatafuta muda mtanijuilisha Spika, halafu nitaruhusu kwa kutoa nafasi ili serikali ije itoe maelezo. Nashukuru sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa imani yako na ubinadamu wako uliouonesha wa hali ya juu Mwenyezi Mungu akujaalie kila la kheri.

Mhe. Spika: Ahsante.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya Mwaka 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya Mwaka 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, baada ya shukurani zangu kwako naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa wanayotupa katika

kutekeleza kazi zetu za kila siku katika Baraza lako tukufu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika naomba sasa niwasilishe mswada huu.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, madhumuni ya kuanzishwa mswada huu ni kufuta sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya mwaka 1992 na kuunda sheria ya kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo ili kuweka mfumo bora zaidi wa usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mswada huu umekusudiwa kuimarisha utendaji na ufanisi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kuweka bayana muundo na majukumu ya Afisi ya Tume.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, mswada huu una sehemu kuu zifuatazo:

Sura ya Kwanza, inaelezea masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha masuala ya jina, muda wa kutumika na ufafanuzi wa baadhi ya maneno;

Sura ya Pili, inaelezea kuanzishwa kwa Tume majukumu yake na uwezo iliyopewa;

Sura ya Tatu, inaelezea kuanzishwa kwa Afisi ya Tume ya Uchaguzi na kazi zake;

Sura ya Nne, inaelezea masharti ya fedha za Tume;

Sura ya Tano, inaelezea masharti mengineyo yanayohusiana na sheria hii ikiwemo uandaaji wa ripoti za Tume, makosa na adhabu na uwezo wa Tume katika kutunga kanuni.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, umuhimu wa mswada wa sheria hii.

Mhe. Spika, umuhimu wa mswada huu unatokana na haja ya kuzitafutia ufumbuzi kasoro mbali mbali za kisheria na za kiutendaji zinazojitokeza katika usimamizi wa masuala ya uchaguzi. Miongoni mwa kasoro hizo ni kama ifuatavyo:

a) Kuwepo kwa mgongano wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi na Katiba ya Zanzibar hasa katika muundo na uteuzi wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi. Sheria ya Tume inatoa mamlaka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuteua Mwenyekiti

na Wajumbe wa Tume kama atakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria. Wakati muundo wa Tume uliopo katika Katiba unamtaka Rais katika uteuzi wa baadhi ya wajumbe kushauriana na kiongozi wa shughuli za serikali na kiongozi wa upinzani katika Baraza la Wawakilishi;

b) Kati ya vifungu 11 vya Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya mwaka 1992 ni vifungu vitatu tu ambavyo havikuathiriwa na marekebisho ya nane ya Katiba ya Zanzibar;

c) Kuwepo kwa mgongano wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi katika uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo. Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Uchazugi kila Katibu Tawala wa Wilaya atakuwa msimamizi wa uchaguzi wa majimbo ya Wilaya yake, ambapo ni kinyume na maelekezo ya sheria ya uchaguzi ambayo inatoa mamlaka kwa Tume ya Uchaguzi kuteua wasimamizi wa majimbo kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa sifa zilizowekwa na Tume;

d) Kutokuwepo kwa mfumo unaotambulika kisheria wa uendeshaji wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi, idara zake na Afisi za Tume ya Uchaguzi za Wilaya;

(e) kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria kunaiwezesha Tume ya Uchaguzi kutoa vibali kwa waangalizi wa uchaguzi, na kutumia majengo ya serikali au binafsi kwa shughuli za uchaguzi,

(f) kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria unaoiwezesha Tume ya Uchaguzi kuunda kamati za ushauri kwa masuala ya uchaguzi na mambo mengineyo,

(g) kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria wa kuratibu na kulipa fidia kwa Wajumbe wa Tume na watendaji wa uchaguzi wanapopatwa na madhara wakati wa utekelezaji wa shughuli za uchaguzi.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, mswada huu wa sheria utasaidia kuondoa kasoro hizo na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Masuala Muhimu yaliyozingatiwa:

Mhe. Spika, katika kusaidia kuondosha kasoro zilizotajwa pamoja na kuongeza ufanisi wa Tume, mswada huu wa sheria umependekeza na kuzingatia utaratibu wa utekelezaji katika maeneo makuu yafuatayo:-

1. Kuondosha mgongano wa sheria iliyopo na Katiba ya Zanzibar

Mhe. Spika, kifungu cha 119(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinaelekeza kuundwa kwa Tume ya Uchaguzi yenye wajumbe saba, ambapo wanne kati yao wapatikane kwa kuteuliwa na Rais baada ya kushauriana na vyama vya siasa. Wakati huo huo Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam.9 ya mwaka 1992 kifungu cha 3 kinampa uwezo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuteua wajumbe wote saba wa Tume akiwemo mwenyekiti bila ya kushauriana na mamlaka yoyote.

2. Kuimarisha muundo wa kitaasisi

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa Afisi ya Tume ya Uchaguzi pamoja na vitengo vyake kutaifanya sekretarieti ya Tume ya Uchaguzi inayoongozwa na Mkurugenzi itekeleze majukumu yake ambayo hayakuainishwa katika sheria ya Tume ya Uchaguzi. Hivyo, mswada huu unapendekeza kuanzishwa vitengo mbali mbali vya Tume vitakavyorahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

3. Kuanzisha Ofisi za uchaguzi wa wilaya

Mhe. Spika, sheria iliyopo sasa haikuzingatia uwepo wa ofisi ya kudumu ya uchaguzi wa wilaya, mswada huu wa sheria umezingatia kuanzishwa ofisi hizo ambazo zitasimamiwa na maafisa wa uchaguzi wa wilaya na kuainishwa majukumu yao.

4. Uundwaji wa Kamati za Ushauri kwa masuala ya uchaguzi

Mhe. Spika, sheria iliyopo sasa haikuzingatia uwepo wa kamati za ushauri kwa masuala ya uchaguzi, ambazo zina jukumu la kuishauri Tume katika masuala mbali mbali ya uendeshaji wa uchaguzi. Mswada huu wa sheria umezingatia uanzishwaji wa kamati hizo ili kuhakikisha kunakuwepo ushirikishwaji wa wadau.

5. Kuipa Tume uwezo wa kutumia majengo ya serikali au binafsi kwa shughuli za uchaguzi

Mhe. Spika, sheria iliyopo hivi sasa haikuzingatia kuipa mamlaka Tume ya Uchaguzi kutumia majengo ya serikali au binafsi kama vile skuli na kumbi za mikutano kwa shughuli za uchaguzi. Mswada huu wa sheria umeipa uwezo Tume ya Uchaguzi kutumia majengo ya serikali au ya binafsi baada ya mashauriano na wahusika wa majengo hayo.

6. Kuainisha makosa na adhabu.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, sheria iliyopo hivi sasa haitoi adhabu kwa mtu yeyote atakayekwenda kinyume na maelekezo ya vifungu vya sheria hiyo. Hivyo, mswada huu wa sheria umependekeza kuwepo na vifungu vya makosa na adhabu.

Hitimisho:

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo hayo sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili na kuuchangia mswada huu ili tupate sheria iliyo bora zaidi. Baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ili aje atoe maoni ya Kamati hapa.

Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma hotuba hii ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya mwaka 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2016.

Mhe. Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa utukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kufika hapa kujumuika kwa pamoja kwa lengo la kuendelea na majukumu yetu.

Pili naomba kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam.9 ya 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, majukumu, uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wa Tume ya Uchaguzi kwa mashirikiano yao makubwa wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku, hususan katika kuupitia na kuuchambua mswada huu adhimu. Sambamba na shukurani hizi napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana wahusika mbali mbali waliojitokeza katika kamati yetu na kuwasilisha maoni yao kwa lengo la kuufanya mswada huu uwe bora zaidi. Kwa kuthamini mchango wao ndio maana kila tunapokuwa na miswada huwa tunawaalika wahusika hao ili waweze kutusaidia kuichambua miswada hiyo.

Mhe. Spika, Mswada huu wa Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ni muhimu sana, kwani umekuja kuweka misingi bora ambayo itakuwa inaenda sambamba na Katiba ya Zanzibar ambayo ndio iliyoanzisha tume hii. Hivyo, mswada huu umekuja kuanzisha uwepo wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itaongozwa na Mkurugenzi ambaye atakuwa Katibu wa Tume ya Uchaguzi. Pia Mswada huu wa Sheria umeanzisha Afisi za Tume za Wilaya ambazo zitakuwa kwa kila wilaya, zitakuwa na jukumu la kuhakikisha uchaguzi au kura ya maoni zinaendeshwa katika misingi ya demokrasia na utawala bora.

Mhe. Spika, kamati yangu baada ya kuupitia mswada huu imependekeza baadhi ya marekebisho ambapo naamini waraka wa marekebisho hayo kila Mjumbe ameshapatiwa nakala yake. Hivyo, ni vyema tukaupitia kwa makini ili tuweze kutoa mapendekezo zaidi kwa lengo la kuufanya mswada huu muhimu kuwa bora zaidi. Baadhi ya marekebisho ambayo Kamati imependekeza ni kuongezwa kwa kifungu kidogo cha (3) kitakachosomeka “Afisa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa msimamizi wa jimbo au majimbo katika Wilaya yake katika kipindi cha Uchaguzi”.

Mhe. Spika, sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa uchaguzi katika majimbo ambao utafanywa na Afisa huyo wa Wilaya ambaye atakuwa ni Afisa wa Tume, kinyume na utaratibu uliopo sasa ambapo msimamizi wa uchaguzi katika majimbo anakuwa sio mwajiriwa

wa Tume, hivyo anapotenda kosa lolote Tume haina mamlaka ya kumuwajibisha.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 26(2) Kamati imependekeza kuingizwa neno “zitawasilishwa” baina ya neno “fedha” na neno “kwa”. Sababu ya marekebisho hayo ni sheria hii kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kumaliza ukaguzi wa Hesabu za Tume kuwasilisha ripoti yake kwa waziri.

Mhe. Spika, ni wazi kuwa utekelezaji wa Sheria hii hautakamilika bila ya kutungwa kanuni zake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mara baada ya Baraza lako tukufu kupitisha Sheria hii na kusainiwa na Mhe. Rais, Kanuni za Sheria hii zitungwe haraka iwezekanavyo kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

Mhe. Spika, kazi ya kuupitia mswada huu tumeifanya kwa mashirikiano ya pamoja baina ya Wajumbe wa Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa ambao ni Wajumbe wenye kupenda kujituma na kufanya kazi kwa bidii ya hali ya juu.

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa kuwataja majina Wajumbe hao kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe
5.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
6.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
7.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
8.	Ndg. KassimTafana Kassim	Katibu
9.	Ndg. Maryam Rashid Ali	Katibu

Mhe. Spika, mwisho kabisa nachukua nafasi hii kukushukuru tena kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya kamati juu ya Mswada huu ulio mbele yetu, lakini pia kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini. Hivyo, naomba waupitie, waujadili, wakosoe na hatimaye kuupitisha mswada huu muhimu kwa ajili ya kukuza demokrasia na maendeleo katika nchi yetu, na hatimaye kuwa Sheria itakayotumika katika kuendesha shughuli za Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla, Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Waheshimiwa Wajumbe sasa tunaanza kuchangia lakini nina wachangiaji wachache sana, kwa hivyo kama kuna mtu anahitaji kutoa mchango wake kwenye mswada huu ningeomba basi alete jina lake ili niweze kumtambua.

Sasa mchangiaji wetu wa mwanzo kwa leo atakuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali akifuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Rashid Makame Shamsi ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza hili tukufu nikiwa niko salama pamoja na wenzangu wote kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam.9 ya mwaka 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya Mwaka 2016.

Mhe. Spika, mimi naipongeza serikali yetu kwa kujua kwamba kila jambo lina taratibu zake za kisheria, Tume yetu ya Uchaguzi ilikuwa inafanya kazi zake kutokana na mambo mbali mbali, lakini pia wakati mwengine palikuwa na matatizo ya kisheria bila ya kujua kwamba inakwenda ambako hatutegemei. Kwa sheria hii ya kuanzisha afisi rasmi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar tunaamini Tume itakuwa vizuri zaidi na itakuwa na wajibu wa kufanya kazi zake ipasavyo kwa kujua kwamba sheria inawalinda pale panapotokea tatizo ambalo hawakulitegemea.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ni chombo muhimu katika nchi yetu na chombo hiki kila wakati kinataka kupewa uwezo wa kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria zetu bila ya kutetereka. Lakini tu, naipongeza Tume yetu kwa kufanya kazi zake vizuri huko inakotoka na kujua wajibu wao. Pamoja na majukumu mazito waliyokuwa wanapambana nayo, lakini wameweza kutufikisha hapa kwa salama na amani na tunaendelea na kazi zetu bila ya matatizo.

Kwa hivyo, nampongeza Mwenyekiti wa Tume, wajumbe wake, Mkurugenzi pamoja na watendaji wote kwa kuhakikisha kwamba tuko salama katika

shughuli zetu hadi leo na sisi tunatunga sheria hii kwa maslahi ya kuiweka vizuri afisi hiyo ya Tume kwa ajili ya kazi zake za kila siku.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi itakuwa na Mkurugenzi ambaye kisheria atateuliwa na Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia Mkurugenzi huyo na yeye atakuwa ni kiongozi katika kurugenzi mbali mbali za wilaya zetu na kwa baadhi ya maeneo fulani katika kazi zao, ili kuwa kiongozi kwa kuelekeza na kuweka vizuri mambo ambayo yanaonekana yanakwenda sivyo. Kwa hivyo, mimi nilipongeze hili, ni zuri hasa tukizingatia kwamba Tume ya Uchaguzi inakwenda katika muelekeo wa ushindani katika mambo yetu ya kazi zetu nzuri.

Jengine ni kwamba Tume ya Uchaguzi inafanya kazi katika mazingira magumu na hasa siku za uchaguzi au siku ya kuboresha daftari letu au kuliongezea nguvu, huwa panatokea matatizo wakati mwengine wasiyoyategemea. Kwa hivyo, mimi nimeona kifungu ambacho kimenipa faraja nzuri awe na fidia, kwenye masharti na mengineyo kifungu cha 28, pawe na fidia ya wajumbe au watendaji wa Tume ya Uchaguzi pindi wanapokwenda kazini kwao. Mwenyezi Mungu awaepushie lisitokee, ikiwa wamepatwa na ajali au mtihani ambao hawakuutegemea basi pawe na fidia ya kuwalipa na kuwaongezea kitu, kwa kuwapa imani kwamba hili lililotokea limetokea katika nyanja za kazi zao, basi ni vyema na wao kuwezeshwa au kupewa uwezo wa kujikimu katika shughuli zao.

Mhe. Spika, Tume itakuwa na kazi nyingi za kufanya. Ukurasa wa 227 kwa huku itakuwa Sura ya Pili pana majukumu. Kutakuwa na "Kuanzishwa, Majukumu na Uwezo wa Tume". Kutakuwa na masharti ya kuhusiana na kuanzishwa na muundo wa Tume kama yalivyoainishwa katika Katiba. Tume itakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kusimamia na kurekebisha mwenendo mzima wa uchaguzi na kura ya maoni.

Mhe. Spika, hili ni suala zuri na zito, tuamini kwamba wenzetu hawa huwa wanapata shida na huwa wanapata matatizo mengi wakati mwengine, huwa wanazongwa. Kwa hivyo, kwa kuwa kumeanzishwa sheria hii ambayo inawapa uwezo wa kusimamia na kuendesha mwenendo mzima wa uchaguzi na kura ya maoni nasema wao ndio wenye kutoa matangazo ya mwisho. Matangazo kwenye vituo, kwenye majimbo au wilaya, lakini pia mpaka Tume ya Uchaguzi ya Taifa hawa ndio wenye kutoa matangazo. Naomba sana vyombo vyetu vinavyohusika au Tume yenyewe itoe taaluma nzuri kwamba uchaguzi unasimamiwa kisheria na uchaguzi unasimamiwa kutokana na mwenendo wa

kisheria. Vile vile basi mwenye kutoa taarifa ile awe mtu ambaye karuhusika kutokana na sheria hii.

Mhe. Spika, mara nyingi huwa tuna vyombo vyetu vya mitandao huku ndiko kunatokea kadhia kubwa sana katika nchi, taarifa haijatoka huku yameshatoka mambo ambayo hayakutegemewa na kusababisha zogo katika baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, mimi ningeomba sana hili liangaliwe kwa maslahi ya usalama wa uchaguzi wetu na kuhakikisha kwamba tunakuza taratibu zetu nzuri za kuhakikisha kuwa Tume ndio yenye mamlaka ya mambo yote katika uchaguzi huu.

Taaluma ya Elimu. Mheshimiwa elimu ni sura mojawapo ya kuhakikisha kwamba, ukitoa taaluma nzuri na elimu nzuri kwa wapiga kura na wananchi wote kwa ujumla, basi mambo yatakwenda vizuri na yatakuwa yanaeleweka, kwa sababu wananchi wengi Mheshimiwa wanajua siku ya kwenda kupiga kura na kumaliza kura yao basi, lakini huku kumbe kuna nyanja chungu nzima za kutoa taaluma ambayo inaongoza uwezo na utaratibu mzima wa kupiga kura uwe moja, mbili, tatu.

Niiombe sana Tume yetu Mheshimiwa baada ya kupita Sheria hii, wasichoke, waendeleze zaidi kutoa taaluma kwa kuhakikisha kwamba hiyo ndiyo hali halisi inayotakiwa katika nchi yoyote juu ya wapiga kura.

Mhe. Spika, kuna taarifa nyengine kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kuendeleza daftari la kudumu la wapiga kura.

Mhe. Spika, mara nyingi inatokea matatizo baadhi ya wakati, daftari ni halali la kuongezwa wapiga kura wapya, lakini inatokea hitilafu wakati mwengine fulani au vijana kama kumi, ishirini au hamsini wamepigwa picha na kila kitu, lakini picha ile unapokwenda katika matokeo unaambiwa picha zile zimeharibika. Anatafuta suti au njia nyengine kwa siku nyengine anakwenda kupigwa tena. Taratibu zinazojitokeza Mhe. Spika, huwa malalamiko yanatokezea mtu huwa na vitambulisho vitano au vinne. Hii ninaiomba Tume iwe makini sana kuliangalia suala hili, kwa sababu hili tunalisema sisi tumeshuhudia.

Mimi jimboni mwangu, ninatoa mfano mimi, tulimkamata kijana fulani ana sura zaidi ya tano, yaani ana majina matano tofauti, sura ile ile kama Shihata ndiyo Shihata lakini huku ukienda kavaa suti, huku kavaa shati la rangi

nyengine, huku kavaa kitenge, kavaa kofia ya Doholo hayupo. Sasa Mheshimiwa ile yote ni kubabaisha, lengo kwamba asijulikane na majina tofauti.

Sasa tuulize tu, kuna ujanja naomba radhi kusema hii sina uhakika nalo lakini linaweza kutokea. Hawa watu kuna wajanja maalumu wana vitendea kazi maalumu vya kutafuta vitambulisho vya Mzanzibari na kwenda ku-*lobby* katika Tume ya Uchaguzi kupigwa picha, leo kavaa shati hii, kesho hii. Je, imetokea katika majimbo mbali mbali mtu yule yule akitoka Kijitoupele anakwenda Kwahani, akitoka Kwahani anakwenda Mpendae huo ni mfano.

Mhe. Spika, ninaiomba Tume iwe na watu madhubuti sana wa kuyaangalia haya. Hilo Mhe. Spika, ndiyo moja litakalotupa somo zuri juu ya wananchi wetu kuwa wanajitambua na kufanya kazi zao ipasavyo.

Mhe. Spika, ninaloliomba tu kwa Tume, Tume ndiyo yenye dhamana ya uchaguzi, Tume ndiyo yenye dhamana ya kura ya maoni, pindi inapotokea kura ya maoni inakuja kutokana na jambo fulani lipelekwe katika mambo ya kura. Lakini kubwa ninaloliomba Mhe. Spika, wenzetu wa Tume wapewe uwezo wa kutosha, wana kazi ngumu, wana majukumu mazito. Kwa hivyo niseme pindi linapotokea haja yoyote ya kufanya kazi zao, basi ni vyema wakaongezewa nguvu ili kazi zile ziende vizuri kwa kufanikisha uchaguzi wetu kwa kila baada ya kipindi kinachofika. Zuri zaidi Tume ya Uchaguzi inasimamia kura za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kura za Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kura za Mheshimiwa Diwani, hayo yote kuhakikisha kwamba wao ndiyo dhamana wa nchi hii na dhamana ya kufanya kila kitu kiende vizuri ili tupate matokeo ambayo yanastahiki katika shughuli zetu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa samahani una dakika tano zimebaki, lakini naomba nimwite kwanza Mwenyekiti, baada ya hapo utamalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti karibu.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunaendelea.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea na mchango wangu niseme tu kwamba ninaiombea sana fedha Tume ya Uchaguzi, na ninaiombea sana majukumu

yake yaende vizuri, kwa sababu wakiwezeshwa kufanya vizuri basi hapo ndiyo tutakwenda vizuri katika kazi zetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza kazi zetu hizi kwa Sheria yetu hii, Sheria imesema kutakuwa na maeneo maalumu kwa kazi maalumu za uchaguzi, yaani majengo maalumu yatatumika. Majengo ambayo yatakayotumika yatakuwa ni majengo ambayo yamekubalika mfano Maskuli, hapa nimeona labda maeneo ya wazi ambayo yatajengwa kama mahema ili kama halimo naomba liongezwe, kwa sababu unakwenda katika maeneo mengine au pahala pengine panakuwa na ufinyu na vituo vipo vingi. Si vibaya kwa mfano kama uwanja wa mpira wowote, pazuri panaweza kujengwa mahema pale chaguzi zetu zikaenda salama bila ya matatizo.

Lakini ni kosa kwa Sheria yetu hii hakuna kitu kitakachokubalika kufanyika ndani ya jengo la Chama fulani. Hilo litakuwa ni kosa, na naomba Sheria ifanye kazi yake juu ya kuliangalia hili kwa sababu tunaamini kwamba Tume ipo huru haina chama, ipo katika majukumu yake kihalali kabisa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba hivi sasa tumo katika marekebisho ya Sheria yetu hii na kuifanya Tume kuwa Ofisi yake, lakini Ofisi ina mambo yake. Ningeomba sana tuangalie kwa kuweka vizuri haya tunayotegemea kuyaleta kwa ajili ya maendeleo ya shughuli zetu hizi.

Sheria ipo nzuri, na niwaombe Waheshimiwa wenzangu tuiangalie tuichangie ili Sheria yetu hii tuweke vizuri kwa ajili ya watendaji wetu wasipate mitihani ambayo hatuitaki itokee, hasa tukizingatia kwamba wakati mwengine mtu hujisahau.

Mimi nimekwenda pahala fulani katika mambo yetu ya uchaguzi mfano, lakini inaonekana nimeshashindwa, basi ninaanza kutoa kauli ambazo si nzuri. Tume iwe na uwezo wa kumdhibiti mtu yeyote atakayekwenda kinyume ikiwa kenda kuomba kura za Uwakilishi, Udiwani hata Urais, asianze kujitangazia jambo ambalo Tume haijatoa. Tume ndiyo yenye mamlaka ya kumtangaza Shihata, Tume ina mamlaka ya kumtangaza Diwani fulani, Tume ina mamlaka ya kumtangaza Rais fulani na siyo mwengine. (*Makofi*).

Kwa hivyo niombe tu kama kuna mitandao inafanya kazi zake hizo, Tume itoe tahadhari kabisa iwe na kifungu maalumu cha kusemwa tu kwamba yeyote atakayetangaza kama ilivyo, atakayejitangazia ushindi, Mwakilishi wa Kijitoupele nimeshinda mimi wakati taarifa haijatoka, basi nidhibitiwe. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na ninaamini kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele wanaojali maendeleo ya jimbo hilo na nchi yetu kwa ujumla, tunaiunga mkono au ninaiunga mkono Sheria hii, na ninawaomba wenzangu waichangie ili tuweke vizuri kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali. Sasa ni zamu ya Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa kutunga Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nije tu moja kwa moja Sura ya Kwanza katika masharti ya utangulizi kwenye Kifungu cha pili chenye kutoa ufafanuzi wa maana mbali mbali ya mambo yaliyokuwemo ndani ya Mswada huu.

Kuna kifungu kinachosema uchaguzi maana yake, katika marekebisho waliyotuletea Kamati imeandikwa neno uchaguzi itakuwa maana yake ni kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Uchaguzi, Sheria ambayo tumeifuta na kutunga Sheria hii ya Kuanzisha Tume ya Uchaguzi.

Sasa kidogo nikawa ninapata mashaka pa kuanzia, kwamba tafsiri yake tuipate kwenye Sheria ya Uchaguzi wakati hapa tunaanzisha Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Sasa kidogo tunamuomba Mhe. Waziri pia hapa aje kutupa maelezo ya ufafanuzi wa ziada wa kifungu hichi, kwa sababu hapa panapo maelezo ya Kamati hayajatutosheleza. Lakini pia kwangu mimi kwa sababu chaguzi zimetajwa katika tafsiri huku mbele lakini tafsiri pia nayo haikujitosheleza.

Kuna kifungu kinasema cha Sekretarieti, maana yake ni Sekretarieti ya Tume itakayoanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 18 cha Sheria hii, ikisha kuna (a), (b), (c) hadi (e). Zimeoneshwa chaguzi hapa. Sasa nilikuwa ninasema labda tafsiri yake kwangu ianzie kwenye Kifungu (a), (b) mpaka (e) iwe ni sehemu ya tafsiri za chaguzi hizi moja kwa moja isomeke hivyo.

Kama sijapata maelezo ya kutosha, sasa hayo ndiyo maoni yangu. Lakini pia katika tafsiri ya maneno huku ndani katika kuupitia Mswada huu kwenye Kifungu cha 12(1) kuna neno muhuri na nembo haukutolewa tafsiri yake katika uchambuzi au ufafanuzi ule ambao uliokuwa unatangulia huku mbele. Sasa

ningependa basi na tafsiri ya neno muhuri na nembo basi pia yatangulie kama ulivyotolewa ufafanuzi wa maelezo ya vitu vyengine huku ndani ya Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, niende sasa katika kuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwenye Kifungu ambacho kinaelezea Sekretarieti Kifungu cha (d) na Kifungu (e) tupate tu maelezo ili kuweka sawa uchambuzi wa Mswada kuwa tupate tafsiri ya neno uchaguzi mdogo, tupate tafsiri ya uchaguzi wa marejeo ili kuweka sawa tu, ninasema utaratibu wa kwenda vizuri na Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Sura ya Tatu sasa. Kifungu cha 11 (2), naomba nikisome, "Afisi itakuwa ni taasisi inayojitegemea, endelevu na yenye muhuri wake na jina kila itakapokuwa na uwezo wa" kuna *list* inayotoka (a) mpaka (d) sitaki kukariri huko. Lakini naomba pia kwa mujibu wa Kifungu cha Katiba ya Zanzibar Kifungu 119(9), naomba pia nikisome ili kuweka sawa haya ninayotaka kuyasema,

"Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake, Tume ya Uchaguzi itakuwa na Idara inayojitegemea na Mtendaji Mkuu wake atakuwa ni Mkurugenzi wa uchaguzi ambaye atateuliwa na kufanya kazi zake kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi".

Sasa katika Kifungu hichi kimeeleza pia Afisi itakuwa ni taasisi inayojitegemea. Sasa wakati ninapitia huu Mswada ninaona hii Afisi haijitegemei, ile *full autonomy* haipo. Kwa sababu kama inajitegemea basi la kwanza tungepata huu muundo wake wa utumishi, lakini la pili tungepata kuona *scheme of service* inaonekana, lakini la tatu ile Tume ya Ajira yake yenyewe. Sasa ukiangalia tu utaona huku Mkurugenzi na watumishi namna wanavyopatikana wote wanapelekwa kwenye Tume ya Utumishi Serikalini.

Sasa kama Idara inayojitegemea, huku watumishi unawapata katika eneo jengine, tunafika pahala ile tafsiri ya Sheria tunazozitunga kwa mujibu wa Katiba hii tunayoifanyia kazi, mambo mengine yanafuata huo utaratibu lakini kuna mambo mengine yanatoka nje ya utaratibu wa Sheria. Sasa katika majibu basi tupate tafsiri nzuri ili twende sambamba na hichi ambacho ninakizungumzia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane pia katika Kifungu kile cha 15 (2) kuondoshwa, maana nilikuwa napo nina mchango wangu lakini ninakubaliana na Kamati kiondoshwe sababu hakitusaidii, kingetuletea mashaka. Lakini naomba nikubaliane na Kamati wamekuja na mawazo mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende pia katika Kifungu cha 18 (2) (b) "Wakuu na Kurugenzi, na". Kwenye Mswada huu imeelezwa na tafsiri tumeupata lakini sifa zao hazikuainishwa hawa. Sasa tutakapokuwa tunaunda taasisi hii na Mswada huu tunaweka tu pale Kurugenzi, tunaweza tukapata Wakurugenzi ambao au Kurugenzi zile ambazo zinamsaidia Mkurugenzi Mkuu kama hatukuweka sifa za wale wakuu au zile Kurugenzi ambazo tunaziweka humu, tunaweza sasa tukaja tukaipeleka Tume ambapo hatutegemei kuwa iende, kwa sababu tutakuja kuajiri watu wasiokuwa na sifa. Maana juzi tu nimepitia tangazo moja likawa linataka waratibu wa Wilaya, wakati huku katika muundo huku kuna Maafisa wa Uchaguzi wa Wilaya. Sasa unajiuliza huku wale kazi zao nini, sifa zao kule wameambiwa alau *Diploma* lakini hawa watakuwa na sifa gani, huku ndani hawakuelezwa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Kifungu cha 20 "Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa na kazi zifuatazo".

Marekebisho ya Kamati katika Kifungu cha (a) baada ya kusajili wamesema kuandikisha wapiga kura. Sasa mimi nilitaka mimi isomeke zaidi yale marekebisho yaliyofanywa na Kamati kwa kuandikisha wapiga kura katika Wilaya zao. Maana isijekuwa na jukumu la kuandikisha, tukaweka tu hapa tukaandikisha uchaguzi baadae wakaenda kuandika katika Wilaya ya mwenziwe kwa sababu kaambiwa tu andikisha uchaguzi. Sasa tuweke ile tafsiri ya moja kwa moja kwa kuandikisha wapiga kura katika Wilaya zao, kwa sababu hapa tunaangalia Afisa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa na kazi zifuatazo. Sasa nilipendekeza tu isomeke hivyo.

Pia kuna marekebisho ya Kamati wameyafanya katika Kifungu wao wametwambia Kifungu cha (e).

Kifungu cha (e) kabla ya marekebisho kilikuwa kinasema "Afisa Uchaguzi wa Wilaya kazi zake itakuwa kuteua wagombea wa nafasi ya ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na ujumbe wa nafasi za Serikali za Mitaa. Sasa wakasema kifanyiwe marekebisho. Wakasema Kifungu (e) sasa kinarekebishwa na kuwa "Taratibu za shughuli za elimu kwa mpiga kura katika Wilaya yake". Yaani mimi kwanza sikubaliani na hii, labda ninaweza nikakubaliana nao kama tutakubaliana kuwa kifungu (d) kiondoshwe na kisomeke hiki ambacho wamekiainisha wao. Kwa hivyo, mimi kwenye eneo hilo naomba niyaseme hayo, nikubaliane na Kamati kuondosha kifungu (e), kwa sababu hakitaniteua tena kama nitashinda Afisa wa Wilaya atakuwa hana uwezo wa majukumu hayo, kwa sababu anasema kifutwe kabisa.

Kwa hivyo, katika marekebisho mimi nasema, nakubaliana kwamba kifungu (d) kitaondoshwa na kibaki hiki kifungu ambacho wao walisema (e) kiwe (d), ili kisomeke katika utaratibu huu waliloueleza wao. Naomba nirudi nyuma kidogo katika kifungu hicho hicho, kwa kifungu cha (b) ambacho kinasema;

Kifungu (b)

"Kuhamisha taarifa za mpiga kura kutoka sehemu moja na kumpeleka sehemu nyengine"

Mimi naomba niongezee tu hayo maelezo baada ya hapo yalipofikia iwe kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, isijekuwa tunampa mamlaka ya moja kwa moja hatumfungi na zile kanuni ambazo tunaziweka. Sasa naomba hili nalo lisomeke hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 21, sina mabadiliko hapo, isipokuwa nilikuwa napendekeza tu ili kuweka sawa mswada huu, kwa sababu kifungu cha 11(2) kilikuwa kinafanana na maelezo ya kifungu hiki cha 21, basi ningeomba tu kifungu hiki kiambatane na kifungu cha 11, yaani tukiweke pale chini baada ya kifungu cha 11 basi kiingie hiki baada ya kukiweka huku, kwa sababu yale mambo ambayo yamezungumzwa na kifungu hiki yapo kule ambayo ndio yanabeba ujumbe kwa maudhui mazuri.

Naomba niende sasa Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 22, naomba nikisome;

Kifungu cha 22

"Kwa ajili ya kuhakikisha uhuru wa Tume na uwazi wa afisa, isipokuwa yule aliyeteuliwa na Mhe. Rais, hatohamishwa bila ya ridhaa ya Tume"

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi sikubaliani napo, na nina mawazo yangu ambayo nahisi Waheshimiwa Wajumbe tutakubaliana. Kwa sababu nilipochangia kifungu cha 11(2) nikasema huu mswada tunaotunga sasa, Tume haiko na yale mamlaka yanayojitegemea. Kwa hivyo huyu afisa hatohamishwa kwa ridhaa ya Tume ya Uchaguzi. Tukiangalia Sheria ya Utumishi, maana sasa lazima tuipeleke kwenye ile sheria ya Utumishi Serikalini. Tukiangalia ile sheria inasema, watumishi wote isipokuwa wateule wa Rais, hawa kiongozi wao mkuu ni Katibu Mkuu Kiongozi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, leo afisa huyu awe hana mamlaka ya kuhamishwa na wakati huu mswada tunaoujadili hapa na Tume ambayo tunaijadili hapa, haina

mamlaka ya yale tuliyoyazungumza kule moja kwa moja, hatuwezi sasa na hiki tukakibana. Aidha, kule tutoe mamlaka ile *full autonomy* niliyozungumzia, au hapa sasa tukiachie wazi kwa Katibu Mkuu Kiongozi awe na wajibu wa kuwahamisha watumishi, isipokuwa wale ambao ni wateule wa Rais kama muongozo wa sheria ya Utumishi wa Umma inavyosema. Kwa sababu vyenginevyo sasa tutakuwa sasa tunahalalisha sheria mbili zenye kukinzana miongozo yake.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tufike pahala tuangalie vizuri, aidha tujadili katika mfumo wa kuonekana tunafuata katiba inavyosema kuwa kutakuwa na idara maalum inayojitegemea, au kama hatuendi kwenye idara maalum kwa kuwapa mamlaka yao kamili, basi turudi katika huu mfumo wa utumishi, kipengele hiki hakitakuwa *khaalis.* Kwa sababu kutohamishwa bila ya ridhaa na huyu afisa ni sehemu ya mtumishi kama watumishi wengine katika watumishi wale wa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, warudi kwa Katibu Mkuu Kiongozi ndio atakuwa mtumishi kwa watumishi wote, isipokuwa wale watumishi ambao ni wateule wa Rais. Kwa hivyo, yeye ana uwezo wa kumuhamisha. Kwa hivyo, kifungu hiki mimi kwa maelezo hayo hatohamishwa bila ya ridhaa, mimi napendekeza yafutwe kwa sababu sheria hizi za utumishi zitakuwa zinapingana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisogee sasa kwenye kifungu cha 23, ambacho maudhui yake yanafuatana na kifungu kile cha 11 ambacho nilikizungumza kule. Sasa hii mimi sina marekebisho, isipokuwa naomba sasa ifuatane iende katika kifungu cha 21 baada ya kujitegemea hapo kama kilipo sasa kifungu cha 23.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 32(1).

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna malipo ya Wajumbe wa Tume ambao watalipwa kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina na kwa kiwango ambacho kitaamuliwa na Rais. Sasa ndio nilipokuwa nazungumza kwa ujumla sasa tutaona kama hapa ile mamlaka ambayo nilikuwa naizungumzia mwanzo, pia nayo itakuwa inakinzana. Kuna watu ambao wanafanyakazi kwenye Tume wao mamlaka yao hayaguswi na utumishi, yatakwenda moja kwa moja kwa Mhe. Rais. Sasa kuna watendaji ndani yake ambao wanafanyakazi zile zile za Tume pale pale, sasa hawa wanarejeshwa kule kwenye utumishi. Sasa kwa nini tusifike pahala tukaamua tu kuwa wale wajumbe na maafisa wale maslahi yao yakajadiliwe huko huko na mapendekezo yake yaende huko huko kwa Mhe. Rais, kwa sababu tukiwaweka nusu ya wajumbe, lakini na hawa watendaji wanaosaidiana na wajumbe na ndio waratibu wakuu, wao tunawaondoa tunawapeleka kwenye

scheme hizi za kawaida, hawa tunawapelekea kwenye *scheme* yao ambayo imefunga sana katika kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis muda wako uko karibu ya kumalizika. Kwa hivyo, jitahidi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Bado dakika ngapi?

Mhe. Mwenyekiti: Nakugaia dakika mbili. Muda umemalizika. Kwa hivyo, jitahidi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Naomba nimalizie kwa kifungu namba 32(2), naomba nikisome;

Kifungu 32(2)

" Bila ya kujali kifungu (1) katika kifungu hiki Afisa wa Tume atalipwa mshahara kama itakavyoamuliwa na Tume kwa mujibu wa masharti ya sheria ya fedha za umma"

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba tumuulize ili tupate tafsiri ya moja kwa moja ni Tume gani? Kwa sababu kule juu hatukupata muundo, pengine kuna Tume ya Utumishi ndani ya Tume yenyewe au ni Tume kama ambavyo tunaipitisha hapa itatoa maamuzi haya. Sasa atakopokuja Mhe. Waziri aniweke sawa kwenye eneo la kifungu hichi, ni Tume ipi? kwa sababu wamesema hawa hawakuwa katika idara inayojitegemea kama itakuwa na muundo wao wa Tume ya Utumishi. Sasa hapa inazungumzwa tunawapeleka kwenye Tume, kwa mujibu wa masharti ya sheria ya fedha. Sasa Tume tumeipa mamlaka ipi au hii ambayo tunaipitisha sasa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, yale mengine nitayachangia kwa maandishi, kwa sababu uwezo wa nafasi ya Tume tunayoijadili sasa, kuna mapungufu mengine ya ujumla, hata zile ofisi wanazofanyia kazi utakuta kule ofisi moja ile ina vyumba viwili inawaratibu wilaya nzima. Nitachangia kwa maandishi maana muda wangu hautoshi, nakushukuru sana *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Miraji Khamis kwa mchango wako. Sasa ni zamu ya Mhe. Rashid Makame Shamsi, karibu uchangie.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia katika mswada huu muhimu wa Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea kutoa michango juu ya mswada huu, nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kutoa ufafanuzi mzuri, juu ya ufutaji wa sheria hii na ufafanuzi wake nafikiri umetusaidia sana, kwenye madhumuni hasa ya kufuta sheria hii.

Vile vile niishukuru Kamati inayohusika kwa kuweza kutoa ripoti yake na nimpongeze sana Mhe. Bi Panya kwa ufasaha wake katika uwasilishaji. Pia niwashukuru na niwapongeze wachangiaji wenzangu ambao wamepita. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti mswada huu wa kufuta Sheria ya Tume ni muhimu sana, hasa tukizingatia kwamba baada ya kumalizika kwa uchaguzi mmoja ni maandalizi ya uchaguzi mwengine. Kwa hivyo, umekuja wakati muafaka tukielekea katika uchaguzi wa 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nije moja kwa moja kwenye mswada katika Sura ya Kwanza, masharti ya utangulizi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 2 cha ufafanuzi nilikuwa natoa pendekezo, na mara nyingi huwa napendelea kulitoa kwamba, maneno ambayo yametolewa ufafanuzi yakae katika muundo wa *alphabet* inapendeza zaidi na msomaji inamrahisishia, kuliko ilivyo hivi sasa, kwamba imeanza na M ikaja T ikaja K ikaja M, kwa hivyo twende katika muundo wa *alphabet*.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije sasa katika ukurasa wa 228 wa waraka huu, katika mstari wa kwanza hapo kwenye neno ambalo linaendelea ambalo limeanza na hizo ndani ya muda aliotakiwa ametenda kosa. Nashauri hapo pawe na neno atakuwa ametenda kosa ili iweze kusomeka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu cha 9, uwezo wa kuruhusu uangalizi.

Mhe. Mwenyekiti, Tume inapewa uwezo wa kuruhusu uangalizi. Napenda tu hapa nitoe msisitizo kwamba, suala la uangalizi ni suala ambalo linakubalika ulimwengu mzima. Lakini Tume naiomba iwe makini sana, kiuzoefu na baadhi ya waangalizi wetu wanaokuja kuangalia chaguzi zetu, wawe makini katika utoaji wa vibali, kwa sababu baadhi ya waangalizi wenyewe wanakuja kwanza na utashi wao. Sasa huwezi kuwa na mwangalizi halafu akatanguliza utashi

wake, kwa hivyo hilo liangaliwe. Baadhi ya waangalizi wanachangia kuchochea amani iliopo katika nchi yetu, inahitaji sana kuweza kuchunguza ni waangalizi gani wameleta maombi yao na Tume kuweza kuwapa vibali vya kuweza kuifanya kazi ya uangalizi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hata katika ripoti kifungu cha 3, ripoti zao zinapokuja ziangaliwe kwa umakini sana, na isiwe tu sheria inaweza ikamnyima kibali mwangalizi ambaye hakuleta ripoti kwa uchaguzi ujao au utakaokuja, lakini hata yule ambaye ameleta ripoti ambayo inaonesha utashi, nafikiri kuna haja nao waangalizi wa namna hiyo kunyimwa vibali katika kuangalia uchaguzi au kura ya maoni itakayokuwa inafuata.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika ukurasa wa 229 kifungu cha sheria 12 kinachozungumzia muhuri na nembo ya ofisi. Hapa tunazungumzia suala muhimu sana, kwa sababu nyaraka mbali mbali za Tume huwa zinabidi kuwekwa muhuri au nembo.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia kwamba inaonekana teknolojia siku hizi imekuwa, Tume inalazimika kuweza kuwa na utunzaji na udhibiti mzuri sana katika suala zima la muhuri na nembo yake, kwa sababu inajitokeza hivi sasa mpaka watu kuweza kughushi vitambulisho vya wapiga kura, sasa seuze kuweza kuja kughushi muhuri wa ofisi. Ni muhimu kuwa makini sana, na tuwe na watendaji walio waaminifu ambao watakuwa wanadhibiti nyenzo hizi ambazo zisije zikaleta kufanyika kwa ghushi ambayo inaweza ikaja kuathiri utendaji kazi wa Tume.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika kifungu cha 14 kuhusu sifa za Mkurugenzi. Katika kifungu (c) kinasema;

Kifungu cha 14(c)

"Awe ni afisa muandamizi katika Utumishi wa Umma"

Mhe. Mwenyekiti, katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu Zanzibar neno "muandamizi" halipo, napendekeza liwe neno "mwandamizi" kwa "mw" na sio "mua".

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na michango yangu nije katika ukurasa wa 232, kifungu 24 Fedha za Tume, kifungu (b), nina wasi wasi na hili neno kwamba fedha zitakazopewa. Nahisi neno muafaka iwe fedha watakazopewa Tume. Kifungu cha 25 kuna neno "Muhasibu" napendekeza iwe "Mhasibu".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 26(2) kwenye mstari wa mwisho ambao umeanza na ... huo pamoja na taarifa za fedha kwa waziri, nafikiri kulikuwa kuna maneno hapo yalilazimika yaingizwe, pamoja na taarifa za fedha kwa waziri. Naona kama pana maneno yamekosekana, mimi nilifikiria na ninapendekeza kwamba, pawe na maneno na taarifa za fedha ziwasilishwe kwa waziri. Kwa sababu kulikuwa na taarifa hapa, sasa kwa waziri kidogo inakaa vibaya kama hapana maneno ya ziada, lakini ulazima ni kwamba hizo taarifa vile vile zimfike waziri.

Mhe. Mwenyekiti, tukija kwenye kifungu cha 28 kuhusu masuala ya fidia ya ajali.

Mhe. Mwenyekiti, hapa imetajwa kwamba sheria inapendekeza kuwe na fidia kwa mjumbe wa Tume na watendaji pale ambapo inatokea ajali. Nina wasi wasi tu kwamba watendaji hawa watakuwa ni wale tu ambao wameajiriwa na Tume, yaani waajiriwa wa kudumu au hata wale wanaoajiriwa kwa muda katika suala la usimamizi wa vituo, wawe ni wasimamizi wakuu wa vituo au wasaidizi, kwa sababu hawa nao wako katika harakati za uchaguzi. Sasa kama watendaji hii haiwaingizi wale, mimi napendekeza Mhe. Mwenyekiti, kwamba wale watumishi wa muda mfupi, kwa maana ya wasimamizi wa vituo na wasaidizi wao, kwa sababu wako katika harakati za uchaguzi na wao, basi na wao wafikiriwe pale itakapokuwa inatokezea ajali na wao wako katika shughuli ya Tume basi na wao wafikiriwe katika kupewa fidia.

Mhe. Mwenyekiti nije katika makosa na adhabu katika kifungu hichi cha Sheria kimeeleza kwamba kutakuwa na adhabu kwa wale ambao watatenda makosa mbali mbali, nashukuru kwamba imetaja kuna kifungu cha (a)(b) na (c).

Nikija katika kifungu cha (b) kwa makusudi ataharibu mwenendo wa mkutano wa Tume au kufanya vitendo vitakavyopelekea mkutano wa Tume usiendelee, na kifungu cha (c) kimejumuisha kwa maana ya kwamba atafanya jambo jengine lolote litakalosababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake.

Mimi nafikiri kuna makosa ambayo yashazoeleka zoeleka, pamoja na kwamba kifungu cha (c) kinafunga na makosa mengine yote, lakini napendekeza haya makosa mawili yangeingizwa hapa yakawa bayana, kwa sababu watu wameshaanza kuyazoea.

Kosa moja ni kufanya fujo katika kituo cha uchaguzi. Ningependa hicho kifungu kiingie, hilo kosa liwe bayana, kwa sababu watu wamezoea kufanya makosa katika vituo vya uchaguzi, lakini kuna kosa ambalo linaendelea

kujitokeza la kujitangazia matokeo, hili naomba nalo liwe bayana, liwe bayana kwamba kusiwe na utata kwamba halikutajwa, wachukuliwe hatua ambazo zinastahiki kwa mujibu wa sheria hii.

Nikija katika kifungu cha 30 Mhe. Mwenyekiti, ambayo inasomeka "kitendo chochote kilichofanywa au kimeachwa kufanywa kwa nia njema na Afisa wa Tume katika utekelezaji wa kazi na uwezo wake chini ya Sheria hii, au Sheria nyengine yoyote hatokuwa na hatia ya madai au jinai kuhusiana na tendo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi wa hili neno "kwa nia njema", kwa sababu inakuwa ni vigumu sana kumpima mtu kwamba kweli alikuwa na nia njema. Sasa ningependa wanasheria waitizame hii kwa sababu mtu anaweza akaja akaacha kutenda jambo halafu likasababisha madhara halafu ikaja ikawa kafanya kwa nia njema. Sasa hii nia njema sijui *Mwana- psychology* gani anaweza kuisoma kwa nia njema, alikuwa na nia njema hiki kifungu lazima kitazamwe. Kwa sababu ndani ya Tume yetu tuna watu ambao kwa kweli imejionesha kwamba hizo nia njema hawana, na nchi hii sasa hichi kipengele kisije kikaleta mwanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie suala zima la Kanuni katika kifungu cha 33. Uzoefu unaonesha kuchelewa kutungwa kwa kanuni aidha na taasisi au Wizara inayohusika na Sheria ambayo tunaipitisha. Ningeiomba sana wizara inayohusika na hususan Taasisi hii ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi baada tu ya kuipitisha sheria hii kuweza kuona kwamba kanuni hizo zinatungwa haraka, ili kuweza kuona kwamba kabla ya uchaguzi wa 2020 Kanuni hizo zipo na wananchi wanaelimishwa nazo wanazifahamu ili kuweza kuona kwamba Afisi inafanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na michango hiyo Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na mimi naunga mkono hoja ya kuweza kuupitisha mswada huu asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (Makofi)

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuweza kuchangia mswada huu.

Kwanza kabisa nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutoa ufafanuzi mzuri madhumuni na sababu ya kuanzishwa kwa Mswada huu, lakini pia naamini kwamba tutakapopitisha Mswada huu basi Tume inaweza kutekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa Mkurugenzi ambaye yeye ndiye atakayekuwa na dhamana ya kutekeleza majukumu na kazi za kila siku za Tume.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi, kwa sababu wajumbe wenzangu mengi niliyotaka kuchangia wameyazungumzia, lakini katika kifungu cha 16 (d) kinachozungumzia kuandaa bajeti na kalenda ya shughuli za Tume. Napendekeza kwamba neno kalenda basi liwekwe neno ratiba ya shughuli za Tume.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 8 kinachozungumzia kwamba uwezo wa kuanzisha kamati za ushauri. Katika kifungu hichi napendekeza kwamba katika hiyo kamati ambayo itakayoanzishwa ya ushauri hawa Wajumbe wa Kamati wawe na sifa maalumu.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya kupendekeza marekebisho hayo basi niende moja kwa moja kwa kuwa Sheria ya Tume ya Uchaguzi Namb. 9 ya 1992 inafutwa, na kwa sababu tu ya changamoto mbali mbali walizoziona na ndipo badala yake kuletwa kwa mswada huu, niseme naungana na wenzangu kwa asilimia mia moja kwamba tuupitishe mswada huu ili tuweze kufanikisha masuala mazima ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika sura ya pili kuanzishwa kwa Majukumu na uwezo wa Tume. Katika kifungu cha 4(1) Tume itakuwa na majukumu yafuatayo, katika kifungu hicho cha 4(d) Tume itakuwa na jukumu la kufanya mapitio na kuweka mipaka ya majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kila baada ya muda wa miaka mitano Tume inafanya mapitio ya mipaka, lakini napendekeza kwamba katika Sheria zilizopita Tume ilipita katika maeneo na kuchukua maoni ya wananchi kwa ajili ya kutoa mapendekezo kwa ajili ya kurekebisha au kufanyia mapitio ya mipaka ya majimbo, lakini cha kusikitisha kwamba changamoto zilizopo Tume badala ya kuchukua maoni ya wananchi baadae mapendekezo yale yanayotolewa na wananchi yanakuwa hayatekelezwi, Tume inatoa mapendekezo yake na badala yake inasababisha uingiliano baina ya jimbo na jimbo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maneno haya niliyoyasema hapa nasema niungane na wenzangu, na pia nawashauri sana tuupitishe mswada huu ili kuhakikisha kwamba unapita na kuona Tume yetu ya Uchaguzi ya Zanzibar inaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Mswada huu mzuri wa kubadilisha Tume ya

Uchaguzi ya Zanzibar. Kama tunavyoelewa Zanzibar tumeingia katika uchaguzi juzi na tumeona kasoro nyingi zilizojitokeza katika uchaguzi, sasa naamini Serikali imeliona hilo kama kulikuwa na kasoro humu ndani ya Tume yenyewe, sasa imeleta mswada bora ambao utaweka misingi bora, imara na kuwa na Tume ya Uchaguzi iliyo imara.

Mhe. Mwenyekiti, umeniwahi kidogo lakini nilikuwa naendelea kupitia huu Mswada, lakini kwa kweli nimefurahishwa na baadhi ya mambo ya Mswada, kulikuwa kuna kasoro nyingi ukiziangalia kasoro alizosoma Mheshimiwa zilianza (a) mpaka (g) kasoro ambazo zilikuwemo ambazo zote zilikuwa zinahitaji kurekebishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kilichonifurahisha katika Mswada huu nambari moja kile kilichobadilishwa na Mswada kinachosema Sasa Rais hatoshauriana na mtu katika kuteua mtu yeyote katika Tume ya Uchaguzi.

Nilipokuwa nachangia Baraza lililopita nilisema Rais wa Zanzibar ni Rais wa Serikali anayeongoza wananchi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kufanya baadhi ya maamuzi yake hatakiwi kabisa kabisa kushauriana na mtu au kikundi cha watu au taasisi. Huyu ni Rais wa Zanzibar, wananchi wana Mapinduzi, wakwezi na wakulima ndio waliomchagua kuwa Rais, kwa hivyo hakuna haja ya kushauriana na mtu.

Ilikuwa inanisikitisha sana kuona Rais wangu wa Mapinduzi ati ashauriane na Chama cha upinzani au kiongozi wa upinzani nikasema aah! Mungu akinijaalia mimi nikiwa Rais kipengele hichi nitakifuta, lakini nashukuru sana kwamba leo Serikali imeliona lile kosa ambalo inalifanya na kulifuta, sasa Rais wa Zanzibar atawatangaza na kuwateua watendaji wa Tume ya Uchaguzi bila ya kushauriana na mtu yeyote anapoona unafaa, akiona leo Mhe. Ali anafaa kuwa Mjumbe katika Tume ya Uchaguzi amemuweka, hakuna kushauriana na watu, akiamka usubuhi tu hiyo ndio nchi ya kimapinduzi na hiyo ndio sifa ya mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mapinduzi matukufu ndiyo yaliyotufikisha hapa, kwa hivyo tuna kila sababu ya kuendesha nchi yetu kimapinduzi, na kila mtu kujua kama Zanzibar ni nchi ya Kimapinduzi kwa lengo la kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima.

Nitakwenda na kitu ambacho nimekiona hakifai hebu twende katika kifungu nambari 11 kinasema "Ofisi itakuwa na taasisi zinazojitegemea, endelevu,

zenye uhuru wake na jina lake litakuwa na uwezo wa. (a) Kushtaki na au kushtakiwa.

Mhe. Mwenyekiti tumeona uzoefu wa hizo taasisi Tume mbali lakini uzoefu wa hizo taasisi naomba sana kutoa ushauri wangu hichi kipengele (a) kiondoke mara moja. Iwe Tume au Taasisi ya Tume iwe haina uwezo wa kushtakiwa, kama kushtaki au kushtakiwa ashtakiwe AG kwa kupitia sheria ya kusimamia kesi za madai ya Serikali. *Government Proceedings Act* itumike sheria hiyo isitumike Sheria ya kushtakiwa Tume" Kwa sababu kama unakwenda kuishtaki taasisi ya Tume unataka sasa kutupotezea muda, Hassan kashashinda Urais akitaka kugombania tena unashtaki Tume utaratibu mzima haupo itakuwa tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hii ni nchi ya Mapinduzi, unapoanza kutupotezea muda katika kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima kutaja kushtaki taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tena ya uchaguzi ni kutupotezea muda, naomba sana itumike *Government Proceedings Act* hapa, hii iondoke kama kushtaki au kushtakiwa, ashitakiwe AG sio Taasisi ya Tume Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, 12 kuna muhuri kuna maelezo mengi hapa lakini hakuna panaposema atakayeutumia muhuri huu wa Tume ya Uchaguzi vibaya ahukumiweje. Kuna watu wajanja, kuna watu wakorofi, atakayeutumia muhuri huu wa Tume ambao ndio unaotuwekea Serikali ya Mapinduzi baada ya uchaguzi lazima atolewe hukumu humo humo, lazima mtolee hukumu sheria.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Serikali ilione hili atakayeutumia muhuri wa Tume ya Uchaguzi vibaya, na ikithibitika basi miaka 20 Tume ya Uchaguzi ni kitu kikubwa, hii ni kutoa fundisho kwa wengine kwamba kuheshimu Serikali iliyopo madarakani na vyombo vyake.

Mhe. Mwenyekiti wamejitokeza watu wana *fake documents* za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na ku-*forge* muhuri halafu wanakwenda tu kiholela holela na leo lazima Mhe. Mwenyekiti, tutoe tanbihi kali kabisa kwa yeyote yule atakayeutumia muhuri wa Tume ya uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, tumekaa hapa tunapitisha sheria hii sisi ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Tisa ambao tumekuja humu kuwatetea wakwezi na wakulima kwa maendeleo yao.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kipengele namba 9 kifungu namba 5, mtu yeyote au taasisi yoyote itakayofanya uangalizi wa uchaguzi bila ya kibali cha Tume itakuwa imetenda kosa na ikipatikana na hatia itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi shilingi milioni tano.

Mimi hapa sikubaliani napo hata siku moja, kuna watu wana mamilioni hata hayana hesabu huko duniani. Sasa mtu kashafanya uangalizi keshakuwa na *data* anazozitaka yeye ashapelekwa Mahakamani analipa milioni tatu au milioni tano si katoka *free* huyo.

Mimi namiliki hivyo na nimeshafanya uangalizi nimeshampa mtu kujitangza leo anakwenda Mahakamani, sheria imetaja wazi wazi alipe milioni tatu au tano kumbe ana uwezo wa kulipa mara 40 kuliko vile, haiwezekani Mhe.Mwenyekiti, huyu awe amefanya kosa la jinai atakayefanya uangalizi wa uchaguzi ina maana umeshapata *data*, kwa maana hiyo kama umeshapata *data, you can use the data* katika kufanya unavyotaka.

Sasa leo ukatoe milioni tatu au tano *okay* mtu mwengine atafanya uangalizi atatumia *data* alizozipata halafu atapelekwa Mahakamani atakwenda kulipa milioni tatu au tano, sasa lakini *impact* yake ni kubwa kuliko fedha tulizoziweka.

Mhe. Mwenyekiti hapa pesa si kipimo, hapa awe amefanya kosa la jinai na nchi zote za Kimapinduzi mtu atakayetoa *data* za Serikali nchi zote za Kimapinduzi duniani huyo amefanya kosa la jinai. Uingereza pale, Marekani pale ukitoa *Government data* wewe umefanya kosa la jinai hatuwezi kumuwekea katika sheria kulipa milioni tatu au tano itakuwa sisi wenyewe pia tunafanya kosa la jinai kwa pesa hizi tulizoziweka.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda 12 tayari muhuri nimeshasema. Mambo mengine mengi ambayo nimeyaona katika sheria hii mimi nakubaliana nayo sana, lakini tunatunga sheria, tuna utaratibu tunazitunga hizi sheria zetu halafu huwa hatuzitumii kama tulivyozitunga au kama kusudio tulivyolitaka Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria nyingi tunatunga, Waafrika, Wazanzibari, Watanzania na *East Africa* sote tunafuata *Common Law* za Kiingereza, tuna nyingi lakini hatuzitumii. Kwa hivyo Mwenyekiti naomba sana sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Tisa tumekutana hapa kutunga sheria hii ya uchaguzi ambayo halafu tuitumie.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna pahali hapa nilikuwa nina wasi wasi napo sana nambari 8(1) panasema "Tume inaweza kwa madhumuni ya utekelezaji wa

majukumu yake mazuri chini ya sheria hii kuanzisha kamati za ushauri kama itakavyoona inafaa".

Mhe. Mwenyekiti, ushauri, mimi sitaki iwe Tume, nataka unaposema Tume unaisema vibaya, nataka iwe Mwenyekiti wa Tume isiwe Tume. Unajua mwisho wa hii sheria naomba kiongezwe kipengele kiseme, Mwenye mamlaka ya mwisho katika masuala ya uchaguzi na maamuzi yote ya Tume ya Uchaguzi awe Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mambo yote mwisho wa hii *document,* inaongea wazi wazi kwamba mamlaka yote inayohusiana na masuala ya uchaguzi Zanzibar awe Mwenyekiti wa Tume tena awe hakuna mtu au taasisi ya watu inayoweza kumshtaki wala kumuuliza.

Jana naangalia TV sijui kuna hata sijui nimuiteje, sijui Mahakama gani huko Bara inampeleka Mhe. Jecha sijui Mahakamani ah! *come on!* Uchaguzi upo Zanzibar Mhe. Jecha ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, kunako TV sijui kuna mtu gani huko, kuna mtu kampeleka Mahakamani sijui kuhusu uchaguzi.

Mimi rohoni mwangu nikasema ah! *I wish* ningekuwa na nafasi fulani, maana yake huyo huyo angekuja huku Zanzibar basi hata kama hatuwezi kumfanya chochote hata mawe tungempiga. Mambo haya unatuletea sisi tunataka kuendelea sasa hivi unakwenda kurudisha katika masuala ya kwamba ooo uchaguzi uchaguzi, sisi uchaguzi tushamaliza *(Makofi)*

Mimi nishaamka hivyo kweli kuna mtu anaweza, mimi nauliza kuja kunivua madaraka yangu ya uwakilishi Jimbo la Welezo, nani? Umoja wa Mataifa, *European Union*, hakuna. Nani anaweza kuja kumvua madaraka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alishaapa Amani katika hadhara ya watu, Tume ya Uchaguzi imemtangaza.

Mimi nawaomba sana wale wote wenye dhana hiyo waiondoshe. Rais keshaapishwa, Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Welezo keshaapishwa, huu ni Mkutano wa Nne anaingia, hakuna mtu wala watu ndani ya nchi mwenye uwezo na mamlaka ya kuweza kumvua Hassan Khamis Hafidh uwakilishi wake wa Welezo kwa miaka yake mitano iliyobakia, au kumvua Rais wa Zanzibar uraisi wake aliochaguliwa na wananchi na Tume ya Uchaguzi kumtangaza.

Mhe. Mwenyekiti, naona umewasha taa yako. Nawaomba wale watu tushirikiane katika kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima, waache kudanganywa. Tume ya Uchaguzi ndio yenye mamlaka na imeshamtangaza Rais.

Mhe. Mwenyekiti, umefika wakati wa kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima si kudanganyana.

Mwenyekiti mwisho naomba kiongezwe kipengele kinachompa uwezo Mwenyekiti wa Tume ya Uchanguzi ya Zanzibar kwamba ndio mtu wa mwisho ili tulinde mtu yeyote yule tena kusikia kwenda mahakamani nakwenda wapi.

Baada ya hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nachukua fursa hii adhimu kukupongeza kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mswada huu kwa kutoa maoni yangu machache niliyonayo juu ya mswada wa kuanzishwa kwa Tume ya Uchaguzi. Mswada ambao umekuja kwa muda stahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi sina budi kutoa shukurani zangu za dhati ingawa kwa kanuni zetu tunatakiwa tusipongeze sana, lakini mimi kupongeza kwa jambo zuri nitapongeza kidogo, kwamba kwa kusema kwamba mswada huu umefikika kwa wakati muafaka ambapo tunafikiria wengi tulikuwa tunajiuliza lini mswada huu wa marekebisho na kuanzishwa kwa Tume ya Uchanguzi utafika na hatimaye tuipate hiyo sheria yenyewe ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kusema mengi kwa sababu pale Mhe. Rashid yeye ana tabia akinitangulia mimi huwa ananipitia mimi mule ninamosema ikisha akatangulia yeye. Siku hizi nina ombi langu nitalileta maalumu kwamba nitangulie mimi kisha aje yeye, mjanja yule, mchokozi kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti mimi nachukua nafasi hii kusema kutaka kuzungumzia juu ya mswada huu kuhusiana na muundo mzima jinsi ulivyo. Tumekaa tumeutafakari kwa kina lakini tumegundua kwamba mswada wa sheria kwa kuanzisha Tume ya Uchaguzi, ndio utakaokuwa ni jibu la maswali ya uchaguzi ambayo tukijiuliza sisi kwa kila siku, tulikuwa tukizungumzia mapungufu mbali mbali yaliyomo kwenye sheria ambayo tumeifuta sasa kwa mswada huu ambao tumeuwasilisha sasa hivi muarubaini wake umepatikana.

Mheshimiwa mwenzangu hapa *Diaspora* alikuwa akizungumzia suala la watu watakaotumia vibaya nembo ya Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Sasa jibu hili la kutumia vibaya nembo ya Tume ya Uchaguzi imepatikana, kwa sababu sheria tuliyokuwa nayo zamani, wafanyakazi wetu watumishi wa Tume ya Uchaguzi wengine walikuwa si waajiriwa, sasa ilikuwa ni vigumu kumkamata mtu wakati huna sheria ya kumdhibiti, lakini kwa mswada huu tumeona kwamba hakutokuwa na tatizo la utekelezaji au wa matumizi mabaya ya muhuri wa Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu sheria inaeleza wazi kama tukija kwenye 19 kuanzishwa kwa sheria au haki ya kupata habari, haya mambo yote yameelezwa wazi na yametengewa adhabu. Mtu anajua kwamba mimi nitakapofanya kosa hili adhabu yangu ni hii, ambayo imetajwa katika sheria.

Mhe. Mwenyekiti tukija kwenye namna ya kupata habari ndiyo nilikuwa naiangalia. Kama tunavyofahamu kwamba mambo ya habari ndio kitu muhimu. Matatizo yote tumeyapata kutokana na habari.

Leo mtu anatoa habari ya hapa anamwambia mwengine na mwengine anamwambia mwengine, matokeo yake habari hizi zinaenea bila ya kuwa na usahihi. Hiki ndio kilichokuwa chanzo kikubwa cha matatizo ya uchaguzi wetu uliopita. Lakini kwa sheria hii tuliyonayo ambayo tunaitegemea si muda mrefu Mhe. Rais ataitia saini huu mswada kugeuka kuwa sheria, itakuwa mtu ana wasiwasi juu ya kutoa taarifa za uongo. Ingawa na yeye anapotakiwa kutoa taarifa akikataa itakuwa vilevile kuna kifungu cha adhabu kinachomkabili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa sababu nilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati iliyosimamia Mswada huu na kuuchambua kwa kina na tumeyaona mengi ambayo tumeyaeleza. Lakini kwa upande wangu mimi kama Omari binafsi natoa wito wangu kwa wenzangu ambao wamechangia mambo mazuri, kwamba ni vyema sasa tukaunga mkono mswada huu, tukaupitisha mswada huu kwa umoja wetu hatimaye na kuwa sheria. Sheria ambayo itakuwa ndio dira itakayotuongoza katika uchaguzi unaokuja. *(Makofi)*

Mswada unaeleza wazi jinsi gani tutaanzisha Ofisi za Tume za Uchaguzi za Wilaya na namna gani Tume itakuwa na mamlaka ya kuajiri watumishi wengine. Zamani Tume walikuwa hawana mamlaka kwa sababu hawaajiri, kwa sababu walikuwa hawana mamlaka ya kisheria, tutakapopitisha mswada huu tutaipa Tume sheria za kuanzisha Ofisi za Wilaya na hatimaye kuajiri

wafanyakazi pale itakapoona inafaa. Ni imani yangu kwamba tutauchangia vizuri, tutaunga mkono vizuri mswada huu ili kama nilivyosema baadaye ugeuke kuwa sheria tutakayoitumia na kutuongoza katika mambo yetu ya uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mengi wenzangu ya marekebisho wameyazungumza. Mheshimiwa Kwanza pale ametangulia kufanya marekebisho sambamba na Kamati yetu. Kamati imeyapitia na Mhe. Rashid na Waheshimiwa wenzangu wengi, mimi kwa upande wangu nasema naunga mkono hoja ya mswada huu ulioletwa na natoa wito kwa wenzangu wote tuunge mkono kwa asilimia 100 na hatimaye tuipate iwe sheria inayotuongoza.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu kwa asilimia 100.

Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti mimi mchango wangu naanza katika ukurasa wa 288 kifungu cha 10 naomba nikinukuu kidogo Mhe. Mwenyekiti ili baadae niweze kueleweka lile ambalo nakusudia kulizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu kinasema kwamba, "Tume ya Uchaguzi wakati wowote katika mazingira yatakapohitaji katika utekelezaji wa majukumu yake kuandaa kanuni au muongozo". Mchango wangu hapo ndipo unapotaka kupata ufafanuzi wa ziada kwamba wakati wowote mazingira yatakapohitaji. Nataka kujua hiyo tafsiri ya mazingira yaliyokusudiwa ni mazingira ya aina gani, na mazingira hayo yataeleweka vipi na nani ambaye ataenda kushauri kuhitajika kwa hayo mazingira.

Sasa tabu yangu ninayoipata Mhe. Mwenyekiti, kujua hayo mazingira yatakapohitaji ni mazingira ya aina gani, na ni nani atakayoyajua hayo mazingira. Mimi nilikuwa nahisi labda angalau tungeainishiwa jambo moja ambalo litaonekana lina muongozo wa kimazingira hilo jambo ambalo limeonekana ambalo linaweza likapelekea huo uhitaji katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, nikishaliachilia hilo nakwenda katika kifungu 29 ukurasa wa 232 (1) pia naomba ninukuu:

29(1)"Mtu yeyote ambaye:-

(a) kwa makusudi atamzuia mjumbe wa Tume au Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Tume kutekeleza majukumu yake;"

Mhe. Mwenyekiti, nipongeze kwa kifungu hiki ambacho kinaweza kutupelekea kuweka hali ya utulivu katika nchi yetu.

Katika kupata uhuru watendaji wa Tume kufanya majukumu yao, nataka niongeze jambo moja wenzetu walione ni jambo la umuhimu katika kifungu hiki katika kukiweka kifungu hiki angalau na sisi kikaweza kutusaidia, kwa sababu sheria imetuelekezea sisi zaidi au imeelekezea wananchi pindipo watakapopelekea hatua za aina yoyote ambazo zitapelekea mikutano kuvunjika.

Mhe. Mwenyekiti, hata Tume nayo katika utendaji wao wana mikutano yao, ya kiutendaji na inapelekea mikutano yao ushafahamu kuashiria au kuvunja taratibu za kikanuni. Lakini katika sheria hii sijaona pahali popote pale ambapo inapelekea, na hili limetokezea katika uchaguzi ambao uloharibika kwamba tumeambiwa miongoni mwa mambo yaliyoharibu ni baadhi ya maafisa wa Tume yaani Makamishna kuacha kufanya kazi ambazo ziko katika utaratibu wa kisheria wakaelekeza siasa zaidi katika kuharibu kazi ya Tume ya Uchaguzi.

Sasa katika sheria hii sijaona wapi maafisa wa Tume ama watu wa Tume watakapopelekea kuvuruga taratibu za Tume za kisheria wao hatua za kisheria zinapowabana. Ningeomba watusaidie hili wapi wanaweza kuliweka hili, kwa sababu lengo na madhumuni ni kuangalia pande zote mbili, kwetu sisi na kwao watendaji sheria wapi inawaelekeza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, chengine ni kifungu cha 21, kilikuwa kinazungumzia masuala ya ajira, kinasema Tume inaweza kuajiri watumishi wengine wa afisi kadiri itakavyoona inafaa.

Hapo hapo nilikuwa naomba tusaidiane katika kuelezea sifa za muajiriwa pale Tume itapoona kwamba kuna haja ya kuweza kuajiri. Mara nyingi tutakuwa tunaangalia vigezo vya elimu lakini kwa unyeti wa kazi za Tume ya Uchaguzi, na kwa hatua ambazo tulifikia pahala zikatuweka katika mazingira magumu kwa baadhi ya watumishi wa Tume ya Uchaguzi.

Mimi naomba kungekuwa kuna mambo ya ziada yakawekwa katika kuangalia sifa ambazo mtumishi anaweza akaajiriwa, nimeziweka mbili tu lakini waongee wanaweza kungalia za ziada. Lazima kuwe na sifa ya uzalendo wa mtu katika

nchi yake, lazima mtu huyo aangaliwe anayo hiyo lakini na pili kuangalia tabia na mwenendo wake kabla ya uajiri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia katika mswada huu liko katika kifungu cha 19 (3) suala la kiapo.

Mhe. Mwenyekiti imeandikwa tu Afisa Uchaguzi wa Wilaya kabla hajaanza kazi zake atalazimika kula kiapo cha utendaji wa kazi mbele ya hakimu kwa namna kitavyoelezwa na Tume.

Sasa nilitaka ufafanuzi tu, kwa sababu imetajwa hakimu tu haikutajwa kama Hakimu wa Mwanzo, Hakimu wa Wilaya ama Hakimu wa Mkoa, sasa angetusaidia kama kilichokusudiwa ni Mahakimu wa aina yoyote au ipi hapa, ningeomba msaada katika eneo hili, lengo na madhumuni lililokusudiwa ni Hakimu wa aina gani.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo ningeomba na mimi kama walivyotangulia baadhi ya wenzangu natilia mkazo kwa dhati kabisa kuweka kifungu cha mtu ama Afisa asiyehusika, yaani kwa mgombea ama awe Rais, Uwakilishi au Udiwani kujitangazia ushindi kabla ya muhusika kujitangaza ama Afisa asiyehusika na kazi hiyo kuanza kutangaza ushindi pasipo na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili kwa haraka haraka unaweza kuliona kama ni jambo la kawaida, lakini ni suala zito sana ambalo linaweza kupelekea kutoweka kwa amani ya nchi yetu, linaweza kupelekea kuanzisha migogoro isiyokuwa na msingi. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo zito sana, naomba patafutwe pahala pa kuingizwa kifungu hiki na naomba niwashawishi wajumbe wenzangu waniunge mkono katika hili endapo atatokezea mgombea wa aina yeyote kujitangazia urais pasipo na utaratibu wa kisheria, Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapendekeza hukumu yake iwe kifungu cha maisha na nawaomba wenzangu waniunge mkono katika hili kwa sababu ni jambo ambalo limetuweka pabaya katika mazingira ya nchi yetu limeshatokezea, mtu anajitangazia halafu baadae anarudi anasema mimi sikujitangazia mimi nimenukuu karatasi.

Kama hatukuliweka katika sheria waziwazi Mhe. Mwenyekiti, litaendelea kututesa. Ninawaomba wajumbe wenzangu ninataka kutumia kauli nzito hapa, wenzangu wakanambia usende huko mbali sana. Lakini nawaomba ili sheria hii tuipe wepesi basi kifungu cha kujitangazia mtu ama Urais, Uwakilishi au Udiwani bila ya utaratibu kiwekewe hukumu iliyokuwa nzito ili kuweza kutokomeza suala hili lisirejee mara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine na la mwisho, mdogo wangu hapa Mhe. Hassan Khamis Hafidh, alizungumzia zaidi suala la muhuri wa Tume na alikemea sana akataka lazima ziwekwe sheria kali kwa mtu ambaye atatumia pasipo na utaratibu wa kisheria au pasipo na mamlaka ya kisheria ambayo inamruhusu mtu kutumia muhuri. Mimi nataka kukazia suala hili ni kweli, nazungumza kweli kwa sababu tunajua lazima tuseme ukweli na niwapongeze sana watu ambao wameandaa mswada huu wa kuja kurekebisha haya masuala ya Tume ya Uchaguzi.

Kwa sababu tumepata kadhia kubwa na mambo mengi ambayo tumeyaona kwa watu kufanya mambo ya ovyo ovyo yasiyostahiki katika jambo hili la Tume Uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, yeye alizungumzia zaidi muhuri, lakini ushahidi unatuonesha, moja katika mambo ambayo yalipelekea kuharibika kwa uchaguzi basi ilikuwa watu ku-*duplicate* fomu za matokeo ya uchaguzi, fomu halali zinazungumza vyengine, lakini watu wakatoa fomu ambazo zina matokeo mengine matokeo ambayo kwa kweli ukiyaangalia hata katika akili ya binaadamu haiji.

Kuna jimbo Pemba fomu ya uhalisia haikutolewa lakini imetolewa fomu ya bandia ambayo ilikuwa inazungumzia matokeo ya Mhe. Rais kama katika jimbo lile amepata kura 3, akili ya mwanadamu haikubaliki. Jimbo hilo lina Mkuu wa Mkoa, jimbo lina Mkuu wa Wilaya, jimbo hilo lina Mwakilishi mwenyewe mgombea, lina Mbunge anayegombea lina Diwani anayegombea, lina Sheha wa Shehia, lakini mambo ambayo baada ya kuangaliwa ni *forgery*, yaani fomu haiko sahihi.

Sasa kama tunafikia pahala watu wana *forge* fomu, nina imani kuna siku watu watakuja ku-*forge* na hii mihuri. Sasa katika maeneo haya Mhe. Mwenyekiti, naomba marekebisho yawe mazuri, hukumu ziwe kubwa ili mambo haya tuweze kuyapiga vita, vyenginevyo tukiachilia tu katika hali ya kawaida yanaweza kuja kutuweka katika mazingira ambayo hayako sahihi. Ndio maana ninarudi katika kifungu changu cha uajiri, tunafikia pahala tunawaajiri watu kwa kuangalia elimu hawana uzalendo, hawana uchungu, wameweka roho zao tamaa mbele, mtu akishagaiwa rushwa shilingi laki tano anabadilisha matokeo anapiga muhuri.

Sasa lazima tuweke adhabu ambazo kali, matokeo yake wametuvuruga katika uchaguzi na sikutaka kusema hapa lakini ningeomba Wizara itwambie wale watu wamefikia wapi kuhukumiwa katika nchi hii. Kama sheria haziko wazi basi pia tuweke hizi hukumu tuone.

Mhe. Mwenyekiti, naona unataka kuwasha taa, najitahidi kutaka kwenda kwa wakati, ninakushukuru mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu ninaunga mkono mswada huu wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi na nawaomba wenzangu wachangie kwa nguvu. Lakini lazima twende katika maeneo ambayo tunahisi yatatuweka katika nchi yetu katika hali ya usalama na amani baada ya chaguzi zijazo. Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima lakini pia kwa kunipatia nafasi hii ya kuchngia mswada huu wa Tume ya Uchaguzi. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta mabadiliko ya sheria hii ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuendea katika eneo la jina. Mimi ninahisi kwamba wakati umefika wa Tume hii ya Uchaguzi tuiongeze ukubwa wa jina badala ya kuitwa Tume ya Uchaguzi tu Zanzibar kwa maoni yangu mimi tungeliita Tume ya Uchaguzi na Ugawaji wa Mipaka. Kwa sababu ni moja ya kazi zake za msingi, ukiacha uchaguzi lakini Tume hii ina kazi ya msingi ya kuangalia na kugawa mipaka ya majimbo na wadi ili kufanya uchaguzi mzuri katika hali njema sana. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naona hili lingelikuwa ni moja ya jambo ambalo lingelizingatiwa.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, Tume hii ina kazi kubwa sana kwa maslahi ya nchi. Tume hii inaweza kuchafua amani ya nchi lakini pia inaweza kuendeleza amani ya nchi na maendeleo ya nchi na wanafanya kazi Tume hii wakati mwengine katika mazingira magumu sana. Kwanza hawapati bajeti yao kwa kawaida na wakikosa bajeti ya kawaida na kwa kiwango walichokihitaji inasababisha mipango yao ya kazi kuharibika sana. Mathalan mara nyingi utasikia wanataka kufanya pengine maboresho ya daftari la wapiga kura, wanataka kuingiza wapiga kura wapya, lakini mazoezi haya mara nyingi hayaendi na wakati.

Kwa sababu fedha ambazo wanatarajia kuzipata huwa hawazipati na kwa nchi kama yetu ukitegemea kwamba ufanye uchaguzi, urekebishe majimbo, uandike wapiga kura wapya kwa kutarajia fedha za wafadhili utakuwa unaharibikiwa. Kwa hivyo, wito wangu kwa Serikali najua mgawanyo wa fedha zinataka taasisi nyingi lakini wajitahidi sana kuiangalia kwamba Tume ya Uchaguzi ni moja ya Taasisi nyeti na mipango yao wanayoipanga ili iweze kufanikiwa lazima wapewe fedha za kutosha na kwa wakati.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niende kifungu namba 9 kuhusu uangalizi wa uchaguzi. Niungane na waheshimiwa wenzangu waliozungumzia kwamba kuwa na waangalizi katika uchaguzi ni jambo la lazima; wawe waangalizi wa ndani na wawe waangalizi wa nje. Lakini ipo tabia ya waangalizi zaidi wa nje kuangalia uchaguzi lakini pia kupotosha matokeo ya uchaguzi na kupotosha habari za uchaguzi. Sasa Tume wao ndio wana ruhusa ya kumruhusu mtu kuja kuwa muangalizi. Kwa maoni yangu Tume iwe makini sana na iweke adhabu za watu ambao watakuja kama waangalizi na wakaja kufanya mambo ambayo hayalingani na uangalizi wao.

Tunayo mazoea ukifika uchaguzi Zanzibar tunakuwa na waangalizi wengi kuliko upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na waangalizi wenyewe pia hawaendi kwenye mikoa ya vijijini wanabakia hapa katika Mkoa wa Mjini Magharibi katika kuleta vurugu vurugu zao. Unakula kuna waangalizi 500 Zanzibar wanafanya nini wanajaa kuliko wapiga kura na wanajaa kuliko watu wengine katika vituo vya kupiga kura. Kwa bahati mbaya waangalizi wengine wanakwenda kwenye vituo vya kupigia kura na wao pia wanatoa maelekezo wakati wao hawahusiani na uchaguzi, wao ni waangalizi wa uchaguzi na sio wasimamizi wa uchaguzi. Kwa hivyo, tunaiomba Tume iwe na utaratibu mzuri, iwe na sheria au kanuni zitakazowalinda lakini pia kutoa adhabu kwa waangalizi wa uchaguzi.

Jambo jengine ambalo nataka kuzungumzia Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu wa vitambulisho vya wapiga kura. Tume zetu hizi zina mamlaka ya kutoa na kufuta pia vitambulisho lakini mimi napenda nipendekeze kwamba kuwe na muda maalum. Kama kitambulisho cha mpiga kura kwa miezi 6 hakijachukuliwa, hicho kitambulisho kwamba ni kitambulisho mfu. Haiwezekani mtu akae Zanzibar kitambulishe chake kizagae zagae Tume mpaka 2020 ndio anakuja anasema mimi kuna kitambulisho, tunamjua alikuwa wapi, alikuwa nchi gani wakati wote mpaka kitambulisho chake kiko Tume, kwa hivyo, lazima Tume iwe na utaratibu kila baada ya miezi 6 kuvifuta vitambulisho ambavyo havijachukuliwa na wenyewe ili kuwa na wapiga kura halisi.

Matokeo yake sasa tunakwenda kwenye chaguzi tunaambiwa watu laki moja hawakupiga kura kwa sababu vitambulisho vimezagaa havina wenyewe, havichukuliwi na watu wengine huko wanapata vitambulisho kwa mpango mpango, wanakaa nje, wanakaa pengine Kenya ikifika uchaguzi anakuja kuchukua kitambulisho chake anapiga au kimekaa sehemu fulani yeye anakuja anakitumia kile na mwengine anatoka anakwenda kutumia cha mwenzake. Jimbo unalikuta lina watu elfu saba, linaambiwa limepiga watu elfu tisa. Kwa

hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba hili nalo liangaliwe sana kuwa na muda wa vitambulisho.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, tunawaelewa wanaishi wapi Tume majengo yao. Tumpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwamba juzi kazungumzia umuhimu na kaahidi kwamba kabla 2020 majengo ya Tume yataboreshwa na kuwa katika hali nzuri. Mimi nasema jambo hili au tamko hili liungwe mkono kwa vitendo. Mhe. Mwenyekiti, majengo ya Tume na zaidi ya Wilaya yako katika hali mbaya na wengi hawana hayo majengo. Ikifika wakati wa uchaguzi ama wanahamia skuli ndio Ofisi zao za Wilaya ama wanahamia maeneo mengine, Halmashauri na sehemu nyengine.

Mimi ninafikiri wakati umefika sasa kwa kila Wilaya Tume kuwa na Ofisi yake ya kudumu ambayo itakuwa na nafasi na wataweza kufanya kazi zao kwa utulivu. Na pale Makao Makuu kama lile jengo bado, maana yake kuna kipindi cha nyuma ilikuwa lile jengo walinunuwe ninafikiri wameshalinunua, kama limenunuliwa basi ninashukuru Mungu kwamba lile jengo liwe lao. Lakini kwa hao Makao Makuu ghala lao la kuhifadhia vitu vyao hawana, kwa muda wote wanakodi ghala pale Kikwajuni.

Sasa uchaguzi wa Zanzibar halafu unakwenda kukodi eneo la kuweka vifaa vya uchaguzi, hizo kura si zitapigwa huko huko halafu uje ushindwe halafu ije kuwa tabu. Kwa hivyo, Tume mimi naomba wawe na ghala lao tena la kisasa ambalo litakuwa linaweza kuhifadhi na wanaweza kuingia wenyewe peke yao sio mtu ambaye kawakodisha. Mhe. Mwenyekiti, hilo pia pendekezo langu.

Mhe. Mwenyekiti niungane na Kamati ambayo ilipitia mswada huu kwa kupendekeza kukifuta kifungu namba 15(2), kifungu hiki kilikuwa hakileti afya nzuri katika uzito na madaraka ya Rais. Kwa hivyo, kukifuta kifungu hiki hapa sina maneno naunga mkono na sasa kimekaa vizuri badala ya kuwa na 15(1) na (2) Kifungu kibakie namba 15 tu, kwa hivyo, hilo naunga mkono.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie wasadizi au wasimamizi wasaidizi wa Wilaya. Kwa kawaida yao Mhe. Mwenyekiti, hawajaajiriwa muda mwingi, kila ukifika wakati wa uchaguzi Tume inatangaza nafasi, watu wanaomba kazi wanakaa miezi 3 wanafanya uchaguzi halafu wanaondoka. Mimi ninafikiria hii pia ndio inaleta kasoro katika huu mchakato wetu wa uchaguzi. Ni vyema baada ya kuajiriwa Afisa wa Wilaya na wale maofisa wengine wa uchaguzi waajiriwe ili wawe wa kudumu na wakiajiriwa mimi naomba kama walivyosema wenzangu Mnadhim na Mhe. Hassan na hawa vijana wetu waliotumika muda mrefu tuwape nafasi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vijana wamefanya uchaguzi tangu 2005, 2010 na 2015, lakini nina hakika zikianza ajira wao watatupwa nje na wameteseka sana katika wakati mgumu. Kwa hivyo, mimi naomba kwamba wakiajiriwa pamoja na Sheria ya Utumishi lakini wale nao iwe kipa umbele cha kuajiriwa. Mhe. Waziri, hili ninafikiri tuchukulie kwamba wale vijana wamefanya kazi kubwa tukiwatupa sasa hivi tutakuwa hatujawatendea haki. Kama kuna sifa nyengine waajiriwe lakini wapewe miaka ya kutimiza sifa wazifikie ili waweze kuwa katika viwangu vizuri lakini wale vijana waweze kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine na mimi niungane mkono na wenzangu waliozungumzia kuhusu kujitangazia matokeo. Lakini naona kama adhabu hii haikuwekwa wazi wazi, ingawa katika kifungu 31 cha mswada huu wa sheria kinasema hivi ifuatavyo:

"Kama mtu yeyote ambaye kwa makusudi atatoa taarifa yoyote ya Afisi kwa mtu yeyote asiyehusika atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua laki tano na isiyozidi shilingu milioni moja au atatumikia kifungo cha mwezi 1 au adhabu zote 2 kwa pamoja".

Ninafikiri hapa ndio tunapowakamatia lakini kama ni hapa mbona adhabu yenyewe ni ndogo sana, laki tano kwa kudanganya kutoa habari za ofisi, habari za ofisi pengine ni miongoni mwa matokeo ya uchaguzi. Leo kwamba mtu akifanya kosa hili atoe laki tano mpaka milioni moja kama faini, isizidi milioni moja au kifungu cha mwezi mmoja. Lakini nchi inaathirika kiasi gani na habari zake alizozitoa, hatuoni kwamba kufanya hivi ni kuhamasisha watu waweze kutoa hizi habari. Kwa hivyo, mimi nashauri Mhe. Mwenyekiti, ninamshauri Mhe. Waziri, kifungu hiki wakiangalie sana kinaweza pia kikaleta matatizo kwa nchi yetu.

La mwisho kabisa upo mtindo kwa badhi ya watu, ama wagombea, ama wananchi kuharibu mabango wa wagombea wenzao, hii adhabu yake ikoje. Kwa sababu mgombea yeyote anakuwa kaingia gharama kutengeneza hayo mabango, kwa nini mtu aling'oe bango la mwenzangu. Kwa hivyo, ninafikiri tungeweka adhabu nayo kwa wale ambao watang'oa mabango kuwe na adhabu ambayo inawakabili.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu haya machache au mchango wangu huu mchache mimi naunga mkono kwa asilimia mia mswada huu na waheshimiwa wenzangu naomba tuchangie sana. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nami awali ya yote nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na leo hii na mimi kutoa mchango wangu japo kidogo kutokana kwamba michango mingi imeshatolewa na Wawakilishi wenzangu waliopita.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea Mswada huu wa Sheria kuhusu Tume ya Uchaguzi kuifuta hiyo sheria iliyokuwepo hapo kabla. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na michango mingi isipokuwa kwa ufupi tu mimi nilikuwa napitia hii Ripoti ya Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani ya mwaka 2015, nikaona kwamba kulikuwa na kasoro zimejitokeza na matatizo na Tume ya Uchaguzi katika ripoti yake hii wametoa mapendekezo yao lakini mimi ninashukuru sana Serikali iliyaona mapendekezo yao na wameyafanyia kazi. Moja wapo ya mapendekezo hayo ni hii sheria ambayo imeletwa hivi sasa ya kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sasa kwa kuwa serikali ina nia ya kuhakikisha kwamba yale matatizo yote yaliyotokezea katika uchaguzi uliopita hayatokezei tena, nina imani kubwa sana baada ya kuupitisha mswada huu sheria basi wale wote ambao wanahusika na utendaji wa kazi za kila siku za Tume ya Uchaguzi nao watatumia nafasi ambao sisi tumeitumia hii ya kuwapitishia sheria ili wafanye kazi zao kwa uadilifu mkubwa sana na uzalendo ili baadae matatizo ambayo yametokezea na kuigharibu taifa pesa nyingi sana yasitokezee tena.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu wa sheria mimi moja kwa moja niende katika kifungu Nam. 9, sehemu ya pili kuhusu mambo ya uangalizi. Kusema kweli mimi shuhuda jinsi gani waangalizi wa uchaguzi uliopita walivyokuwa wameelemea zaidi katika upande mmoja wa chama cha kisiasa, kiasi cha kwamba unajiuliza hawa wamekuja kuangalia uchaguzi au wamekuja tayari kuthibitisha kile ambacho wamekisema mwanzo kwamba watahakikisha chama fulani ndicho kinachoshinda.

Kwa hiyo, utaona humu kuna adhabu, adhabu iliyotolewa Nam. 5 wenzangu wamesema kwamba ni adhabu ndogo, lakini mimi nilikuwa nataka kuuliza tu hawa waangalizi wanaotoka nje ambao baadhi ya wakati hata ripoti wanakuwa hawazileti katika Tume ya Uchaguzi tunawabana vipi na sheria hii? Kwa sababu wanakuja hawa baadae hata hizo ripoti hawazileti kwetu katika hizo

siku 90, utakuta wamefika huko nje wao moja kwa moja wanatoa taarifa zao bila ya utaratibu wowote.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri akija atusaidie tutatumia taratibu gani za kuhakikisha kwamba na hawa tunawadhibiti na kama kuna hizo faini au adhabu na wao pia wanaweza kuzipata hizo adhabu. Kwa sababu kama unavyojua wengine ni waangalizi kutoka nje ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna suala hapa lilizungumziwa kwamba, iwapo itaonekana hawa waangalizi hawawasilishi ripoti zao basi watakuwa hawaruhusiwi kushiriki katika chaguzi nyengine au kura za maoni. Lakini tuangalie je, athari yake inakuwaje? Tayari mtu haleti ripoti yake anaichafua nchi ikisha baadae anapoichafua nchi inakuwa ni hali ngumu sana kuirejesha katika hali yake kwa muda mfupi. Kwa hiyo, mimi napendekeza watu hawa wachukuliwe hatua za kisheria wasiachwe hivi hivi tu ikawa wanaachiwa wasishiriki katika uchaguzi ujao. Na wao vile vile wapewe adhabu ambayo itakuwa fundisho kwa wengine wasifanye jambo kama hilo wanalolifanya waangalizi ambao kwa kiasi kikubwa wakija Zanzibar wanakuja na malengo yao tofauti na yale masharti au zile kanuni wanazowekewa na Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nikitoka hapo nakuja kwenye sifa au Ibara ya 14 kuhusu mtu anatakiwa awe na sifa gani za kuwa Mkurugenzi. Mhe. Mwenyekiti, hapa zimetajwa sifa nazo ni:

a) Ni Mzanzibari;
b) Awe na angalau shahada ya kwanza ya chuo kikuu kinachotambulika; na
c) Ni Afisa Mwandamizi katika utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeshauri kama inawezekana basi vile vile uangaliwe uzoefu wa taalamu inayohusika katika ile kazi anayoifanya yule Mkurugenzi kwa hii kada ya Tume ya Uchaguzi.

Kwa hiyo, ningeshauri kama inawezekana basi tuambiwe ile shahada yake inatakiwa ya aina gani, iwe ya *IT*, iwe ya *law* au iwe ya *administration* au uchumi lakini tuwekewe angalau tuijue ili mtu anapopewa zile sifa tunaona kweli anastahiki kwamba kuwa Mkurugenzi, kwa sababu hiki ni chombo kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi vile vile nichukue nafasi hii kuzungumza kuhusu hizi sheria zetu hasa tunapokuja katika adhabu tunazozitoa. Katika sheria iliyopita tulisema kwamba kutangaza matokeo ni kosa la jinai, japo humu katika ripoti ya tume ukiangalia Ibara ya 7, kifungu cha 2 kwenye ukurasa wa 52 katika ripoti hii walielezea kwamba kuna mgombea mmoja alijitangazia matokeo ya urais wakasema tu kwamba ni kinyume cha sheria. Sasa mimi natoa ushauri kama itawezekana kwamba hata katika *league* zetu kama timu itafanya udanganyifu wa aina yoyote inateremshwa daraja. Labda na sisi tuweke katika sheria yetu hii kwamba asiruhusiwe tena kugombea katika uchaguzi wowote ule. Tukifanya hivi hili tatizo litakuwa halitorejea kwa sababu mtu kama huyu ukimpeleka Mahakamani utaambiwa kuna ushahidi, ushahidi wake unachukua muda mrefu na baadae ile kesi hata ikienda matokeo yake tunaambiwa kwamba hii kesi ilienda Mahakamani. Kwa hiyo, mimi labda ikiwekwa sheria hiyo kwamba huyu mtu asiruhusiwe tena kugombea naona itakuwa ni fundisho tosha kwa wagombea wengine wa ngazi yoyote ile kuanzia uwakilishi, udiwani na ngazi kubwa ya urais.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu wa sheria kuna sehemu hapa imeelezea kuhusu masharti ya fedha, sehemu ya nne. Katika Ibara ya 24(2) inasema Mkurugenzi anaweza baada ya kuidhinishwa na Waziri wa Fedha kuandaa utaratibu wa kuchangia mfuko zaidi. Mimi nilikuwa nataka katika ibara hii basi lazima tuambiwe anaekewa masharti gani, je, anaandaa utaratibu wake mwenyewe tu wa kuchangia hizo fedha, kwa sababu kuna pesa nyengine unaweza ukapewa fedha na masharti ili baadae yule anayekufadhili na yeye umtekelezee yale yake. Kwa hiyo, mimi nitashauri sana katika kifungu hiki tuekewe masharti yake, je, ana uwezo wa kuandaa utaratibu wa kukusanya fedha, lakini utaratibu ambao unaaminika zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashuhuda kwamba Mhe. Rais hivi karibuni tu alienda kukagua majengo na akaonana na Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi pamoja na watendaji wake na akaelezea kwamba nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba Tume hii ya Uchaguzi inafanya kazi zake katika njia za uhuru na ufanisi zaidi na akaahidi kwamba atasaidia kufanikisha hilo. Kwa hiyo, mimi natumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais na nina imani kubwa sana tume hii nayo haitamuangusha Mhe. Rais itafanya kazi yake kwa uzalendo na uaminifu wa hali ya juu bila ya shindikizo kutoka upande wowote ule.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi kuunga mkono mswada huu na kuwaomba wawakilishi wenzangu waunge mkono mswada huu na kuwaomba wawakilishi wenzangu waunge mkono mswada huu ili Tume yetu hii ya Uchaguzi ifanye

kazi zake kwa ufanisi na vile vile nao wakijua kwamba wana dhima kubwa kwa wananchi na wao wasituangushe kabisa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia machache katika mswada ulio mbele yetu Mswada wa Marekebisho ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba moja kwa moja niende kwenye kifungu cha 9 kinachohusu uwezo wa kuruhusu waangalizi.

Mhe. Mwenyekiti, sote tutakubaliana kwamba kwa chaguzi zetu nyingi waangalizi wetu au waangalizi wanaotoka nchi za nje wamekuwa wakituletea matatizo katika kufanya kazi zao. Haya hasa yanatokana kwamba wanakuja tayari na ajenda yao mfukoni, na ajenda yao kwamba chama tawala kiondoke madarakani, hii ndio ajenda yao. Hayo wameshayafanya nchi nyingi za Kiafrika kama Kenya, Zambia na kwengineko, sasa hawaangalii mazingira ya nchi, nchi ile kwa nini chama kilichopo madarakani kinaendelea kushika hatamu? Hili ndio suala la msingi wajiulize, lakini wao wanakuja na ajenda yao mfukoni kwamba kiondoke tu, kwa hiyo, wanaiingilia tume wanapokuja kuangalia tayari wanachagua pakwenda.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kupendekeza katika Nam. 9 uwezo wa kuruhusu waangalizi kwamba tuongeze kifungu kimoja kidogo pale kwamba mwangalizi atapangiwa kituo cha kuangalia au kufanya kazi zake na tume. Kwa sababu hawa wageni Unguja na Pemba hawaijui, kwa hiyo, wakija wanajikita tu ah! Mimi nataka kwenda Dimani, mimi nataka kwenda Jang'ombe, hasemi nataka kwenda Nungwi, hasemi anataka kwenda Mkanyageni, hasemi anataka kwenda Wete hasa Pemba tumegundua kwamba hawaendi kwa nini?

Sasa Mheshimiwa nataka kushauri sana tuongeze kipengele kwamba, tume iwapangie kituo cha kazi waangalizi kama hataki muangalizi basi aende zake asitulazimishe wanajazana kwenye majimbo ya Unguja, wanajazana mfano Jang'ombe hasa haya majimbo ya Mjini Magharibi ndio wanajazana tele wanne wanne wanagongana. Kwa hiyo, tena wanafanya mikutano yao wana-*exchange notes* mle mle vituoni kuna ajenda gani? Kwa hiyo, inaonesha kuna ajenda ya siri.

Kwa hiyo, mimi naipongeza sana tume yetu ni taasisi inayojitegemea kwa hili wawe wakali sana, hawataki, kwa sababu tunaona na tume yetu hapa inapoalikwa kwengine wanapangiwa hasa *instructions* utafanya kazi moja,

mbili, tatu, nne, sio kama wanafanya wanavyotaka wao tu. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nataka kushauri kwamba suala la waangalizi tusiwape nafasi, wengi wao ni wachochezi, wengi wao hawaji kwa nia njema, wanakuja kwa uchochezi na kutugombanisha na kuingilia kazi za tume.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nirukie katika kifungu cha 16 kinahusu kazi za Mkurugenzi na hasa niende kwenye kifungu cha 16(1)(d) kuandaa bajeti na kalenda ya shughuli za tume. Naomba nimpongeze sana Mkurugenzi wa Tume kwa kazi hiyo kubwa, yeye pale ndio kama *dictionary* au ndio *working machine* ya tume. Tume inamtegemea yeye kwa utendaji wa kila siku wa kazi na yeye meno yake ni bajeti ya serikali, hana pesa yeye ukiondoa ruzuku za hawa wahisani wetu.

Kwa hiyo, mimi naomba kwanza niipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya kiongozi wetu jamadari Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kukiwezesha chombo hiki kufanya kazi zake kiufanisi, na ufanisi wenyewe ni hela. Kwa sababu Mkurugenzi yeye anapanga mwenyewe leo nitahakiki daftari, leo nitaanza kuandikisha upya, leo nitafanya nini na shughuli zote hizo zinataka pesa. Na wanapotaka pesa, *alhamdulillah*, serikali inajipinda inaua mambo mengine inamtafutia pesa. Kwa hiyo, tunaishukuru sana serikali yetu kwa hilo, kwa sababu kama tume itakuwa tegemezi kwa hawa tuliowataja hawa *donors*, kwa hiyo, itakuwa kwa kweli tume yetu haina mashiko na itakuwa inayumbushwa.

Lakini tunaishukuru sana tume yetu na serikali yetu kwamba imeiwezesha tume kufanya kazi zake vizuri katika chaguzi zote na kwa kuiwezesha bajeti. Kwa hiyo, mimi naipongeza sana serikali na nampongeza Mkurugenzi kwa hii mipango ya tume ambayo sasa kwa kweli ukizingatia na serikali yetu kugatua madaraka Mikoani wameanzisha mpaka hizo tume za Wilaya, nafikiri itakuwa jambo rahisi vitambulisho vile sasa vinapatikana Wilayani hata wao tume wanavipeleka Wilayani, ni jambo la msingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda hapo hapo kwenye kifungu cha 16(g) kinazungumzia kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi ambazo zinafanya kazi za uchaguzi, demokrasia na utawala bora. Pana maneno mazito matatu mwenyekiti hapo, ni kwamba zinafanya kazi za uchaguzi, demokrasia na utawala bora. Hizi taasisi za nje nyingi kwa kweli zikija kwenye nchi zetu wao wanakuja kuingilia mambo ya tume au mambo yetu ya ndani, huko kwao hawafanyi haya. Sasa kwa nini wanakuja kwetu kutufanyia haya? Wao wanakuja suala zima la ku-*observe* sio ku-*interfere*, sio ku-*manage* ila wao wanakuja ku-*observe*, yaani kuangalia tu, basi waangalie tu kama walivyosema

wenzangu waandike ripoti, wakishaandika ripoti kazi yao imekwisha, lakini sio wanakuja ku *dictate terms;* mfanye hivi, hivi, hivi, tutawapa pesa hizi, hizi, hivyo sivyo.

Sasa nisingependa kutaja nchi lakini tunazijua hizo nchi ambazo zinakuja na *package* zao au mashirikia ya kimataifa wanakuja na *package* zao za misaada tunazijua. Inaonekana kusema sio vizuri kuzitaja, lakini tunazijua. Wanapokuja hawa wanatwambia kabisa tutakupeni dola labda 4000 kuboresha daftari la uchaguzi, tutakupeni dolla 5000 au 200,000 kuboresha elimu ya wapiga kura. Wanakuja kwa mnasaba huo, lakini ukitizama kwa undani wanaingia kwenye tume wanajaribu ku-*dictate terms* ndani ya tume yetu. Lakini kama ninavyosema tunaishukuru tume iko *very stable* wanajua nini wanachokifanya. Sasa mheshimiwa, hiki kipengele kiko *very strong,* anasema kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje zinazofanya kazi za uchaguzi, demokrasia na utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hapa Mkurugenzi ajitahidi sana hawa asiwakaribishe kuingia maungoni au serikali isiwakaribishe kuingia maungoni katika chombo hiki, wao wana misaada yao ya mapesa, wana ushauri wao, tunashauri sana bora wawasiliane na wizara husika. Najua watakuwa wakaidi, watasema aah, sisi bwana tumekuja hapa tufanye kazi na Tume ya Uchaguzi, aah, sisi tukatae tu tusikubali kirahisi kwa sababu tunajua madhara yake, wanapoitoa pesa pale wanakusudia na wao wa-*dictate terms* wafanye moja, mbili, tatu. Na sisi hatukubali lakini tusiwakaribishe, kwa nini tuwakaribishe na tunajua kwamba *spoon-feeding,* yaani anatoa pesa yake anakusudia anakuja kufanya nini, na tumeona ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, nimejitahidi nisiseme lakini itabidi niseme, tumeona msaada tulioupata wa *UNDP,* yaani ruzuku waliotupa *UNDP* tumeshuhudia walitupa ruzuku lakini nini matokeo yake, walikuwa na watendaji wao *UNDP,* walikuwa wanafanya kazi bega kwa bega na tume, matokeo yake tumeona walivyolichezea daftari na madhara waliotuletea. Sasa mheshimiwa, nimeona bora niutaje huu mfano ambao wengine ilibidi nchi yetu ichukua hatua za kuwaondosha nchini watendaji wake wa *UNDP* baada ya kugundua hayo mambo waliyoyafanya. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hiki kipengele kwa kweli nashukuru sana kwamba kimemtaka Mkurugenzi yeye ashirikiane na taasisi, lakini sasa ashirikiane nayo kwa mantiki lakini pia ningeshauri sana misaada wasiji - *interact* moja kwa moja na taasisi hizo, wao watataka lakini sisi tuwe waangalifu sana kwa sababu madhara yake ndio kama hayao tumeyaona.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema nichangie vifungu viwili hivi na naamini vitatusaidia katika kuboresha sheria yetu hii mpya ya Tume ya Uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni waheshimiwa wote waliojitokeza kuchangia pamoja na kwamba nilishamtangaza Mhe. Suleiman, lakini muda hauruhusu hawa ambao wataendelea baadae kuchangia wakati wa jioni ataendelea Mhe. Suleiman na baadae wataendelea kufuata utaratibu kama utavyokuwa.

Sasa naomba niliakhirishe Baraza hili hadi saa 11:00 jioni. Ahsanteni sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liiliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

(Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma)

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye mswada huu wa marekebisho ya Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kifungu cha 20, "Afisa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa na kazi zifuatazo:

a) Kusajili wapigakura, na
b) Kuhamisha taarifa za mpiga kura kutoka sehemu moja na kuzipeleka sehemu nyengine..."

Mhe. Mwenyekiti, lakini ningeomba kuingia na kipengele chengine hapa, zoezi la uandikishaji wa upigaji kura liwe linaendelea kama vile vitambulivyo vya Uzanzibari Mkaazi, iwe hakuna haja ya kusubiri muda maalum kwamba watu wapatikane kwenda kuandikisha, isipokuwa kwamba hii nayo iwe ni endelevu kama vile vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye kifungu cha 29. "Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa makusudi atamzuia Mjumbe wa Tume au Mkurugenzi, au Afisa mwengine wa Tume kutekeleza majukumu yake..."

Sasa hapa naona sikuona sheria inayosema kwamba, na yeyote ambaye ataweza kumzuia mpiga kura ili kumkosesha haki yake ya kupiga kura, pia hapa ningeomba kuingia hii kwamba na yeye aweze kuchukuliwa hatua. Kwa sababu unapofika wakati wa kupiga kura matatizo mengi hujitokeza wakiwemo watu kutishwa vitisho vilivyokuwa havina maana, kupangiwa mambo mbali mbali na kusababishiwa mtu yule kuogopa kwenda kupiga kura. Pia na hili ningeomba likaingia hapa kwamba mtu yeyote ambaye atamhatarishia maisha au atamtisha mpiga kura ili asipate nafasi ile ya kupiga kura basi na yeye iwe kuna hatua kali ya kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la mgombea. Hapa Waheshimiwa wengi wamechangia kuhusu suala la mgombea, Mnadhimu pale alisema kwamba mgombea yeyote aweze kupewa kifungo cha maisha. Mimi naona hapa mgombea yeyote ikiwa wa urais, ubunge, udiwani na uwakilishi anayejitangaza bila ya tume yenyewe kutangaza kwa sababu tume ndio chombo huru chenye maamuzi ya uchaguzi, basi aweze kuzuiwa, kuwe na kanuni maalum ya kuweza kumzuia mgombea yule kwa kipindi cha muda wa miaka 15, iwe hana ruhusa ya kugombea nafasi ile aliyojitangaza.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi isipokuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Mussa: *Bismillahi Rahmani Rahym.* Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu, ingawa mswada huu unanihusu sana kwa sababu mimi mwenyewe nimo katika hii kamati husika, lakini kuna mambo mawili matatu niliyaacha nataka kuyarekebisha ili yaingizwe katika hiki kipengele kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka kuzungumzia katika kifungu cha 226(2), Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kazi yake ni kutangaza matokeo ya uchaguzi na shughuli nyengine zote, ina maana watu wote walioko kwenye tume wako chini yake, yeye ni kiongozi wa juu kabisa. Lakini la kushangaza utakuta watu wengine wanatoa matokeo kabla ya yeye kutangaza, hili ni jambo halikubaliki katika nchi yoyote na tunakuwa na utaratibu wa kuwa hatuchukui hatua katika jambo hili, tunaliona jambo la utani tu au la mzaha. Mtu anajitangazia mimi nimeshinda, umeshinda nini haelezi, umeshinda kura ngapi, haelezi; umeshinda wapi, hasemi; yeye anasema mimi nimeshinda na hakuna hatua inayochukuliwa. Hii ni kusababisha vurugu, wewe unashinda au umeshinda kwa nini humuachii ambaye ameruhusiwa kutangaza ushindi wako akatangaza na akaeleza kuwa wewe umeshinda. Hili ni jambo ambalo nimeona halikubaliki.

Jengine ambalo nimeliona linafanyika hasa kwa kisiwa cha pili ni kupigiwa kura watu ambao hawastahiki kupigiwa kura. Mtu ana *Form IV* anapigiwa kura kunawekwa kundi maalum la kupigia watu kura, ina maana ukishampigia mtu kura umemnyima haki yake ya kuchagua kiongozi anayemtaka, anakwambia mimi imekuja simu kutoka Unguja tumchague fulani kama hutaki kumchagua fulani basi ina maana wewe si mwenzetu, tupe kura yako tukakupigie kura na masikini kwa sababu anaogopa ama atagomewa au atafanyiwa mambo ambayo sio anakubali anatoa kitambulisho anakwenda kupigiwa kura; iweje mtu ana *Form IV* apigiwe kura. Hiki ni kipengele nacho kinatakiwa kiwekwe, haiwezekani hata siku moja kijana wa miaka 25 aweze kupigiwa kura, mambo haya yanatokea kule kwetu. Hilo ni jambo ambalo niliona kidogo niliweke sawa nililisahau katika haya majumuisho yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nataka niwaombe Wawakilishi wote waliomo ndani ya jengo hili hasa wale wazoefu wauchangie mswada huu. Kwa sababu mswada huu ni muhimu sana na mswada huu sio wa kuunyamazia kimnya kwa sababu ndio mswada ambao unaweza kuleta matatizo katika nchi yetu. Kwa hiyo, wale Waheshimiwa ambao hii ni mara ya pili kuingia katika Baraza hili wana uzoefu mkubwa nawaomba sana wajitokeze kuuchangia mswada huu, wasikae kimnya, huu ni mswada muhimu sana, sio mswada mdogo, mswada huu ndio wenye usalama wa nchi yetu, nchi nyingi zimeingia kwenye matatizo kwa sababu ya uchaguzi.

Jambo jengine nataka nizungumzie habari ambayo imekuwa maarufu katika nchi hii kudanganya watu. Wewe unadanganya watu, unawaweka watu katika wasiwasi, unaifanya nchi iwe katika wasiwasi. Wizara zote sasa hivi hazifanyi kazi kutokana na matokeo haya, kila mtu anangojea tarehe 15, 25, 30 ndio patoke matangazo. Uchaguzi umekwisha, matokeo yameshatokea, wewe unangojea tarehe 15 unawafanya watu wasimamishe shughuli zao, unawafanya watu katika idara wasiwajibike kwa sababu wanaambiwa kuna tarehe 15 au 25 na kipengele hiki kiwekwe hapa ili mtu yeyote atakayetoa tarehe zaidi ya ile iliyotangazwa na rais aliyetangazwa naye awe mkosa katika makosa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema mwanzo kwamba kwa kuwa huu mswada unanihusu na mimi ni mhusika mkuu na ndiye ambaye nilikaa na kamati, nataka niwaachie wenzangu wachangia na mimi nikae kitako.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, lakini nawaomba sana, tena sana wale wawakilishi wenzangu ambao wana uzoefu wasimame kuuchangia huu mswada, ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa hii kuweza kuchangia mswada huu, mswada ambao una umuhimu wa kipekee katika kuleta au kusimamia uchaguzi huru, haki na kidemokrasia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na wenzangu kuchangia mengi kuhusu mswada huu, mimi ningependa kuchangia katika vipengele vinne. Kwanza nianze na kipengele cha Daftari la Wapiga Kura ambalo mara nyingi inaonekana *dhahir shahir* kwamba hata Tume ya Uchaguzi nayo ikifika wakati wa daftari lile kupewa watu wa vyama husika basi utakuta kuna chama chengine kinapewa mwezi mmoja kabla tena karibu daftari la *origin*, lakini vyama vyengine vinasota kupata daftari lile kujua wapiga kura wao.

Hii inatokea na naomba katika mswada huu kuweko kipengele maalum cha kuhakikisha kwamba tume yenyewe au Sheria ya uchaguzi inatoa haki kwa vyama vyote kupata daftari lile mapema iwezekanavyo, ikiwezekana siku moja, saa moja badala ya kupewa vyama vyengine wiki mbili au mwezi mzima kabla ya vyama vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu kuna mambo ambayo yanafanyika ambayo yanahusika na Tume hii ya Uchaguzi au Sheria ya Uchaguzi. Wakati wa uchaguzi unapofika kunakuwa na vitisho vingi ambavyo vinanyima uhuru wa wananchi kupiga kura kwa sababu wanatishwa, wanakuwa waoga, wengine wanashindwa kwenda kupiga kura. Naomba sheria hii nayo iingizwe kwa ukamilifu kuhakikisha kwamba wananchi wote wa nchi hii wanakuwa huru kwenda kupiga kura na kusiwe na chama ambacho pengine kina wafuasi wa kutisha wafuasi wa chama chengine. Hii inapunguza haki na uhuru na uchaguzi wa demokrasia ya kweli.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi pia kunakuwa na uharibifu, tumeona mazowea mengi na hususan kule Pemba, kuna vyama vinazuwia mpaka vyakula vya vyama vyengine vya mawakala wao kwenda kula wakati wanasimamia uchaguzi, wanamwaga, wanazuwia gari, wanavunja gari, lakini hakuna hatua ambazo zinachukuliwa au sheria maalum iliyowekwa kuweza kusimamia uharibifu ule. Naomba mswada huu uzingatie hayo pamoja na kipengele cha vitambulisho vya kupigia kura.

Mhe. Mwenyekiti, vitambulisho vya kupigia kura kunakuwa na mashaka kidogo. Baadhi ya vyama vinapata vitambulisho haraka sana, haidhuru ndivyo vinavyopiga kelele mwanzo kwamba kuna wafuasi wetu hawajapata vitambulisho, lakini utakuta vyama vyengine hata ile kupata vitambulisho vyao

inakuwa tabu na hii inakwenda upande wa watendaji wa Tume ya Uchaguzi, wanakuwa na shida zao. Ni vyema ingehakikishwa kunawekwa mswada maalum wa kuhakikisha hawa watendaji wa Tume ya Uchaguzi nao wanatenda haki au wanakuwa waaminifu katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimalizie na kipengele cha mawakala. Tumeona kuna mazowea makubwa katika uchaguzi uliopita, mawakala wa vyama vyengine wameshindwa kupata vitambulisho vyao kwa wakati na imesababishwa na watendaji wa Tume ya Uchaguzi, wanawacheleweshe kwa makusudi kule uchaguzi umeshaanza mawakala wale wameshindwa kuingia ndani kwenye vyumba vya kusimamia vyama vyao, matokeo yake wamefanya wanavyotaka kwa sababu mawakala wa vyama vyengine hawamo. Hii inaleta utata Mwenyekiti, mimi naomba mswada huu ungezingatia na kupitisha vipengele hivi vikawekewa sheria kwamba yeyote atakayevunja au kuharibu uchaguzi basi achukuliwe hatua inayopaswa asiachwe tu.

Mimi napenda kuungana na wenzangu kwa mswada huu na kuwapongeza walioleta mswada hapa kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu ndio chombo pekee kinachoweza kutunga sheria au kupitisha huu mswada baadae ukawa sheria kamili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu na nawaomba wawakilishi wenzangu tuupitishe haraka ili sheria hizi zitumike tuweze kupata uchaguzi huru, wa haki, wa demokrasia na tuondoe ile zana ya kwamba kuna watu wanaweza kuingia Tume ya Uchaguzi wakafanya wanavyotaka. Wenzangu wamesema mengi nayaunga mkono, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu wa mabadiliko ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuweza kushirikiana pamoja na serikali na kukaa na kuamua kuweza kutuletea mswada huu ambao una umuhimu mkubwa kwa wananchi wa visiwa viwili vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia mswada huu nije kipengele cha 23 kinachosema;

"Tume ya Uchaguzi ipewe mamlaka ya kuweza kutumia fedha wenyewe kwa ajili ya kuendeleza ofisi zake za wilaya na kuweza kujenga

majengo ambayo yataweza kudhibiti vifaa vya uchaguzi, kama vifaa ambavyo vinatakiwa asiruhusiwe mtu yeyote kuweza kuvikabili ili kuweza kufanya ubadhirifu ambao utahatarisha maisha ya wananchi pamoja na serikali".

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye maafisa wa wilaya. Maafisa wa Wilaya tukiangalia Mkurugenzi ndiye atakayewateuwa maafisa hao, lakini mapendekezo yangu ni kwa kushirikiana pamoja na serikali. Kwa sababu maafisa hawa lazima iweko *gender;* kuwe na upande wa wanawake na wanaume kwa sababu na wanawake nao wanaweza kutekeleza wajibu wao kwenye shughuli za serikali hususan kwenye Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema hivyo, Mhe. Waziri kama tunavyojua chaguzi zetu nyingi huwa zina harakati nyingi ambazo zinakiuka maadili na hususan upande wa wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umekuja wakati ambao ni muwafaka kwa sababu mwaka 2020 kutakuwa na uchaguzi. Hivyo uchaguzi huo uwe wa haki na huru.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele tuangalie wakati wa uchaguzi kunatokea matokeo mbali mbali, huwa wanajipanga watu ambao wanahatarisha maisha ya wananchi kuweza kwenda kijijini na kuweza kuzunguka nyumba za wananchi na kubuni mbinu ambazo hazistahiki kwenye serikali au kwenye jamii. Huwa wanapanga mipango ya kubuni mbinu za kwenda kuwatilia moto wananchi magari yao na kuwapiga, kuwe na kitengo maalum kwenye mswada huu ili yeyote yule atakayekuwa na shutma mbali mbali za kuwakabili wananchi na kuwahatarishia maisha wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Waziri suala hili kwa upande wa wanawake huwa tunapata usumbufu mkubwa sana. Kwa hivyo, kuwekwe mikakati thabiti kwenye mswada huu, ili mtu yeyote yule atakayefanya fujo kwenye ofisi za majimbo na maeneo mengine achukuliwe hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nije kwa wale wanaojitangaza wakati wa uchaguzi kabla matokeo hayajatokea, hata kama amekuwa ni kiongozi yeyote yule hatuchagui kama huyu yuko upande huu ama upande ule, kwa sababu lazima sheria ifuate mkondo wake, anapojitangaza basi achukuliwe hatua za kisheria na ikifika wakati aweze kuzuiwa kugombea kwa miaka 20 asigombee tena mtu kama huyo aliyejitangaza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele kwa sababu mswada huu una umuhimu mkubwa, tumetakiwa tuuchangie na kila mmoja wetu asimame hapa kuunga mkono mswada huu, kwa sababu mswada huu unatuokoa sisi wananchi wa Zanzibar wa visiwa viwili vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bihindi Hamad Khamis. Sasa namwita Mhe. Mussa Foum Mussa, akifuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa ya kuchangia mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka nianze kwa kuupongeza huu mswada, mswada umekuja katika wakati muafaka na ni vyema tukauunga mkono mswada huu.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nianze kwa kusema hivi, Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ina katiba na ina sheria mbali mbali kama hizi ambazo tunazizungumza hivi sasa. Lakini ninavyofahamu mimi kwamba tunapotunga sheria, basi sheria hiyo inamdara mtu yeyote wa nchi hii. Sasa mimi naomba tu kwamba tuelezwe kwa sababu hapa ndio pahala maghususi pa kuelezwa sisi pamoja na wananchi wetu, kwamba tumefanya uchaguzi mwaka 1995 lakini kuna baadhi ya watu walijitangaza, tumefanya tena uchaguzi huu uliopita vile vile kosa limetokea, tunataka tuelezwe je, ni hatua gani serikali imechukua juu ya jambo hili? Kwa sababu tunapitisha sheria hapa na zinavunjwa na hazichukuliwi utaratibu kama ulivyopangwa, itaonekana kama serikali haichukuwi hatua.

Kwa hivyo, kama walivyoeleza wenzangu kwamba mtu yeyote atakayejitangaza basi ikiwa hatuwezi kumchukulia hatua, basi angalau pawe na gogo la kwamba pindipo mtu akijitangaza basi kwa uchaguzi ujao asiruhusiwe kugombea, kwa sababu inaonekana kuchukua hatua hatuwezi, basi angalau akigombea itakuwa kuna yule mgombea mwenzake atamkatia rufaa angalau hicho kitakuwa kizuwizi. Lakini makosa kila wakati yanarejewa rejewa, labda kuna watu fulani ndio wanaotungiwa sheria hizo wengine haziwahusu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nikija katika kuuchangia mswada huu, mimi naomba nianze kwenye sura ya kwanza katika namba 2 ufafanuzi, katika neno "jimbo". Hapa katika mswada jimbo maana yake, naomba ninukuu;

"Jimbo maana yake ni kuhusiana na uchaguzi wowote isipokuwa wa Rais".

Katika maelezo ya hapa inaonesha hiki kifungu hakifahamiki vizuri. Sasa mimi naomba iandikwe hivi; "Jimbo maana yake ni eneo la uchaguzi lililotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar", nadhani kwa kuiweka hivyo basi itafahamika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile niende katika ukurasa wa 228, kifungu cha 8(3), naomba ninukuu;

"8(3) Taasisi yoyote itakayopewa kibali cha uangalizi chini ya kifungu hiki itatakiwa kuwasilisha kwa Tume Ripoti ya Uangalizi inayoelezea namna ya uchaguzi au kura ya maoni ilivyoendeshwa na mapendekezo yake ndani ya siku 90 baada ya kutangazwa kwa matokeo".

Vile vile, 8(4) inazungumza;

"8(4) Taasisi yoyote ya uangalizi itakayoshindwa kuwasilisha ripoti ya uangalizi katika kipindi kilichoelezwa katika kifungu cha (3) cha kifungu hiki, haitopewa kibali cha uangalizi katika uchaguzi au kura ya maoni zinazofuatia"

Mhe. Mwenyekiti, kwa maoni yangu mimi adhabu hii ndogo, kwa kusema kwamba mtu amekuja hapa ameangalia muda uliowekwa hakupeleka ripoti kwamba anyimwe kibali kwa uchaguzi ujao, hapa tutakuwa hatujafanya kitu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwanza hizi taasisi zinazopewa vibali ziangaliwe zimekuwa utitiri mwingi. Inaonesha watu wanajiingiza kwenye taasisi na wanaomba maombi kwenye Tume ya Uchaguzi ili wapate kuangalia kwa maslahi yao wao. Kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba taasisi yoyote itakayokwenda kinyume na vifungu hivi, basi angalau ile itakayoshindwa kuleta ripoti basi angalau faini yake ianzie shilingi 500,000/-, isiwe tu kwamba kunyimwa kibali tu kwa kipindi kijacho, hiyo itakuwa kila mtu anaweza kuona aah! kwa mara nyengine naweza nikabadilisha jina.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, niende katika ukurasa huo huo, kwenye uwezo wa kutunga kanuni na miongozo katika kifungu cha 10. Hapa naomba pia ninukuu;

"10. Tume inaweza wakati wowote mazingira yatakapohitajika"

Hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, naomba isomeke hivi; "Tume inaweza wakati wowote kuweka mazingira yatakapohitajika". Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, pia naomba kwamba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote wachangie huu mswada ili upate baraka kubwa kwa sababu ni muhimu sana.

Vile vile, naamini kwamba sheria hii itapita, lakini itakapopitishwa basi yale yote yaliyozungumzwa kwenye mswada huu basi yafanyiwe kazi kama yalivyoelezwa. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa kuweza kuuchangia mswada wetu huu, ambao utatuletea manufaa makubwa sana kwa tunavyotegemea kwa wananchi wa Zanzibar, lakini kwa nchi yetu yote kwa ujumla.

Kwanza kabla sijaanza kuuchangia mswada huu, ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kwa umoja wetu, tuupitishe mswada huu bila ya kuwa na gati gati yoyote, kwa sababu tumeona baada ya kuusoma mswada huu wa marekebisho kwamba kutakuwa kuna manufaa makubwa sana juu yetu. Kwa hivyo, ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe sote tuunge mkono mswada huu na tuupitishe kwa nia safi ili ulete mafanikio makubwa juu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nianze kuuchangia kidogo mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Mswada unasema kwamba ni Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Kwa hivyo, kwa vile tunafuta yale yaliyopita nyuma bila shaka haya yanayokuja mbele yatakuwa ni mazuri na yenye manufaa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia moja kwa moja kwenye ufafanuzi. Kwenye kifungu hiki kuna kipengele kinasema kwamba 'mgombea' maana yake ni yule mtu aliyepewa mamlaka na Tume, kwa hivyo, ni kwamba keshaidhinishwa na Tume kwamba yeye ndiye atakayegombea. Kwa hivyo, kama keshaidhinishwa na Tume kwamba yeye ndiye atakayegombea, basi ana uhuru pia wa kusubiri ile ile Tume ndio imtangaze ili yeye awe ndio mgombea. Atakapotangazwa na Tume tayari atakuwa mgombea na atakapotangazwa na Tume tayari atakuwa ndio mshindi. Kwa hivyo, kama Tume haijamtangaza kwenye kushinda basi hajakuwa mshindi, na kama imemtangaza kwenye kugombea basi afanye kazi yake ya kugombea mpaka pale itakapomtangaza kwa nia nyengine kama ya ushindi ama kushindwa, ndipo atakapojijua. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini pia kuna kipengele kimesema kuhusu afisa wa uchaguzi. Kuna afisa anayesimamia uchaguzi ndani ya wilaya. Kwa hivyo, tunafahamu kwamba ndani ya wilaya zetu zote kuna maafisa wanaosimamia huu uchaguzi. Lakini pia tufahamu kwamba hawa hawa maafisa wanaosimamia uchaguzi ndani ya wilaya, bila shaka na ndani ya majimbo pia watakuwa wanahusika, kwa sababu jimbo limo ndani ya wilaya. Kwa hivyo, kama wamepewa kazi hii ya kusimamia uchaguzi mzima, tangu wa kura za maoni mpaka mkubwa, basi waifanye hii kazi kihaki lilahi, kwa sababu tumeyaona mengi yanayofanyika kinyume na hizi taratibu.

Kwa hivyo, kwa vile tunafanya marekebisho ya sheria hii, tungeiomba wizara husika ilisimamie hasa suala hili la maafisa wa wilaya, kuanzia mwanzo wa kura za maoni, na mpaka kumalizia kwenye uchaguzi mkubwa, kwa sababu kuna malalamiko makubwa sana ya ubovu unaofanyika na unaotendeka katika kipindi hiki cha tangu kura za maoni mpaka kumalizikia uchaguzi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia suala la vitambulisho ndani ya mawakala. Tunafahamu kwamba kunakuwa kuna mawakala wanaosimamia uchaguzi, kwa sababu kama afisa yeye haendi kusimamia kule ndani ya darasa au ndani ya kile kituo, yeye ni utaratibu mzima wa kuhusu vituo vyote. Lakini kule kwenye vile vituo tunafahamu kwamba kunakuwa na mawakala na humu kwenye sheria yetu hii pia tumeona kuhusu masuala ya fedha, kwamba fedha zinatolewa kwa sababu ya masuala ya uchaguzi kwamba zitumike kwenye taratibu zote zinazohusu uchaguzi, lakini utakuta wale mawakala wanaosimamia ule uchaguzi wenyewe mpaka anamaliza ule utaratibu wa kusimamia uchaguzi, humjui yeye kama kaajiriwa au kapewa ile kazi kwa malengo gani au kwa namna gani.

Mhe. Mwenyekiti, utamkuta mtu yule anashughulika kule hata yule aliyepewa madaraka makubwa huko juu, anahangaika kuifanya kazi ile mpaka anahakikisha keshaimaliza, na inawezekana akawa hajalala kwa usiku miwili, lakini bado ukakuta zile ruzuku zake anazostahiki hazipati, na sijui kwa vifungu gani na sijui kwa taratibu gani, wakati tunafahamu kwamba kile kitu tayari kimeshaangaliwa na kimeshatayarishwa na vihusika vyake vyote vinakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeiomba sana wizara ilisimamie hili kwa hali zote na kuhakikisha kwamba hii kazi inafanyika kihaki lillahi, lakini na hawa wafanyakazi wanapata ile ruzuku yao kihaki lillahi. Kwa sababu tunaambiwa unapoifanyakazi kwa moyo, basi pale pale kabla jasho lako halijafutika upewe mafao yako. Kwa hivyo, juu ya hili na juu ya marekebisho haya, tunahakika

kwamba suala hili litakuwa ndio mwisho hapo lilipoishia, kwa yanayofuata sasa hivi tutakwenda na utaratibu mzuri *In shaa Allah. (Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Majukumu ya Tume. Tumeambiwa kwenye Majukumu ya Tume kuna kusimamia na kuendeleza mwenendo mzima wa uchaguzi, kuanzia kura za maoni mpaka kura kubwa. Majukumu ndio hayo hayo tunayoyazungumza, kusimamia majukumu ni tangu kuanzia vipande vya kupigia kura, tunafahamu kwamba kuna vipande vya kupigia kura, lakini kuna wale wahusika ambao wanatakiwa wapewe vile vipande vya kupigia kura. Tunafahamu kwamba kuna baadhi ya wapiga kura wakati wa kutafutiwa hivyo vipande wanadhalilika sana, kwa sababu kuna mambo yanafanyika juu ya mpiga kura wakati wa kupata kile kitambulisho chake mpaka akakipata na hapo wakati wa kukipata kuna watu ambao wanavifanyia vile vipande mambo ambayo hayastahiki. Mtu anakwenda kumlazimisha mtu kwamba lazima ampe yeye na kama hakumpa basi atamchinja.

Kwa hivyo, tunaomba sana serikali isimamie suala hili na kuwadhibiti hawa watu ambao hawapendi maendeleo ya taifa letu. Kwa sababu utakapomlazimisha mtu sifikirii kwamba utakuwa unamtendea haki, na tunafahamu kwamba kupiga kura ni haki ya kila mtu na kila mtu ana haki yake ya katika kufanya jambo ambalo liko sawa. Kwa hivyo, sioni kama kuna haja ya lazima kumlazimisha mtu kwamba yeye lazima ampe kitambulisho chake aende akampigie kura. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala moja ambalo linakuwa ni chachu kubwa sana. Katika mswada huu wa marekebisho, kwenye vipengele ambavyo nimejaribu kuvipitia vyote sijaona suala linalohusiana na Masheha wa Shehia. Tunafahamu kwamba kwenye mawilaya kuna maafisa wa wilaya, lakini ndani ya majimbo kuna masheha na tunafahamu kwamba masheha na wao ni wasimamizi wakubwa wa uchaguzi. Kwa hivyo, tunaiomba wizara iwatizame masheha na wawekewe kipengele chao maalum ambacho kinawagusa moja kwa moja masheha juu ya suala la uchaguzi. Kwa sababu tunawaona jinsi masheha wanavyodhalilishwa na baadhi ya vyama kuhusiana na suala la uchaguzi, inafika hadi sheha anasimamishwa katikati ya mlango anaambiwa huna ruhusa wewe kama nani, wakati sheha anatambuliwa na serikali nzima kama yeye ni sheha wa shehia. Kama yeye ni sheha wa shehia ndiye anayesimamia shehia ile pamoja na kituo kile, japokuwa wapo wasimamizi wengi wakuu wa vituo na mawakala.

Kwa hivyo, masheha wana umuhimu ndani ya wilaya wa kusimamia masuala yote yanayohusu shehia, na hili la kuhusu masuala ya kura nayo wawekewe

kipengele chao hasa kitakachowaonesha masheha umuhimu wao juu ya suala la kupiga kura na kusimamia masuala ya vipande vya wapiga kura wote, sisemi wa chama fulani ni wapiga kura wote *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba kuna mengi ya kuzungumza juu ya mswada huu, kwa sababu tumeona kwamba una manufaa makubwa, endapo utafanyiwa marekebisho haya na yakafanyiwa kazi kihaki lillahi.

Lakini niwaombe sana kwamba huu Mswada ni wa kwetu na umekuja katika kipindi muafaka ambacho kinaweza kutupa tija na manufaa makubwa juu yetu, nawaomba Waheshimiwa wenzangu tuunge mkono Mswada huu na tuupitishe kwa moyo mmoja na kwa nia safi ili ulete manufaa na tuweze kusaidiana kushirikiana kuhusiana na kuyarekebisha haya yote yaliyokuwemo ndani ya Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme naunga mkono hoja asilimia mia, ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya kuchangia Mswada huu uliokuweko mbele yetu, pia nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuweza kutuletea Mswada huu ambao umekuja wakati muafaka.
Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia Mswada huu katika kifungu cha 11 ambacho kinasema;

"Kutakuwa na Afisi itakayojulikana kuwa ni Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar".

Namba mbili ikasema kwamba;

"Afisi hii itakuwa taasisi inayojitegemea endelevu na yenye mhuri wake na jina, pia itakuwa na uwezo wa..."

Imeeleza hapa uwezo mbali mbali ambao. Mfano katika kifungu (a) kinasema;

"kutakuwa na kushtaki na kushtakiwa".

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tumesema kwamba hii itakuwa ni taasisi ya kujitegemea, lakini ukiangalia vifungu hivi haionekani kwamba hii ni taasisi ambayo itakuwa inajitegemea, haionyeshi kwamba kweli sheria hii inaipa taasisi hii kuwa ni taasisi inayojitegemea kutokana na muundo huu ambao tumeuona hapa. Taasisi inayojitegemea kuna baadhi ya mambo inatakiwa lazima yawemo lakini sheria hii haionyeshi hivyo, kwa sababu taasisi inayojitegemea inatakiwa kwanza ionyeshe muundo wa utumishi kwa ile taasisi

ambayo inajitegemea. Lakini katika Mswada huu haionyeshi hilo, pia taasisi inayojitegemea kunatakiwa kuwe na Tume ya Ajira.

Halafu pia kutokana na unyeti wa taasisi hii kunatakiwa kuwe na Tume au Kamati ya maadili na nidhamu, kwa sababu tumekuwa tukiona mambo mbali mbali yanajitokeza na ndio maana Serikali ikaamua kutuletea huu Mswada ili tuweze kurekebisha, kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninachoomba kwamba Mswada huu uonyeshse hasa kama kweli taasisi hii ya Tume ya Uchaguzi ni taasisi ambayo tunataka ijitegemee kikweli kweli. Na ili iwe taasisi inayojitegemea inatakiwa tuipe nguvu ya kisheria na tuweze kuingiza vipengele ambavyo nimevitaja hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja katika kifungu cha 18 kifungu hiki kinasema;

"Kutakuwa *Secretariat* ya Tume ambayo itakuwa na jukumu la kusaidia Tume katika utekelezaji wa Majukumu yake".

Halafu namba 2 inasema;

"*Secretariat* itaundwa na Wajumbe wafuatao".

Sipingi muundo wa hawa wajumbe lakini ninachotaka kuongeza ni kwamba nahisi huu muundo hauna tatizo lakini lazima uwe na sifa na hapa sifa za hao wajumbe wanaotakiwa kuunda hii *Secretariat* haimo, ili kuwe na *Secretariat* madhubuti ni lazima kuwe na sifa ambayo itaweza kupatikana kwa wajumbe...

(Hapa palitokea tatizo katika microphone)

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, samahani nilisahau kuwasha *microphone* ina maana kwenye *Hansard* itakuwa haikuingia. Kwa hiyo, ningeomba kiongezwe kifungu ambacho kitaeleza sifa za wajumbe hawa wa *Secretariat* ili tuweze kupata wajumbe ambao watakidhi haja katika *Secretariat* ya Tume.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakwenda kifungu cha 32 ambacho kinasema;

"Malipo ya Wajumbe na Maafisa wa Tume watalipwa kutoka mfuko mkuu wa Hazina kwa kiwango ambacho kitaamuliwa na Rais".

Namba mbili inasema;

"Bila ya kujali kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu hiki Afisa wa Tume atalipwa mshahara kama itakavyoamuliwa na Tume kwa mujibu wa masharti haya ya fedha za umma".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuchangia hili kwamba kifungu hiki ni kifungu ambacho kinawagusa moja kwa moja Makamishna wa Tume ya Uchaguzi ambao ni wateuliwa wa Rais, sasa mimi nilikuwa naomba kiongezwe kifungu hapa. Kwa sababu naona hapa tumeshuhudia kadhia mbali mbali zinatokea kwa Makamishna waliotangulia huko nyuma, kwa hivyo, mimi ningeomba kuongezwe kifungu ambacho kitasema, "Mjumbe yeyote atasita kulipwa pale ambapo atagoma kufanya kazi na Mwenyekiti wa Tume ataridhia kutoshiriki kwake".

Mhe. Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu kumekuwa na Makamishna wa Tume lakini kumetokea masuala mbali mbali na Makamishna hao wamekuwa hawashiriki kikamilifu katika shughuli za tume. Lakini ikifika siku ya malipo wanakwenda na pesa wanachukua wakati hawafanyi kazi. kwa hivyo, mimi ningeomba kifungu hichi kiongezwe.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda moja kwa moja nikisema kweli wenzangu waliotangulia wamesema katika sheria hii hamna kipengele ambacho kimewaona Masheha. Masheha ni muhimu sana katika taifa letu Masheha ndio wanaojua kaya moja baada ya moja, Masheha ndio wanaojua kila kitu, wanajua yupi anastahiki na yupi hastahiki, kumekuwa na upenyezaji mkubwa wa wananchi wakati wa kupiga kura.

Lakini nani anayemjua huyu ndiye na huyu siye ni Sheha, kwa hivyo, mimi ningeomba Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri kipengele hichi cha masheha wakionyeshe kwenye sheria hii kwa sababu Masheha sisi kama sisi sio Wawakilishi, sio maafisa wa Wilaya, sio maafisa wakubwa wa Tume hatuwezi kuwajua wananchi, Serikali imeamua kuweka masheha kwa makusudi ili iweze kuwasaidi na masheha ni waajiriwa wa Serikali.

Kwa hivyo, kwa maoni yangu mimi nahisi kwamba Masheha ni watu ambao muhimu sana katika sheria hii, kama walivyotangulia kusema wenzangu Masheha wamekuwa wakidhalilika sana, mwanzo walikuwa wanafanya kazi vizuri na tume lakini baada ya kuondoshwa ikawa hawashirikishwe vizuri kwenye uchaguzi, kwa hivyo, mimi ningeomba kipengele cha Masheha kionyeshwe moja kwa moja katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kumsifu tena Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta Mswada huu na mswada huu umekuja wakati muafaka, kwa hivyo, naomba wajumbe wenzangu wote tuunge mkono Mswada huu na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Kwa niaba ya

wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja Mhe. Mwenyekiti Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa fursa hii na mimi nianze kutanguliza kwa kuunga mkono mia juu ya mia kabla sijaendelea kuchangia sheria hii. Lakini katika mchango wangu kwenye sheria hii iliyoko mbele yetu naomba nichangie katika ukurasa wa 228 kifungu Nam. 8 inaposema; Uwezo wa kuanzisha kamati za ushauri. Ushauri wangu na mimi mapendekezo yangu katika kamati hizi jinsia izingatiwe, jinsia isije ikaachwa nyuma tukaonekana kwamba wenzetu hawa wa jinsia ya upande mwengine inayogeuka na mimi wakaachwa pembeni, hawa ni wenzetu nao katika kuteuliwa tume hizi kuanzisha kamati hii ya ushauri na wao wawemo wana mashauri mazuri sana. Kwa hivyo, naomba sana katika kutekelezwa sheria hii hilo nalo lizingatiwe.

Lakini pia niende katika ukurasa huo huo kifungu namba 9 kinachosema;

"Tume itatoa miongozo ya masharti kwa taasisi waliyopewa kibali cha uangalizi".

Mhe. Mwenyekiti, kwa sheria hii, mimi nashauri kwamba taasisi zile ambazo kuwa zitaonekana zina mwelekeo wa kushabihikia mambo ya siasa basi vibali vifutwe mara moja, viache kazi ya uangalizi na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa taasisi ambayokuwa itaonekana imepoteza muelekeo wake.

Nichangie katika kifungu kidogo namba 5 cha sheria hii katika ukurasa wa 228, kinasema;

"Mtu yeyote au taasisi yoyote itakayofanya uangalizi wa uchaguzi bila ya kibali cha tume itakuwa imetenda kosa".

Hapa naomba katika kifungu hichi iongezwe 'kosa la jinai' na ikipatikana hatia itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu, na isiyozidi milioni tano, hapa naomba isipungue, kulipa fedha hizi milioni tatu au milioni tano bali iongezwe na kifungo kisichopungua mwaka mmoja au miaka mitatu au vyote viwili viende pamoja, nashauri sana ili kuongeza makali ya sheria hiyo.

Vile vile, nichangie katika ukurasa 229 katika kifungu Nam. 12 kinasema;

"Kutakuwa na Nembo ya Muhuri wa Afisi ya Muundo na namna ambayo itaamuliwa na Tume".

Hapa Mhe. Mwenyekiti, ndipo pahali ambapokuwa pameweza kutugharimu sana katika taifa letu hili, leo tumeona wakati wa uchaguzi uliopita watu

wanakataa kutia saini fomu ya matokeo ya Urais, kwa macho yangu nawakuta hivi hivi mawakala wanaambiwa msitie saini. Matokeo yake kumbe kuna fomu nyengine zinazotayarishwa huku na kupelekwa katika Afisi za Tume, kwa hivyo, hapa tunasema kwamba kutakuwa na muhuri. Hili jambo la muhuri tuwe makini sana nani atakuwa nao na udhibiti wake uwe mkubwa.

Kwa hivyo, Waziri husika ahakikishe kwamba wanaokuwa na muhuri huu hakuna mjadala ni sawa sawa na silaha hii, silaha hii itatumiwa kwa kuumizwa ambayekuwa hayupo mbele yake pale itatumika vibaya. Kwa hivyo, muhuri ni jambo muhimu lakini uzuiliwe vizuri sana, zisije zikatengenezwa fomu za bandia na baadae zikatumika kwa njia ya matokeo kama zilivyopita hapa, nimeona kwa macho yangu zimepita fomu za Rais wakiambiwa wasitie saini kumbe wana lao jambo wenzetu wengine wasioitakia mema nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa 231, kifungu 19 (2) kinasema;

"Afisi ya Uchaguzi wa Wilaya utaajiriwa na tume kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma"

Naomba Waziri atakapokuja hapa anieleze uajiri huu utakuwa wa kudumu au wa muda mfupi? Kwa sababu yote ni ajira inawezekana mtu awe katika nafasi hii ni muajiriwa wa Serikali au nje ya ajira ya Serikali. Kwa hivyo, atakapokuja Waziri naomba sana atoe maelezo namna gani uajiri huu utakuwa katika tume hiyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika sehemu ya nne kuhusu Masharti ya Fedha. Naomba nichangie katika kifungu 24(1) kinasema;

"Kutakuwa na fedha za Tume ambazo zitajumuisha ambazo fedha hizo zitaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi"

Hapa Mhe. Mwenyekiti, nimepata kuona kwamba wenzetu waliokuwa wanafanya kazi ya Tume wakati wa uchaguzi wanavyopata tabu wanawajibika kufanya kazi lakini maslahi yanakuwa hayafiki kwa wakati, wakati Baraza tumeshaidhinisha fedha hizo zitumike lakini nimeona kwa macho yangu jinsi hata chakula wakati mwengine watumishi wa Tume wanakuwa hawana, ni masikitiko makubwa sana nilipoona uchaguzi uliopita ninawakuta watumishi wa Tume hawana wa kuwapa chakula, tukiwa sisi wagombea tunaogopa hata kuwapa kwa sababu tunaambiwa tutatia kampeni. Lakini wanakula mikate mikavu kama vile wamekata kimio kwa maji ya *drop* wakati fedha za Tume zipo kwa nini iwe kama hivyo.

Kwa hivyo, ni jambo lililonisikitiha sana sana, naomba kwamba inapofika wakati wa uchaguzi Tume ihakikishe kila linalostahiki la watu hawa wanapatiwa mapema na wao waweze kuweka pesa katika majumba yao kabla ya Tume kumaliza kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nichangie mengi mengi yameshasemwa lakini kuhuu suala la vitambulisho naomba na mimi nikazie, muda wa vitambulisho. Vitambulisho vya kupigia kura vinakuweko katika Tume lakini matokeo yake vinakaa muda mrefu, naomba tume iweke sheria ambayo kuwa ikifika muda vitambulisho hivyo havitolewi tena, kwa sababu vitambulisho hivi hufika pahali vikatumiwa sivyo.

Inawezekana mwenye kitambulisho hichi hata hayupo nchini kwa muda mrefu sana hata ndani ya miaka mitatu hayupo, lakini ikifika wakati anafuatwa anaambiwa na kusimamiwa mtu yule lazima kitambulisho chake kipatikane, kwa hivyo, iandaliwe sheria ambayokuwa ikifika muda kitambulisho hicho kama hajakichukua kwenye Tume iwe kinafutwa kabisa na ikiwa atakihitaji chengine basi iwekwe gharama kubwa ndipo hapo utakapoonekana umuhimu wa kitambulisho hicho cha kupigia kura.

Mwisho, nimalizie kwa kusema kwamba suala la Masheha, sheria iliyopita iliwatoa Masheha katika suala la uchaguzi, ni kweli wenzangu waliotangulia wameona suala hilo na mimi nimeona nikumbushie kwamba sasa ni wakati wa kuwarudisha Masheha katika masuala ya uchaguzi, watu hawa ndio wanaowatambua wapiga kura katika shehia hiyo, leo inakuwaje Sheha anaambiwa akae nje yeye hahusiki katika maeneo ya pale ni jambo ambalokuwa halina uhai wowote.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, katika merekebisho yake suala hili halipo hapana palipozungumzwa Sheria yote hii tunayorekebisha hamna inapozungumza masheha, naomba kitafutwe kifungu ili kiwekwe masuala ya kwamba Masheha wawe katika sehemu ya wahudumu ndani ya uchaguzi wowote utakaotokezea.
Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana, naendelea kuunga mkono hoja hii mia juu ya mia Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Moh'd Mgaza Jecha: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia masuala ya Tume ya Uchaguzi katika kipindi hiki au katika Mswada huu. Kusema kweli mimi leo ni mtu wa furaha, mara nyingi nilikuwa nikijiuliza hii serikali imekaa muda mrefu kuweza kufanikisha masuala haya katika kutekeleza sheria ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana tumekuwa tukijiuliza hizi Sheria za Baraza au Sheria za Tume zilikuwa hazipo, kama zilikuwa zipo kwa nini zilikuwa hazifati mkondo wake? Chaguzi nyingi zilizopita katika kuhakikisha masuala haya ya usalama, sheria zilikuwepo na kama zipo zilikuwa zifanyiwe kazi kwa yule anaekwenda kinyume na sheria. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri hatujui kwamba Tume wao ndio wanaozipeleka zile sheria au wanaempeleka mtu Mahakamani, hatujui kama wao au kuna kikundi maalum au kama ni serikali ndiyo inamsubiri mtu ampeleke Mahakamani au apelekwe wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mswada huu ulioletwa katika kipindi hiki, inaonekana sheria zitafuata mkondo wake. Kwa sababu kama ni Tume ya Uchaguzi marekebisho yake yaliyokuwepo hivi sasa yatategemea uchaguzi mwengine utakaofuata wa 2020. Sasa tunaomba watu wa Tume Tume ya Uchaguzi wasipate kazi kubwa sana ya kuwachagua maafisa wa Tume ya Uchaguzi. Hivi karibuni sisi tumefanya uchaguzi wa mara ya pili kwa nini hawawachukui wale vijana waliosababisha mambo yakawa muruwa katika nchi yetu. Wanawachagua watu kana huna digrii 3, huna digirii 4, hutoweza kufanyisha uchaguzi kwa ajili ya majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nataka niulize zile digirii hasa anavumbua nini pale mtu kwenye Tume ya Uchaguzi. Kwa sababu kama ingelikuwa kuna uchambuzi wa kumkata mtu mshipa, ukamtafuta nini kwa usome wake, pale vyengine. Lakini kumuandikisha tu jina lake vizuri, kitambulisho chake anacho, anakwenda kupiga kura, anamaliza anaondoka unasubiri kupiga kura, bukheri hamsa wa ishirini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaiomba serikali au Tume iangalie, uchaguzi wa mara ya pili kulitokea dharuba gani au jambo gani mpaka yakatokea matatizo, ila kulikuwa kuna mambo muruwa. Watu wamekwenda kupiga kura vizuri, wamehesabu kura vituoni vizuri, uchaguzi umetangazwa vizuri bila ya matatizo. Lakini mtakapofanya masuala ya madigirii, wale ndio wachafuzi wa uchaguzi. Mkituletea tena watu kama wale, wale ndio wanaosababisha balaa. Namba elfu moja wanaandika elfu mbili kwa kutumia elimu yao, mimi naiomba Tume iangalie chaguzi zinazokwenda kwa hali nzuri katika vipindi vilivyokwenda hatua kwa hatua ili uchaguzi utakapofuata mwengine isije ikaleta ghasia nyengine. Waangalie historia zinazofuata na chaguzi nyengine zinavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi, kwa sababu sisi wengine katika Baraza hili ni mara yangu ya kwanza kuingia katika Baraza hili. Lakini nawaombeni Mswada huu ulipokuja, umekuja katika hali muwafaka, katika

hali nzuri na hatima ya baadae ya chaguzi zinazofuata. Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tupitisheni Mswada huu, tukizingatia kama hii ndiyo roho ya nchi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, sina mengi zaidi kwa leo isipokuwa ni hayo. Ahsante.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya Mwaka 1992.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi wamenifilisi, kwa hivyo, naungana nao kwa michango yao waliyoitoa isipokuwa mimi nitachangia baadhi tu ya vipengele kwa ufupi sana. Kwanza kabisa nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea Mswada huu. Kama walivyosema wenzangu Mswada umekuja katika wakati muwafaka, kwa sababu kumalizika kwa uchaguzi mmoja ndio maandalizi ya uchaguzi unaofuata, kwa hivyo, sheria hii tutakapoipitisha itasaidia sana kuweka mazingira mazuri ya uchaguzi unaofuata wa mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nije katika kifungu cha Sura ya Pili, kifungu cha 4(d). Mimi ningeomba kifungu hiki tukiboreshe kidogo na kisomeke kama ifuatavyo: Kifungu kilivyo kwenye Mswada kinasema:

"Kufanya mapitio na kuweka mipaka ya majimbo"

Sasa naona kama haikukaa vizuri zaidi. Ningeshauri kwamba kisomeke; "kufanya mapitio ya uchunguzi wa idadi, mipaka ya majimbo ya uchaguzi" kama ilivyoelezwa kwenye kitabu hichi tulichokabidhiwa leo.

Vile vile, kwenye kifungu hicho hicho cha 4, naomba tuongeze kifungu kidogo cha (f) kwa sababu kifungu cha 4(1) kina (a) na (b) - (e), mimi ningeshauri kwamba tuongeze kifungu chengine kinachohusiana na uteuzi wa viti maalum, kwa sababu imeonekana katika sheria hii wenzetu wa viti maalum wamesahauliwa humu na hawa wanateuliwa na Tume. Katika majukumu ya kazi za Tume ilikuwa tuongeze kifungu hichi cha (f) kufanya uteuzi wa viti maalum. Ukija kwenye ukurasa wa 231, kifungu cha (20)(e) tayari tumo tunateuliwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wale wa Serikali za Mitaa. Lakini viti maalum kwa kweli wamesahauliwa, Lakini viti maalum kwa kweli wamesahauliwa kwa hivyo, ningeomba au ningeshauri tuongeze kifungu hicho cha 4(1)(f).

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika kifungu hicho hicho cha 4 ningeshauri kifungu cha 4(2) kiwe kifungu cha 4(3) na kifungu cha 4(2) ningependekeza kiingie kama ifuatavyo:

"kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu Tume itaandaa na kuweka Muundo wa Utumishi kwa watendaji wake"

Kwa hivyo, hichi kiwe ni kifungu cha 4(2) na hichi kifungu kilichokuwepo hapa kwenye Mswada cha 4(2) kiwe kifungu cha 4(3).

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika kifungu cha 19 cha Mswada wetu huu ambacho kinaanzisha Ofisi za uchaguzi wa Wilaya. Kwanza tupongeze suala hili la kuanzishwa kwa ofisi hizi. Kama utatizama sisi Ofisi yetu ya Wilaya ya Magharibi (b) ilikuwa ipo mjini na wapo kwenye kichumba kimoja tu wanabanana banana. Sasa kuanzishwa ofisi zao hizi ni jambo zuri na tunamshukuru Mhe. Rais kwa adhma yake nzuri ya kuanzisha majengo ya ofisi hizi ifikapo mwaka wa 2020.

Kwa hivyo, mimi katika kifungu hichi cha 19, vile vile, nilikuwa napenda tuweke nyongeza ya kifungu chengine hapa. Kifungu hichi cha 19 ina vifungu vidogo (1) - (3). Sasa mimi ningeshauri tuongeze kifungu cha (4) ili tuzidi kumpa nguvu huyu Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya ambaye ndiye atakaekuwa msimamizi kwa uchaguzi wa majimbo katika Wilaya yake husika pamoja na kura za maoni, lazima tumuongeze nguvu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napendelea tuongeze kifungu kidogo cha (4) ambacho kitasomeka kwamba;

"Afisa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa ndiyo msimamizi wa uchaguzi wa jimbo kutoka wilaya yake husika katika kipindi cha uchaguzi au katika kura za maoni"

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kifungu cha 29 kwenye makosa na adhabu, ningeshauri kwamba tuweke makosa ya wale ambao au vyombo vya habari ambavyo vinatangaza matokeo pamoja na mitandao ya kijamii wakati Tume ya Uchaguzi bado haijatangaza matokeo hayo. Kwenye sheria hii hatuoni vile vyombo vya habari au mitandao ya kijamii ambao wanarusha matokeo ya uchaguzi bila ya ridhaa ya Tume. Ningeomba katika sheria hii iwepo wazi adhabu ya vyombo hivi vya habari au mitandao ya kijamii itakayotoa matokeo ya uchaguzi kabla ya Tume ya Uchaguzi haijatangaza.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninashauri kwamba sheria hii ni nzuri, lakini kama haitatekelezwa itakuwa ni sheria hewa. Kwa hivyo, tunaomba uongozi wa Wizara na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuipitia sheria hii na Mhe. Rais kuweza kuweka saini yake. Tuwaombe, watendaji wote waitekeleze sheria hii bila ya kupepesa macho. Vyenginevyo, kama nilivyosema awali hii sheria itakuwa hewa na ile tija ambayo iliyokusudiwa itakuwa haiwezi kufanikiwa. Baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja kwa asilimia 100, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia machache katika Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kuchangia Mswada huu katika vipengele vifuatavyo. Kwanza niungene na waliotangulia ambao waligusia kipengele cha Masheha ambao ndio watambuzi wakuu wa wapiga kura. Katika Mswada huu katika kuchunguliwa na mimi vile vile sikuona wapi sheha yupo. Mapendekezo yangu katika Mswada huu ni lazima sheha aingizwe kwa nafasi yake kwa sababu yeye ndiye anayemtambua nani anayohaki ya kupiga kura kwa sababu yeye ndiye mwenyeji wa pale. Wale maofisa wanakuja pale wote ni wageni na watendaji wote wanaokwenda pale ni wageni, lakini mwenyeji wa pale atakuwa ni sheha, kwa hivyo, sheha katika Mswada huu naomba atambuliwe rasmin.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika kifungu cha 5 kinasema;

"Uwezo wa Tume kusimamia mikutano ya kampeni".

Katika kifungu hichi imeelezwa kuwa;

"Miongoni mwa kazi za Tume kwa mujibu wa Katiba na sheria zinazohusiana na uchaguzi kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake itakuwa na uwezo wa kusimamia kampeni za uchaguzi".

Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi nilikuwa nina mapendekezo yafuatayo. Katika kipindi hichi tulichokwenda nacho tumeshuhudia mikutano mingi ya kampeni ikifanyika, lakini katika mazingira yale katika kampeni wanakwenda watu wenye mazingira tofauti na hali tofauti. Lakini mazingira yale yalikuwa hayamshirikishi mtu mwenye ulemavu vizuri, kwa hivyo, hata kama mtu mwenye ulemavu anataka kwenye kushiriki katika kampeni anakuwa na jitimai au anauzito fulani, anataka lakini kutokana na mazingira hayamuwezeshi kushiriki.

Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba Tume kupanga mipango madhubuti au kuweka vipengele maalum ambavyo vitamlinda mtu mwenye ulemavu ili aweze kushiriki katika kampeni kama wengine kwa sababu na yeye ni haki yake, hawezi kupiga kura kama hajamjua mgombea na kama hajenda kwenye kampeni hawezi kusikia zile sera za wagombea, kwa hiyo, kutokushiriki kwake kunakuwa kama kumemfungia haki fulani kuzikosa, kwa hivyo, anakwenda kuchagua pengine kwa shindikizo tu la mtu kwamba mchague fulani. Lakini kama atashiriki mwenyewe atakuwa na uwezo mzuri au atakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kuchagua nani mwenyewe anaemtaka.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika "makosa na adhabu". Suala la mtu kujitangaza ni kosa la jinai, tena ni kosa kubwa. Kwa hivyo, pamoja na adhabu ambazo zimewekwa katika sheria hii, mimi nilikuwa nina pendekezo jengine pamoja na adhabu zilizopo lakini vile vile azuiliwe mtu huyu kugombea kwa vipindi vitatu mfululizo katika nafasi zote za uongozi asigombe.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 21 kuhusu "Watumishi wengine" Tume katika kifungu hichi inaweza kuwaajiri watumishe wengine. Mapendekezo yangu katika kifungu hichi wanapofanya huu uwajiri kwanza wazingatie jinsia. Mara nyingi katika uwajiri unapotokezea hasa katika sekta kama hizi unakuja kujikuta wanaume wapo wengi, wanawake wapo kidogo au hakuna kabisa. Kwa hivyo, katika Mswada huu kungeelezwa wazi kwamba mbali na kifungu hichi vile vile kungeelezwa wazi kwamba ushiriki au uajiri utakuwaje kuzingatia usawa wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, changine hapo hapo mbali ya usawa wa kijinsia, pia izingatie uwajiri wa watu wenye ulemavu. Hivi sasa watu wengi wenye ulemavu wanapoomba nafasi kama hizi mara nyingi wanakuwa hawapati. Kwa hili ningeiomba tume ikazingatia uwajiri wa watu wenye ulemavu kulingana na uwezo wao na wasiangalie hali zao waangalia uwezo wao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze Tume katika chaguzi zilizopita ilijitahidi sana kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki katika kupiga kura kwa kuwatengenezea wale ambao wanahitaji vifaa maalum, lakini vile vile kuwarekebishia mazingira, walijitahidi sana. Lakini katika vile vifaa maalum ambavyo vilivyokuwa vinatumiwa na wenye ulemavu wa uoni. Vifaa vile vina mapungufu kusema la kweli, vilikuwa hakuna katika vituo vyote. Sasa ningeiomba Tume ikajipanga vizuri ikahakikisha vifaa vile vinapatikana vya kutosha ili kuwawezesha watu wenye ulemavu watumie nafasi ya kupiga kura kwa kumchagua mtu ambaye wanamtaka wenyewe na kuepusha kuchaguliwa mtu ambaye anamtaka yule ambaye anamchagua.

Aidha Mhe. Mwenyekiti, niiombe Tume wanapochapisha machapisho yoyote yanayohusiana na Tume basi wahakikishe wanazingatia wale ambao wana uoni hafifu kwa sababu mwenye uoni hafifu ana maandishi yake maalum ambayo anaweza kuyasoma. Sasa niombe Tume kufanya ili kuwawezesha wenye uoni hafifu na wao waweze kusoma na kufaidika na yale ambayo yanatolewa na kuepuka kupata yale maagizo ambayo hayako sahihi, watapoweza kujisomea wenyewe watapata maelezo yaliyokuwa sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo naomba niunge mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika wakati huu nikiwa mzima kabisa. Lakini la pili nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuleta huu mswada wa marekebisho ya Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja nitakwenda kwenye ukurasa wa 227 kuhusu Uwezo wa Tume katika kupanga mikutano ya hadhara. Mhe. Mwenyekiti, mwaka 1995 kulipangwa mikutano miwili ya hadhara ya mwisho mmoja ulifanyika Kibandamaiti na mmoja tulifanya maeneo ya Mtopepo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mkutano ule baada ya kumalizika vyama viwili vilikutana katikati na watu wengi sana waliathirika kwa kupigwa mawe na wengine wakavunjiwa magari yao na wengine waliwahi hata kuchomewa nyumba zao moto.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kupanga mikutano hii ya hadhara ya kampeni wajiandae vizuri ili usalama wa wananchi wanaokwenda kusikiliza hii mikutano ya hadhara ya kuwajua wagombea wao wasiwe na hofu kama alivyosema Mhe. Mwantatu, wengine hali zao zinakuwa haziko vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 228 kuhusu Uwezo wa Tume kuhusu suala zima la Majengo. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kidogo sisi Wilaya yetu ya Magharibi tunatumia Ofisi ya Shule ya Mwanakwerekwe “C” lakini bahati nzuri na wewe mwenyewe ni mwalimu Mhe. Mwenyekiti, tukienda kule tunapata tabu sana, tunapigana vikumbo na wanafunzi na wakati mwengine wanafunzi wako madarasani inakuwa mtihani mkubwa.

Kwa hivyo, niipongeze Serikali kwa uamuzi wake huu wa kujenga Ofisi kila Wilaya lakini naomba sana katika Ofisi hizi za Wilaya kuwe na Ofisi ambazo

zitakuwa za majumuisho za kila jimbo. Kwa sababu sasa hivi kumekuwa na utaratibu, Ofisi zetu za Tume za Uchaguzi zinakuwa siri sana kujua Ofisi ya Majumuisho ya kila jimbo. Kwa hivyo, niombe sana na majimboni kuwe na Ofisi za majumuisho ambazo kila mgombea atajua nikitoka kwenye shehia hii eneo la majumuisho litakuwa eneo fulani.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 230 kuhusu Kazi za Mkurugenzi, hawa Wakurugenzi au Makamishna huwa wanateuliwa na Mhe. Rais na wanapewa heshima kubwa sana. Lakini la kusikitisha Makamishna hawa huwa wanafikia pahali wanapigana magumi na sisi wananchi tunasikiliza. Kwa hivyo, niombe sana Mhe. Rais wakati wa uteuzi aangalie nani anaweza akamuweka pahali ambapo panapostahiki na atamuwekea heshima yeye Mhe. Rais kwa kumteua kuwa kwenye nafasi ile.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mawakala wenzangu wamelizungumza sana, ni mtihani mkubwa ambao ulijitokeza wakati wa uchaguzi, imefika wakati mawakala wa vyama vyengine wameshaingia ndani lakini mawakala wa vyama vyengine kadi zao za uwakala hazionekani. Mhe. Mwenyekiti, ni kitu cha kusikitisha na wasimamizi wale hatukusikia hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali. Kwa hivyo, niombe sana suala la mawakala likiingizwa kwenye wasimamizi wa Wilaya, wahakikishe vitambulisho vya mawakala vinapatikana mapema.

Mhe. Mwenyekiti, nije na hili kubwa ambalo wenzangu wote waliosimama hapa wamelizungumzia suala la mgombea kujitangaza kabla ya Tume ya Uchaguzi. Suala hili ni suala gumu sana kwa sababu katika nchi hii kuna vijana, wazee na watoto, unapoamua kujitangaza wewe ina maana unahatarisha amani ya nchi nzima. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, na Serikali kwenye hii hatukusikia kauli iliyotoa, kwa hivyo, tuombe sana amani ya nchi hii isichezewe wakati wa uchaguzi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano chini ya Mwenyekiti au Rais wa Jamhuri ya Muungano Mzee Magufuli yeye anasema hataki suala la amani kuvurugwa.

Lakini hapa Zanzibar tunahisi suala la amani wakati wa uchaguzi linachezewa chezewa, unapojitangaza kuwa wewe ni kiongozi fulani katika nchi wakati Tume haijatangaza unahatarisha kwa sababu huko kuna watu walipata *pressure*, wengine walikufa, kuna watu walilazwa hospitali kwa mtihani huu ambao umejitokeza. Naomba sana wakati wa marekebisho wa sheria hii pawekwe sheria ngumu ambayo itaweza kumdhibiti anayejitangaza kabla ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la masheha. Masheha wanamwakilisha Mhe. Rais kila shehia, kwa sababu Mhe. Rais yeye hawezi kwenda kila eneo. Kwa hivyo, kuna Mkuu wa Mkoa, kuna Mkuu wa Wilaya lakini mwisho kuna Sheha. Katika Taasisi zote za Serikali mtumishi wanayemtegemea ni Sheha kwenye Shehia, lakini tunashangaa kwenye suala zima la uchaguzi Sheha kaondolewa kwa sababu ipi ya msingi. Niombe sana Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu utakaporekebishwa lazima Sheha awepo kwa sababu yeye ndie msimamizi kwenye Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niseme tu kuwa ninaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, Mwenyezi Mungu ajaalie ufanikiwe na tuupitishe sote kwa pamoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naona kiti chako kimepitikiwa kidogo Mhe. Mwenyekiti, ulinitaja mimi kabla ya Mhe. Waziri Castico na mimi nipo. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru hakuna mkamilifu isipokuwa ni mmoja tu *Allah Subhana Wataala* na kuteleza si kuanguka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa hata nisichangie hoja hii leo, wengi wamechangia. Sawa sawa na kupika pilau yako nzuri ikaja ikaanguka tojo ya mafuta ya taa tu, pilau ile haiwezi kulika tena. Tunashukuru wote waliochangia, lakini tokea asubuhi kukaa hapa na nilikuwa nikajilaumu Mhe. Mohammed Aboud, katoka lakini ninashukuru karudi. Tokea walivyoanza kuchangia wachangiaji asubuhi mpaka muda huu sijasikia maslahi ya wafanyakazi wetu wa Tume hii ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena nilikuwa nisichangie kwa wenzangu walivyochangia vizuri, wenzangu wametaja masuala ya masheha kitu muhimu, lakini maslahi hawa vijana wetu huko juu yakoje. Wanafanya kazi nzito katika mazingara wanayofanyia kazi, tusiwe tunaandika hati za kiarabu ukawa unavutia kwako, yaani kiarabu ukiandika unavutia huku. Mazingira mazito wanaofanyia kazi Mhe. Mohammed Aboud, hawa watu. Mfano mvua, jua, usiku na mchana, tumewafikiriaje?

Narudia tena mara ya tatu nilikuwa nisichangie lakini baada kuona vijana wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi lazima tuwafikirie binaadamu. Mcheza kwao hutunzwa, kwa usikivu wako na ninavyokuamini Mhe. Mohammed Aboud katika majumuisho, ninaamini kwa umakini wako na huruma uliokuwa nazo hili hutoliacha na vyenginevyo utakapoliacha, nimekuja na *sandals* hii lakini itabidi nitafute buti kwa kuwatetea hawa. Kwa hivyo, jipange Mhe. Mohammed Aboud, kwa umakini wako ninajua hutowaacha

vijana hawa, ulikuwa ukitetea mawaziri humu ndani kwa hoja, ukashindwe wafanyakazi wako hawa, hawa ndio wanaokuongoza wewe ukang'ara humu ndani. Mkuu wa Kituo hang'ari bila kuwa na askari wadogo. Kamanda anang'ara kutokana na watendaji wake, sasa kama hukuwafikiria utakuja kuharibikiwa Mhe. Mohammed Aboud, Waziri makini. Hawa wanataka kufikiriwa wakati mgumu huu na wengine humu walikuwa wanafanya kazi za matofali, mchanga wenyewe haupatikani Mhe. Mohammed Aboud hivi sasa, mchanga Waziri kaufunga, maisha yazidi kupanda kuwa magumu. Hata akaanza kusema kuja kusema kwako Mhe. Waziri mwenye dhamana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, naomba uzungumze na kiti na halafu suala la mchanga sasa hivi sio nafasi yake,tunachangia Mswada wa Marekebisho ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini kutoa mfano si vibaya ukali wa maisha yalivyo, mimi sikusema hoja ya mchanga, nasema maisha kutokanana kazi kuna wengine humu ni vibarua na mchanga wenyewe haupatikani. Kwa hivyo, wanachodai ni maslahi, maslahi mazito.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, nimekuelewa, naomba ukae. Mhe. Jaku, suala tunalozungumza hapa ni Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi, lakini ulikuwa kama una mchango ambao unahisi utaleta maslahi kwa wafanyakazi wa Tume ni vizuri ulikuwa uzungumzie hicho. Ukienda kinyume na hilo itabidi nikuweke kitako nimpishe mchangiaji mwengine achangie mswada huu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mwanzo nimezungumza suala hili na nilichozungumza Mhe. Mwenyekiti, ni Kiswahili wala si lugha nyengine maslahi ya wafanyakazi wetu, ni magumu ndio nikaja mfano huu Mhe. Mwenyekiti, lakini tuache huko tusifike sitaki kushindana na kiti chako. Maslahi ya wafanyakazi wetu ni magumu na kazi wanazofanya ni hatarishi.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba umalizie Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naona nisije nikenda kinyume bora nikae kitako tu niachie uamuzi wa kiti chako, maana yake utafika pahali kushindana bure haina haja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba baada ya michango ya wenzangu wote waliochangia, ukichangia baada ya watu wengi

unakuwa huna hoja nyengine ya kusema kwa sababu mengi yanajirudia ni yale yale na bahati nzuri basi kwamba sasa hivi Baraza kiwango cha uchangiaji kimekuwa kikubwa na ufahamu ni mzuri sana. Tangu asubuhi tunarudia *points* ni zile zile na tunafanya vizuri kwa sababu tunasisitiza. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, la kuchangia kubwa sana sasa hivi sina la kusema zaidi, niseme tu kwanza pia nichukuwe nafasi kushukuru kwa hawa walioandaa gazeti hili.

Kwa sababu gazeti hili limeletwa wakati muafaka na wakati wenyewe muafaka kwa sababu baada ya kupata *experience* ya chaguzi zilivyojitokeza na masuala baadhi ambayo yamejitokeza yakaonekana yana matatizo, kuletwa kwa hoja hii sasa hivi ni wakati wake mzuri kwa sababu tumeweza kujifunza na ku-*experience* kitu ambacho ni hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, humu mna mambo mengi sana ya kuongea ambayo yameshaongelewa na wenzangu, mwanzoni kabla ningewahi nilikuwa nazungumza suala zima la kusema kwamba watoto wanaokwenda kufanya kazi kwenye Tume lazima wawe na *degree*, mara nyengine inaonekana kabisa kwamba, sidhani kila mmoja anaekwenda kufanyakazi kule lazima awe na kitu hicho. Kwa sababu hata ukimuangalia hata Sheha mwenyewe tunayemchagua mara nyengine elimu yake sio lazima awe na *degree*, lakini ufanyaji wa kazi anaoufanya anafanya kazi kwa uhakika na uaminifu na anakuwa anaongoza hasa anafahamu hasa eneo analokuwepo.

Jengine ambalo ninaliona ni pamoja na kuona kwamba labda katika suala la Tume, suala la nafasi kwenye nafasi za juu na wanawake pia wafikiriwe sana kwa sababu wanawake hawana migogoro na tunakuwa na hisia kwamba nikikosea hili jambo natikisa watu na wengi watakaoumia ni wanawake na watoto. Sasa inapotokezea hata katika mitafaruku mengine isiyokuwa na maana wanawake ndio wanao-*balance* ambao wana *sacrify* kusema kwamba sisi tubakie katika mazingira haya kwa sababu najua *repercussion* ya nchi yetu itakuwa katika utaratibu mgumu.

Lakini pia kuna suala zima la kusema kwamba wale watakaokuwa wamesoma chuo, vyuo vinavyojulika viwe na sifa ipi basi, vyuo vinavyojulikana *certificates* zao wamepata katika chuo kadhaa na kadhaa basi viwe vinajulikana ni vyuo gani ili waweze kupata muafaka wa kuona kwamba watafanyaje.

Jambo jengine ningerudi tena kwa Sheha, Sheha ni mtu muhimu sana kwenye eneo lake, anafanya kazi vizuri sana na anawatambua watu wengi. Lakini anapokuja kuwa na mitikisiko kidogo inawezekana asiweze kuwakilisha vizuri, kwa hivyo, kuwe na vitu ambavyo vinaweza vikamsaidia kum-*counter check*

atakapokuwa anafanya vitu ambavyo vinakwenda labda kinyume au anatishiwa mazingira au anapewa *pressure* kubwa isiyokuwa na msingi, kwa hivyo, ni vitu ambavyo vya kuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia pia katika masuala haya tunayozungumza tangu asubuhi hapa ni kwamba Tume ya Uchaguzi ndio muhimili wa nchi tunapokuwa kwenye masuala ya uchaguzi. Kama wenzangu walivyosisitiza kwamba mtu anapotokezea kujitangaza kabla ya uchaguzi ni wakati wa hatari anafadhaisha watu wote na unapojitangaza kabla ya hatua, hiyo peke yake ni kwenda kinyume na kutangaza kama kupindua Serikali au kufanya kitu gani.

Kwa hivyo, suala hili lisichukuliwe mzaha. Anapotokezea kwamba amesikika na watu ushahidi wa kwamba kasikika kwa nani, amekwenda kwenye vyombo vya habari, amezungumza, amekutana na watu na ameendelea kujirudia na kujirudia dunia nzima, mtu anaendelea kushikilia *point* ile ile, inakuwa inafadhaisha nchi inakuwa na tatizo kidogo. Sasa na watu kama hawa wanafanya vitu vya namna hii inakuwa ni kosa sio la kwanza, la pili, wenzangu wengine wamezungumza kwamba mtu wa namna hiyo angeweza kuchukuliwa hatua hata miaka 20, wengine naona wamezidisha hata miaka 20, 30. Lakini nadhani ipo haja ya kupima na kuangalia vizuri watu wanaokwenda kugombea, anapokuwa anagombea anakuwa na mtizamo gani wa nchi yake, anaangalia vipi inakuwa mara nyengine unafika pahala unafadhaika, je, hawa viongozi wanaong'ang'ania hapa lengo lao wakishapata wanataka kutupeleka wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba katika masuala kama haya yasifanyiwe kusema kwamba labda ushahidi uwe kwamba lazima atokezee mtu maalum ya kwenda kusema vile. Lakini hata wananchi wapate nafasi ya kuona jamani mbona tumeambiwa hili na hili na hili, tunaonaje wawe na kitu cha kuzungumza na kujieleza.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nisingependa kurudia mengi napenda kuunga mkono kabisa asilimia mia moja kwa hii hoja kwamba imekuja wakati muafaka na tunaamini kabisa yote ambayo tumeyachangia hapa yataleta sura mpya. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme kwamba napenda nichukue fursa hii kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kujaalia leo mswada huu ukaletwa hapa mbele yetu katika kuujadili na badala yake kuweza kufanya marekebisho, pale ambapo tunahisi kwamba panahitaji marekebisho au ushauri ama mapendekezo. Lakini ukweli

ni kwamba mswada huu ni muhimu sana na ni nyeti sana na jinsi ambavyo unachangiwa kwa kila mmoja wetu anayesimama unahisi kwamba mambo yameshamalizika. Lakini ukweli ni kwamba bado mambo yapo mengi ambayo yanahitaji bado yaendelee kutiliwa mkazo kwa yale ambayo yanahitaji kusisitizwa zaidi.

Mimi kabla sijaendelea, naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na ni ya kuthaminiwa sana na umekuja wakati muafaka sana. Vile vile, naomba nichukue fursa hii kwamba haitokuwa vyema tukajadili mswada huu mpaka tukamalizia kushindwa kukumbuka watendaji wa Tume ya Uchaguzi, hususan Mwenyekiti wake kwa kazi nzuri ambayo aliifanya, itakuwa hatutotenda haki kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba moja kwa moja mimi nizungumze kwa ujumla wake na sitokwenda kipengele kwa kipengele. Lakini kimoja ambacho ninataka kuchangia ni kuhusu muongozo wa maadili ya vyama vya siasa kwa uchaguzi mkuu pale ambapo uchaguzi umefika. Ni dhahiri kwamba tumejifunza mengi na ni lazima kila mmoja wetu akumbuke ambayo yaliyotokea, ni ukweli usiofichika na hatuwezi kuyafumbia macho au tukiendelea kunyamaza kimnya kwa yale ambayo yametokea na tusiweze kuyazungumza ili yasije yakatokea tena.

Kwanza kabla sijaendelea kulisema hilo ningeomba sheria na makemeo mbali mbali ya serikali tumeweza kuyaona ambayo yameweza kuchukuliwa pale ambapo kwa kweli hapakufanywa vizuri, au sheria ilikiukwa. Lakini pamoja na hayo bado inaonekana mambo haya yanakuwa yakijirejea rejea kila uchaguzi, na haya yanasababishwa na mambo mengi. Moja, kuna baadhi ya watendaji Mhe. Mwenyekiti, sio waaminifu ambao kwa njia moja ama nyengine wanapelekea athari ambazo zinajitokeza wakati wa uchaguzi. Ni vyema sasa pale ambapo kwa kweli Tume kutakuwa na utendaji na hizo kamati nyengine ambazo zitaundwa basi tukiweka hawa watendaji au wakichaguliwa watendaji ni vyema izingatiwe sana na watu wenye taaluma mbali mbali ambao wanaweza kubaini matukio au athari zitakazopelekea kuharibu uchaguzi kabla uchaguzi haujaharibiwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika maadili hayo tungeangalia sheria kabla ya uchaguzi haujafanyika au uchaguzi ikiwa unaendelea basi taratibu zinaendelea kufanyika. Kwa mfano, katika masuala ya kampeni kuhusu suala zima la magari lazima tutunge hizi sheria zipo lakini bado ni jambo ambalo hatujalizingatia kwa kina. Sasa hivi tufike wakati Zanzibar tukomae kuijua

siasa au kuujua uchaguzi na athari zake na mafanikio yake, isiwe kila tunaporudi kwenye uchaguzi tunapata maafa makubwa ambayo kumbe tunaweza kuyaepuka. Kwa mfano, watu wanajazana magari kwa wingi kupita kiasi, gari ambazo hazifai na hatimae ukiangalia sheria zipo na zimetungwa lakini bado huoni kama kuna hatua ambayo inachukuliwa kwa kuidhibiti hali hiyo, na badala yake vurumai zinatokea na mwisho ukimalizika pengine mkutano wa kampeni unakuta tumeshapata maafa yaliyotokana na hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, matumizi ya lugha katika kipindi hiki kunakuwa na lugha nyingi ambazo sio lugha ambazo zinahusu masuala ya uchaguzi. Kwa hiyo, ifike wakati sasa tuone kwamba hizi sheria ambazo tunazo basi ziwe zinafanyakazi kuona kila mmoja anajua umuhimu wa sheria ambayo ipo, na ifanye kazi bila ya kuoneana aibu, kwa sababu kumekuwa kuna lugha za ajabu ajabu mtu anachafuliwa jina na hakuna chombo ambacho kinajitokeza wazi wazi kuona inachukua hatua ili jambo lile lisiendelee kuleta maafa kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine tumeshuhudia baadhi ya wakati matumizi hata ya viwanja vya mikutano ya kampeni napo shida ipo. Mhe. Mwenyekiti, unakuta pengine chama fulani kinajua siku fulani hapa ataingia mgombea fulani basi pengine sehemu ile hana mvuto mkubwa, au ana mvuto wa kiasi lakini hatimae unakuta kuna mambo ambayo yanafanyika ndani ya maeneo yale kama kupachika mabango ambayo ya mtu mwengine na wakati eneo lile linaenda kutumiwa na chama fulani. Hali hii pia nayo ni vyema sheria tulizozitunga basi ziendelee kufanya kazi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia, niende kama nilivyosema kwa ujumla wake tunapoziandaa hizi sheria au mswada huu umekuja kwa lengo la kufanya maboresho ili tuone kwamba tunapitisha kitu ambacho hakitakuja kutuletea madhara zaidi kwa mara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sasa katika uteuzi kwa mfano, kuna wateuzi Afisa Mdhamini kwa upande wa Pemba ambaye ana jukumu kubwa la kusimamia uchaguzi kwa upande wa Pemba. Ukiangalia kule kuna Maafisa Wadhamini katika wizara nyengine lakini yeye nguvu yake na thamani yake kimaslahi bado haiko vizuri, lakini inavyoonekana pia kama niko sawa mtendaji huyu hakuteuliwa na Rais anateuliwa na Tume. Nadhani hapa ifike wakati sasa tuweke kipengele ambacho kama niko sawa kwamba mtendaji huyu nae kwa umuhimu wa pekee na jiografia ya maeneo yetu, basi ni vyema na yeye huyu awe kwenye uteuzi wa Mhe. Rais hili litamsaidia na kuweka maslahi na mambo mengine ambayo yatampa uwezo zaidi na kuonesha

kwamba atakuwa na nguvu zaidi katika kufanya kazi upande wa pili wa Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika sheria hii kwa vile tunataka kuweka mazingira ya kuwa na ofisi inayohusiana na masuala ya uchaguzi ambayo inajitegemea, ni vyema pia tujitegemee mpaka na majengo. Kwa sasa hivi Tume ya Uchaguzi kuanzia Makao Makuu mpaka Wilayani inavyoonekana majengo ni ya kuazima na hakuna jengo ambalo wanalimiki wao kama taasisi. Sasa hili nalo linaweza likatupelekea kuwa na ufanisi uliotukuka, kumuweka mtu katika eneo ambalo ameazima hatujui ni nani pengine amemuazima hilo eneo, hatujui ana mtizamo gani, ana hisia gani, ana utashi gani. Anaweza pia ikawa ni chanzo cha kukosa ufanisi katika masuala mazima ya uendeshaji uchaguzi ambao uliohuru na wa haki zaidi. Mhe. Mwenyekiti, naomba hili tuliangalie kwa undani zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu watendaji kwa mfano kama nafasi za Wilaya. Katika ngazi ya Wilaya kwa sasa hivi tunashukuru tumepata kusikia matangazo kuna waratibu ambao wataajiriwa hivi karibuni muda sio mrefu. Lakini pale pia ningeomba tungeangalia makarani katika ofisi zile na sheria pia ioneshe upatikanaji wa makarani. Makarani wale kwa sababu mtu akiitwa mratibu unafika wakati hata kumwambia kufanya usafi katika ofisi au kuweka mambo mengine sawa ndani ya ofisi inakuwa ni mtu ambaye kidogo hatuwezi kumtumia katika mambo mengine kama haya.

Kwa hiyo, naomba pia na makarani tuangalie katika ofisi hizi za Wilaya inaweza ikatusaidia sana kuwe na vijana ambao wameshatumikia tumewaona wana uzoefu, ni waadilifu basi ni vyema tuwazingatie hawa vijana tuweze kuwapa fursa waweze kuendelea kuitumikia Tume ya Uchaguzi kwa ufanisi zaidi na iweze kujitegemea zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi nirejee tena kusema kwamba tufanye kama ambavyo tutafanya lakini vyovyote vile naomba maslahi ya watendaji wa Tume ya Uchaguzi kuazia makao makuu mpaka ngazi ya Wilaya tuyazingatie kwa umuhimu wa pekee, hawa wenzetu wanafanya kazi ngumu, kazi za shida, inafika wakati mtaani wanaonekana kama ni kituko. Sasa tuweke mazingira ambayo yatawafanya na wao jiografia ya kazi yao ni ngumu basi wapewe na umuhimu wa pekee.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kwa umuhimu wa pekee nirejee tena kwamba sasa tufike wakati tutengeneze mazingira kwa wale Wenyeviti ambao wameshafikia ukomo kwa mfano kama Mhe. Jecha muda wake umefika

pengine katika kipindi kile ambacho kwa kweli hatakuja kuondoka pengine kwa muda wake umeisha. Kuwe na fungu maalum au kuwe na bahashishi maalum itakayomfanya kwamba yeye akumbuke kazi kubwa aliyoifanya ambayo itamfanya yeye aweze kufurahia shughuli nzito ambayo ameifanya. Kwa mfano, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi mtendaji Mkuu wa Mkoa kwa kazi nzuri aliyoifanya yeye watendaji wenzako waliweza kumzawadia kuchangishana wakapata gari wakamsaidia.

Sasa, je, huyu mtu ambaye kwa kweli amefanya kazi kubwa na wenzake pia walifanya kazi kubwa awamu kwa awamu, kunyamaza kimya tusiweze kuangalia katika mazingira haya ni kwamba kidogo hatufanyi motisha na kuwatia watu wengine mori waweze kuwa na utayari wa kufanya kazi kama hiyo. Kwa hiyo, kwa vile tunaelekea katika kujitegemea zaidi na uhuru zaidi basi ni vyema pale wanapomaliza muda wao kuwe na fungu maalum sheria itamke iweze kuwapa angalau bahashishi au sijui tutatumia lugha gani ili na wao wajisikie katika utumishi wao uliotukuka wenye nidhamu na uzalendo wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa vile watu wameshachangia mazuri naomba nisiharibu zaidi niseme kwamba, naunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu na wenzangu naomba tuunge mkono zaidi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia mswada huu wa sheria ambao nimeutizama kwa makini jina lake Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Ukitizama mswada wenyewe jina lake unahusisha kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi, kwa hivyo, ukitizama moja kwa moja utaona zaidi tunazungumzia masuala yanayohusiana na wafanyakazi wa Tume, Mwenyekiti, Makamishna na Sekreterieti yake yote. Kwa maana hiyo kimsingi tulitakiwa tuzungumze katika maeneo haya, lakini huwezi kuzungumza ofisi bila ya kuhusisha mambo mengine ya uchaguzi na ndio maana wawakilishi wenzangu wanachangia lakini wanaelewa wapi pakuchangia lakini huwezi kutenganisha mambo haya. Baada ya kutoa ufafanuzi huo na mimi pia nianze kuchangia na mimi hatimae pia nitafanya hivyo hivyo, kwa sababu watu wote wamezungumzia mambo haya katika mazungumzo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nizungumzie suala hili la ofisi hii na nitaanza kwa maelezo haya. Ikiongoka Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ndio kuongoka kwa uchaguzi wenyewe, ikipotoka au ikipotoshwa ofisi, ndio kupotoshwa na kupotoka uchaguzi wenyewe. Nimeanza hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kuelewa

kwamba Ofisi ya Tume ya Uchaguzi inapaswa kuundwa na watu makini, wenye uwezo, wenye busara na wenye uzalendo. Kwa maana hiyo, wakati wa kuundwa ofisi hii mambo hayo ni muhimu sana kuzingatiwa. Wakati nikiangalia kifungu cha 4 kinachoelezea habari ya majukumu ya Tume katika kifungu kidogo (b), kimesema moja katika majukumu yake hii ofisi ni kusimamia, kukuza na kuratibu elimu ya wapiga kura, na ndio maana hapa wakati mwengine tukashindwa kutofautisha Ofisi ya Tume na wapiga kura. Kimsingi wapiga hawamo katika utumishi wa ofisi lakini hatuwezi kutenganisha. Sasa nisisitize katika jukumu hili ambalo limeelezwa vizuri katika kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikiangalia kifungu kingine cha 16 kinachoelezea kuhusu kazi za Mkurugenzi wa Tume nilitamani sana kazi hii ya kutoa elimu ya wapiga kura iandikwe bayana kuliko kusemwa kwa jumla tu na kazi nyengine atakayopewa. Hii nadhani ni kazi muhimu sana, sana, sana na umuhimu wake unatokana na ukweli kwamba wapiga kura ndio kiini cha uchaguzi, hakuna wapiga kura basi hakuna uchaguzi. Lakini pia nasisitiza kwamba wapiga kura ambao watakuwa wameelimika au wamepata elimu ya wapiga kura, kwa kweli hao ndio wapiga kura tunaowatarajia na tunaowataka.

Kwa hiyo, nishauri hapa ni vyema katika kuifanya kazi hii, ofisi ianzishe sijui niite kitengo au idara au kamisheni ambayo itakuwa na kazi ya kushughulikia huu utoaji wa elimu ya kupiga kura. Katika baadhi ya nchi elimu hii ya wapiga kura na nyenginezo unakuta kuna taasisi maalum wengine wanaita *Civic Education Commission* na mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu elimu ya wapiga kura ili ifanikiwe lazima ihusishe na elimu ya uraia, sasa ile elimu ya uraia ndio inayo-*facilitate* elimu ya wapiga kura. Kwa lugha rahisi elimu ya uraia ndio msingi na hii elimu ya wapiga kura inafuatia baadae. Sasa kuna uhusiano kidogo ya uraia, yaani mwananchi ambaye amefahamu haki zake, mwananchi ambaye amefahamu wajibu wake, mwananchi ambaye anajua fursa zake huyu ni rahisi kupata hii elimu ya wapiga kura. Lakini mwananchi ambaye haya yote ameyakosa halafu unangojea siku ya uchaguzi umpe elimu hii ya wapiga kura, kwa kweli hatuwezi kufanikiwa. Kwa hivyo, ningeshauri kwamba wakati serikali bado haijaanzisha kitu hiki au taasisi hii ya *Civic Education Commission* ni vyema sekreterieti ya Tume ya Uchaguzi wakafanya kazi zaidi ya kutoa elimu ya wapiga kura, kutoa elimu ya uraia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanya kazi hiyo ni vyema wakashirikiana na taasisi nyengine, Taasisi za Elimu na taasisi nyengine ambazo zinafanya kazi ya

namna hii. Pia, tuelewe kwamba suala la kutoa elimu ya uraia ni suala la mchakato wa kidemokrasia, na mchakato wa kidemokrasia una mila, desturi na utamaduni wake, kwa hivyo, inajengwa hatua kwa hatua. Kwa hivyo, wakati wa kufanya kazi zao waelewe kwamba ni zoezi endelevu, ni zoezi la kila siku na zaidi tunategemea vizazi vijavyo na hiyo ndio falsafa ya elimu, yule anayeambiwa leo sio aghlabu kuweza kubadilika leo leo, lakini hatua kwa hatua baadae anaweza akabadilika, hayo ni mambo ya kuzingatia sana, sana. Kwa hivyo, si vibaya zile mada zinazohusiana na elimu ya uraia zikaingizwa katika muhtasari katika masomo ya uraia katika skuli zetu za msingi na sekondari, nikasema pale kuna haja ya kushirikiana na taasisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, huyu mpiga kura ambaye ni muhimu sana katika masuala haya, huyu anapaswa kuelimishwa katika hatua zote zinazohusiana na masuala ya uchaguzi. Anahitaji kuelimishwa katika suala la uandikishaji, suala la kuimarisha na kukua na kuhakiki daftari la wapiga kura apate elimu hiyo, anahusishwa pia katika *process* nyengine ya kampeni afahamu inapofika wakati wa uchaguzi ana haki gani, hatua nyengine ya tatu aeleweshe namna ya kupiga kura na hatua nyengine zote zinazofuata na ndio tukasema hili ni eneo endelevu na hapa kwa maoni yangu ndio penye kazi ya msingi kabisa ya hii Afisi ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia suala hili linakwenda pamoja na suala ambalo tunaita siri, faragha na usalama kwa watendaji wa tume. Kipengele hiki nilitamani kiwemo katika vifungu, lakini kama kimekosa nafasi basi ni vyema kikawemo katika kanuni au miongozo inayofuatana. Wafanyakazi hawa na wengine wote kwa kweli wanafanya kazi *very sensitive*, kazi ambazo zinahitaji usiri mkubwa, faragha kubwa lakini pia zinahitaji usalama.

Kwa hivyo, jambo hili lizingatiwe kama si katika vifungu vya sheria basi japo katika kanuni, ni jambo muhimu sana, lazima kuwe na aina fulani ya *guarantee* katika kuifanya kazi hii. Lakini hii haiwezi kufanikiwa peke yake, ndio pale nikasema hatuwezi kuzungumza ofisi bila ya upande mwengine, haiwezi kufanikiwa kazi hii kama nako pia wapiga kura hawana siri, faragha na usalama wao.

Wenzangu waliizungumzia kwa mbali kama waliificha ficha kidogo, mimi nataka niiweke wazi, kwamba kama hakuna usalama wa mpiga kura atahofia kutumia fursa yake ya kupiga kura, kama hana faragha pengine analazimishwa kama walivyozungumza baadhi ya wenzangu; kama fanya hivi, lete kadi yako ya kupigia kura akupigie fulani kwa kulazimishwa hapa tutakuwa kwa kweli ule uhuru na faragha na usalama wa mpiga kura utakuwa haupo. Sidhani kama

ni kazi ya ofisi lakini ni jambo ambalo la kufikiriwa kuwa lazima kuwe na utaratibu ambao utamuwezesha mpiga kura kuwa salama, huru na faragha katika kufanya kazi zake. Hili litatusaidia sana katika kujenga demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningependa kumalizia ni suala la lugha. Mara nyingi imeandikwa afisi, afisi, lakini Kiswahili kilichozoweleka ambacho pia nacho ni *standard* ni ofisi na ndio maana tunazo nyingi tu, Ofisi ya Rais. Ni sawa, lakini twende kwa mlingano.

Baraza la Kiswahili la Tanzania na Zanzibar wanatambua zote mbili tunaweza kutumia, lakini kwa kuwa kukiwa na mlingano ni bora zaidi, kwa hivyo, mimi nashauri hii itumike kama ni 'ofisi' badala ya 'afisi'.

Kwa kumalizia niseme kwamba hii ni hatua muhimu sana ya kuunda chombo imara ambacho kitasimamia masuala ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi ambao ndio roho ya kuendesha uchaguzi wenyewe. Nawaomba wenzangu tuupitishe mswada huu na mimi binafsi naunga mkono mswada huu kwa ukamilifu wake.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie mswada huu wa kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam.9 ya mwaka 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kupongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa umakini na umahiri wake katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Aidha, naomba kuipongeza wizara husika kwa kuweza kusimamia kazi hizi lakini na leo kutuletea mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu. Kwa umuhimu wake mswada huu leo toka asubuhi unajadiliwa na kwa kweli ni mswada muhimu sana kwa faida na maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naangalia sana majukumu ya Tume ya Uchaguzi na majukumu hayo yameainishwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, lakini Tume ya Uchaguzi yenyewe ile sheria yao ya uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya mwaka 1992, pamoja na Sheria ya Kura za Maoni Nam. 6 ya mwaka 2010. Pia, ukiangalia ile Sheria ya Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995 pia majukumu yale yameainishwa na Sheria ya Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji Nam. 4 ya mwaka 1995 imeainisha majukumu ya Tume ya Uchaguzi.

Kwa sababu hiyo basi, mimi nimesema tuna wajibu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watunga sheria, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba, tunaisimamia sheria hii na kuiweka vizuri ili Wazanzibari waweze kunufaika kwa wakati wote hasa katika uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa sababu mengi yameshazungumzwa sitaki kurejea yale ambayo yashazungumzwa, lakini nikasema lazima tuipe meno Tume ya Uchaguzi na kama sheria hii tunataka ifanye kazi vizuri na tukiipa Tume ya Uchaguzi meno maana yake nini, maana yake pia tutaweza kuwadhibiti wale wote wanaoweza kukiuka sheria, kanuni na miongozo na taratibu zilizowekwa ndani ya sheria zetu na majukumu yale ndani ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, tumejikuta ukiangalia sana watu wengi walikuwa wanakiuka sheria kwa sababu unakuta zile *styles* zilizowekwa mara nyingi ndani ya sheria mbali mbali unazikuta ndogo sana. Unakuta wakati mwengine mfano mtu anasema uongo au anatoa taarifa sio sahihi mbele ya tume, au anaitwa kutoa taarifa lakini anaweza kuikatalia tume hata hayo maadili yenyewe hayapo, lakini mtu huyo ataambiwa atoe shilingi laki tano au kiwango kisichozidi shilingi milioni moja. Kwa kweli sasa hivi wakati huu nafikiri umepitwa sana na wakati, sasa hivi lazima tufike pahala tuweke sheria ambayo kila mtu ataweza kujenga heshima, kuheshimu tume, lakini tume pia iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi.

Nafikiri kama tutaweza kulisimamia hili Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini haya mengi yaliyozungumzwa na matatizo mengine madogo madogo ambayo watu wanashindwa kabisa kujua utaratibu au sheria nzima ya Tume ya Uchaguzi na kuwalinda watu wa Tume ya Uchaguzi kwa maana ya viongozi na watumishi ambao wanasimamia sheria zile kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mengi yamezungumzwa sitaki kuyarejea, lakini nilichokuwa naomba sana hili tuliangalie kwa umakini wake ili sheria hizi tunazozipitisha basi tuone kwamba si sheria za kuchezewa chezewa. Kwa sababu wakati mwengine unakuta wenzetu hawa wanatujaribu sana na wanajaribu wanajua ah! Hata nikienda nitaambiwa nilipe shilingi 50,000 au shilingi 500,000/- kwa hiyo, kwao wanaona ni kitu cha kawaida. Kwa hiyo, mimi hili nilikuwa naliomba sana na niwaombe wenzangu tukubaliane kwamba lazima katika sheria hii basi tume tuipe meno.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba sana kwa sababu mengi yameshazungumzwa basi niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja na

nawaomba wenzangu wote tuipitishe sheria hii tuunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii na napenda nishukuru kwa kupata nafasi ya kuwa pamoja na nyinyi katika shughuli hizi kwa uteuzi nilioupata. *(Makofi)*

Kwanza nianze kwa kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Sasa kama jina la mswada linavyoeleza kwamba tunafuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi na kunatungwa Sheria ya kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mimi nimeona nijielekeze zaidi katika Sura ya Tatu, kwa sababu mengine mengi yamezungumzwa lakini labda hili kidogo ningependa kuliwekea uzito.

Mimi ningependa kuipongeza serikali kwa kuanzisha sheria hii kwa sababu inaonekana kutokuwa na sheria hii labda ndiko kulikopelekea matatizo mengi yaliyojitokeza huko nyuma kama alivyosema msemaji aliyepita. Sasa kuwepo kwa sheria hii kunaweza kukatusaidia kuwekana katika mstari madhubuti kwa sababu chochote kitakachotokea kuna sheria ambayo itachukua mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa kuanza na Mkurugenzi kwenye Kifungu Nam. 14 kuna sifa za Mkurugenzi. Nakubaliana na sifa zilizowekwa lakini ya Uzanzibari hiyo haina tatizo na ni lazima iwe hivyo. Hii ya pili ya shahada, shahada inayotakiwa mtu awe na Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu, ni mategemeo yangu kwamba Mhe. Rais kwa sababu yeye ndiye mteuzi atazingatia shahada ya atakayemchagua ilingane na mambo hayo. Kwa sababu Shahada iko *plain*; kuna Shahada hata ya mapishi tu, lakini sidhani kama mpishi ni nafasi yake hii. Kwa hiyo, ni tegemeo langu kwangu Rais atatuchagulia mtu mwenye sifa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha faraja zaidi ni sifa ya uzoefu, tuwe na *senior officer* aliyekwishafanya kazi katika serikali, katika utumishi wa umma na anayejua maadili. Kwa hivyo, pale unaweza ukampima mtu kwa kujua kwamba kweli huyu anafaa kwenye nafasi hii, sio tu labda mtu ambaye kwa kuwa ndio kwanza anaajiriwa, mradi tu kwa kuwa ana hicho cheti hapana. Sasa hii sifa nafikiri ni muhimu zaidi.

Nikienda hapo hapo lakini kwenye kifungu Nam.15 Muda wa Utumishi wa Mkurugenzi. Kwenye kifungu Nam.15(2) kuna kitu kinachosema Utaratibu wa Kumuachisha kazi Mkurugenzi. Mimi ningependa nilisemee hili kwa sababu

tukumbuke kwamba, kwenye Katiba yetu ya Zanzibar, Kifungu cha 119(6) cha Katiba hii kilikuwa kinazungumzia kwamba; "Mjumbe wa Tume ataondolewa kwenye madaraka yake na Rais au kutakuwa na tume ambayo itatoa mapendekezo".

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona hapa serikali imefanya uamuzi wa maana kumuwekea ulinzi Mkurugenzi na watendaji wake. Hili linaweza likampa yule Mkurugenzi *confidence* ya kufanya kazi kwa sababu atajua kwamba analindwa, ni Rais tu ndie anaepaswa kumteuwa, tunajijua Waswahili; Mkurugenzi ana hili, Mkurugenzi ana lile, hafai na mengi yanaweza yakajitokeza, lakini hakuna mwenye maamuzi isipokuwa Rais na Tume. Kwa hiyo, tutakuwa na uhakika wa kile kinachomfanya Mkurugenzi aondoke au abaki. Kwa hiyo, mimi nafikiri hapa uamuzi uliofanywa ni mzuri na utamfanya Mkurugenzi kujiamini wakati wa kutekeleza kazi zake na kuwa na uhakika wa kuwepo kwenye nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia na watendaji wake, tukija tukiangalia kwenye kifungu Nam. 22 kinahusu ufanisi wa wafanyakazi wa Tume. Kipengele hiki kinasisitiza muendelezo mzuri wa kulinda ile hazina ya uzoefu tunayoitaka. Wakiwa kwenye nafasi hizi watu hao wanapata mafunzo mengi, wanapata elimu kubwa, wanatembea sehemu nyingi, kwa hivyo, inakuwa ni wafanyakazi ambao wamepikwa na wamepikika na inakuwa ni hazina. Kwa hiyo, suala la kuondosha ondosha watu kiholela kwenye Tume mimi silioni kama lina tija. Kwa hiyo, kwa kifungu hiki nahisi kwamba hili nalo ni jambo zuri ambalo linaweza likatuwekea watu wetu wale ambao ni hazina kubwa kwa taifa kwenye Tume. Tume sio kitu cha kuchezea tia, toa, hapana, lazima kuwe na watu wanaojiamini na walioelimika kufanya kazi.

Pia, kwa kumalizia niende kwenye Sehemu ya Nne kwenye Masharti Mengineyo. Kuna baadhi ya wasemaji walizungumza kuhusu kwenye kifungu nambari 30 kinachozungumza "Kitendo chochote kilichofanywa au kimeacha kufanywa kwa nia njema". Natamani hapa Mhe. *AG* atusaidie maana tusiojua nia njema tuko wengi. Kwa hiyo, itabidi atusaidie kwa nia njema *AG* wale waliokuwa hawafahamu kama mimi kwa sababu kinatutia wasiwasi. *(Makofi)*

Sasa kutokana na kifungu hiki mimi nilichokielewa kwamba, hawa watendaji wetu majukumu yao ni makubwa na mazito. Kufanya kazi kwenye Tume ya Uchaguzi ni roho kwa roho watu ambao kwa kweli wako kwenye *risk* ya maisha yao wanakuwa *devoted* kuwekwa katika nafasi ile. Kwa hiyo, kutokana na majukumu hayo makubwa, mazito, nyeti na hasa tukizingatia utekelezaji wake na wajibu wao, sasa si vyema tukawatia hofu na wasiwasi wafanyakazi wetu.

Kwa hiyo, mimi ninafikiri hili la nia njema sidhani kama lina maana mbaya, tuwape moyo ili wafanye kazi vizuri na ni mategemeo yetu kama hayo yatakuwepo tutakuwa na Tume nzuri ambayo itaweza kusimamia katika uchaguzi ujao. Nakushukuru Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabla ya kutoa mchango wangu kwa sababu jambo hili ni muhimu sana katika nchi yetu nilikuwa nataka niwaambie Wawakilishi waliomo humu ndani pamoja na Watanzania na Wazanzibari wote wanaotusikiliza kwamba tunachokizungumza hapa ni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kumujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu Nam.119 kinasema kwamba;

"Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kwa utaratibu atakaoona unafaa,

(b) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa shughuli za Serikali kwenye Baraza la Wawakilishi,

(c) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi au iwapo hakuna kiongozi wa upinzani basi kwa kushauriana na vyama vya siasa,

(d) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu,

(e) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kama Rais atakavyoona inafaa".

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar imeshafanya mabadiliko mara kwa mara ya Katiba hii kutokana na miafaka iliyokuwa ikijitokeza huko nyuma kwa mazingatio ya uchaguzi wa Zanzibar. Miafaka hii baadhi yao vifungu havikuleta maslahi kwa Wazanzibari na mwisho wake vilikuwa vinataka kuashiria uvunjifu wa amani. Sasa basi, ni wakati muwafaka kwa sababu hii Katiba si msahafu ina uwezo wa kubadilika mara kwa mara. Sasa umefika wakati wa kubadilisha baadhi ya vifungu na kumpa uwezo Rais wa Zanzibar kuwateuwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi vile anavyoona inafaa, na tusimuwekee mipaka kwamba akutane na kiongozi wa kambi ya upinzani,

akutane na kiongozi wa serikali ndani ya Baraza. Haya hayakulenga maslahi kwa Katiba hii, hayakuleta maslahi. Kwa sababu hiyo miafaka iliyokuwa ikitengenezwa, ilikuwa ni miafaka ya kundi fulani la watu waliokuwa wakitaka wahodhi madaraka ya Zanzibar kwa nguvu.*(Makofi)*

Nasema hivyo kwa sababu. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa Tanzania, sikuwahi kushirikishwa hata siku moja katika miafaka hii, kwa nini na mimi nilikuwa nikishiriki kwenye uchaguzi. Lakini kulikuwa na kundi la watu walikuwa wakivuruka uchaguzi wakitegemea miafaka. Sasa basi tunawaambia kwamba miafaka hii, mimi kama Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, napeleka hoja hii kwenye Baraza la Mapinduzi kufuta vifungu vyote vya miafaka, na vifutwe kwa maslahi ya nchi hii kuelekea kwenye mstari wa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena kusema kwamba kwa sababu mimi ni mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, nitapeleka tena vifungu hivi vya miafaka ambavyo vilitengenezwa kwa kutaka kuiingiza Zanzibar kwenye matatizo, vifungu hivi vifutwe vyote na tutengeneze Katiba ambayo itampa uwezo Mhe. Rais kuunda Tume ya Uchaguzi itakayoongoza uchaguzi wa haki na huru kwa Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi sote ni mashuhuda tulioshuhudia uchaguzi uliopita kwa watu waliogombea baadhi yao kuweza kukiuka Katiba hii na kuweza kuchukua nafasi ya kwenda kutangaza matokeo kinyume na utaratibu waliokubali wenyewe kugombea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwamba sasa umefika wakati wa kuipeleka Zanzibar katika mazingira yanayofaa na yanayokubalika kitaifa na kimataifa, na hawa watu ambao walikuwa wanaichezea Katiba kwa makusudi, tunawaambia kwamba kwa kurudi tena kwenye Baraza hili ni mwiko, hawarudi tena. Waendelee na utaratibu wao wa kupiga ramli kesho, keshokutwa, mwezi ujao, mwaka ujao. Lakini kwa hoja ya kuwaingiza tena katika Baraza hili, sidhani kama Wazanzibari watakubali kuwachagua watu kama hao.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ndio yenye dhamana ya kulinda uchaguzi wote kuwa wa haki na huru. Mhe. Mwenyekiti, Tume hii haiwezi kuchaguliwa kama vile labda watu waliokutana sokoni, huyu kanunua changu, huyu kanunua pono na huyu kanunua nini, hiwezekani kitu kama hichi. Lazima turudi kwenye mstari tumkabidhi madaraka Rais wa Zanzibar achaguwe Tume yeye mwenyewe na itangaze yeye mwenyewe, ili nchi hii iweze kupata uchaguzi wa uhuru na wa haki.

Nasema hivyo kwa sababu, katiba hii kuna vifungu vimefunga humu na kwa sababu ya uwezo walionao Rais, kutokana na nafasi zake kumi, ndizo zilizompa uwezo yeye wa kututeuwa sisi kuingia kwenye Baraza. Lakini katiba hii imeweza kuzuwia na kusema kwamba lazima akutane na kiongozi wa kambi ya upinzani, hizo nafasi mbili akutane na kiongozi wa kambi ya upinzani. *(Makofi)*

Sasa hebu tujiulize, unawazuwia wajumbe wenye uwezo kuja kuwatetea Wazanzibari kwa sababu tu kuna mtu kanuna, eti, kanuna, kahamaki, kakasirika. Sasa sisi tunamwambia hivi, kama wewe umemwaga ugali basi sisi tutamwaga kachumbari. Nchi hii tunairudisha kwenye mstari wa Mapinduzi, haimaanishi kwamba tunaposimamia Mapinduzi ya Zanzibar, labda tunakiuka demokrasia, demokrasi itakuwepo kama kawaida. Lakini lazima tuheshimu Mapinduzi ya Zanzibar na kuheshimu Mapinduzi ya Zanzibar lazima tumuheshimu Rais wa Zanzibar, hapo ndipo tutakuwa tunaitendea haki katiba ya Zanzibar, tutakuwa tunawatendea haki Wazanzibari juu ya katiba yao. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said, kwa mchango wako na ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na ni Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum. Sasa namwita Mhe. Juma Ali Khatib Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, akifuatiwa na Mhe. Chum Kombo Khamis Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa afya njema na leo tukakutana hapa kufanyakazi za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza wafanyakazi wa Tume wa Uchaguzi ya Zanzibar, kwa kazi kubwa, ngumu na nzuri wanayoifanya. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimebahatika kushiriki katika chaguzi tokea mwaka 1995, nilikuwa karibu na Tume zote zilizopita na kuwa na Makamishna na Wakurugunzi wa Tume ya Uchaguzi na Wenyeviti wa Tume ya Uchaguzi. Lakini kwa kweli Tume tuliyokuwanayo sasa ni Tume inayofanyakazi kwa uadilifu mkubwa sana na kwa uzalendo wa hali ya juu sana, hatuna budi kuipongeza kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa, ngumu na ni watu walioweka uzalendo mbele. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni juzi tu tumeshuhudia kwamba ulitokezea mtihani kidogo katika uchaguzi wetu mkuu uliopita, lakini tumewaona wale waliokuwa

wazalendo mpaka leo tunao kwa maslahi ya nchi yetu na taifa letu. Kwa hivyo, napenda kuwapa pongezi sana na kuwapa moyo wasichoke kwa sababu wao wanalolifanya wanafanya kwa mujibu wa kiapo chao walichoapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kuwasihi wafanyakazi wetu wa Tume ya Uchaguzi, hususan wale wasimamizi wa Uchaguzi wa wilaya, kwamba tujaribu wakati wa uchaguzi ili kuepusha malumbano na malalamiko yasiyokuwa ya msingi, sasa zile kamati za maadili ziweze kufanyakazi. Kwa sababu katika uchaguzi Mhe. Mwenyekiti, kunakuwa na kamati ya maadili kwa ajili ya kufuata kanuni za uchaguzi na sheria za uchaguzi. Sasa hizi zisipofuatwa ndipo hutokezea migogoro na mifarakano.

Vile vile, napenda kuwasihi kwamba watowe elimu kwa wapiga kura inavyopaswa na kwa wakati maalum, kwa sababu tuna tatizo. Tatizo lililopo sheria zipo nzuri, lakini kuna watu hawana elimu ya wapiga kura au wanachelewa kupata ile elimu ya wapiga kura, kwa hivyo, kunakuwa na msongomano na matatizo mengi. Sasa Tume ya Uchaguzi wasichoke kusimamia jambo hili, kwa sababu ni jambo lenye maslahi kwa taifa letu na ni jambo litakaloufanya uchaguzi wetu uonekane kuwa ni wa uhuru na wa haki.

Mhe. Mwenyekiti, vyama vya siasa kila wakati wa uchaguzi huwa vinashirikishwa tofauti na hizo chaguzi za huko nyuma. Ndio maana nikasema kwamba Tume hii iko karibu na wadau wake, kwa sababu vyama vyote vyenye usajili wa kudumu na vyote vyenye wagombea, huwa kunaundwa kamati ndani ya Tume ya Uchaguzi, kunakuwa na Wenyeviti wa Kamati, kunakuwa na katibu, na kunakuwa na wajumbe, wajumbe wanatoka katika kila chama cha siasa. Jambo la kufurahisha zile kamati wanapokutana huwa wanaweka kando itikadi za kisiasa, lakini tunakuja kushindwa na tunakuja kuyasahau yote yale na elimu yote tuliyopewa wakati wa uchaguzi wa kutangazwa kwa matokeo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwashauri Tume ya Uchaguzi kwamba sasa hivi wale Wajumbe wa Kamati basi ni bora na wao wale viapo kabla ya kuanza hii kazi, kwa sababu malengo ni mazuri na elimu ni nzuri, lakini kwa bahati mbaya sisi au viongozi wa vyama vya siasa, inafika wakati yale yote tuliyokubaliana pamoja na Tume ya Uchaguzi sisi tunaanza kuvunja sheria baadhi yetu. Sasa jambo hili Mhe. Mwenyekiti, ni bora Tume ya Uchaguzi wakabadilika, ili kwenda mbele zaidi basi wale viongozi watakaotoka kwenye vyama watakaochukua nafasi hii, katika kamati zile.

Kwa mfano, kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama, kuna Kamati ya Maadili, kuna Kamati ya Fedha na Uchumi na kamati nyenginezo. Hawa watu kwanza wale

kiapo, kwa sababu tumechoka kuona kwamba wenzetu baadhi yao hawana lengo zuri, nia ni nzuri ipo. Lakini sasa itakapofika wakati wa mwisho ndipo mambo yanaanza kuharibika tunataka tutengeneze mambo haya ili kuweza kujenga mazingira mazuri na kusimamia chaguzi zetu ziwe huru na haki. Asitokezee mtu au chama chochote cha siasa kikatia doa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, yaliyopita sote tumeyaona matatizo mengi yalitokezea. Hata mimi ni mmoja katika waathirika chama changu kuna mawakala walipigwa Pemba, taarifa zipo na ripoti zipo kituo cha polisi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, haya ni mapungufu. Kwa hivyo, Tume ya Uchaguzi wawe makini sana. Vile vile, inasikitisha kuona baadhi ya wasimamizi wa Tume ya Uchaguzi hususan wa wilaya, wanakuwa na itikadi ya vyama vya siasa. Tumeshuhudia Mhe. Mwenyekiti, siku ya kupiga kura mawakala wengi hapa mjini walikuwa hawajapata vitambulisho vyao vya kwenda kupiga kura, ilichukua zaidi ya masaa matatu. Sasa ile ilikuwa ni *sabotage*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ni lazima Tume Mkurugenzi, Mwenyekiti na Makamishna, wawasimamie wale wasimamizi wa uchaguzi wa wilaya, ili matatizo na migongano yasitokezee ikaja ikaleta mtafaruku. Napenda kusema kwamba nashirikiana na wawakilishi wote wa Baraza la Wawakilishi, naunga mkono hoja zao.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii iliopo mezani kwa asilimia mia kwa mia, sina mashaka wala sina pingamizi, ahsante Mhe. Mwenyekiti. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Juma Ali Khatib, kwa mchango wako. Sasa nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku yetu hii ya leo Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii adhimu na mimi ya kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuahidi kuwapatia ofisi za kudumu Tume zetu za Uchaguzi.

Lakini pili napenda nichukuwe fursa hii niupongeze uongozi wa wizara kwa kuleta mswada huu tukaweza kuujadili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja katika kipengele cha 16(b). Mhe. Mwenyekiti, kipengele cha 16(b) ni kuandaa na kuratibu mikutano ya Tume. Kuandaa na Kuratibu Mikutano ya Tume ni kazi ya Tume ya Uchaguzi. Maoni yangu ni kwamba niwaombe Waheshimiwa Wajumbe mswada huu tuupitishe, ili tuone kwamba unafanyakazi vizuri zaidi na kuweza kuwapatia faraja wananchi wetu, kwa kupitia uratibu wa mikutano, naomba Tume iandae mikutano na iwape mafunzo vyama vya siasa, na ifanye juhudi za makusudi iwape mafunzo kwani inanaonekana katika kipangele hiki, baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wanavunja sheria na hatima yake kuleta migongano ambayo haina tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, naoma niende kwenye kipengele cha 31. Kipengele hiki kimetoa adhabu kwa yule mtu ambaye atatoa taarifa za ofisi. Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba adhabu hii iliyotolewa ni ndogo sana, kwani tumewaona viongozi wa vyama vya siasa kwa chaguzi ambazo zimepita, tumeona mengi yametokea yakiwemo ya uvunjaji wa sheria kwenye kipengele hiki na hatimaye wananchi wetu wanapata madhara kutokana na uvunjwaji na ukiukwaji wao wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kipengele cha 31 nitazungumzia zaidi kuhusu ukiukwaji wa sheria na hasa madhara yake yanayowapata wakinamama. Wakati inapofika hatua mgombea yeyote anayechukua hatua ya kujitangaza bila ya idhini ya Tume ya Uchaguzi, adhari yake wanawake wanapata madhara zaidi, yakiwemo ya mgomo wanawake wale ndio wanaathirika na watoto. Kwa hivyo, nimuomba Mhe. Waziri hili tuliangalie kwa kina suala hili katika mswada huu, na tuone kwamba sheria imechukua mkondo wake kwa wale ambao wanavunja sheria na kuwasababishia madhara wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona duniani kote kunapotokea migogoro kama hii basi wanawake ndio wanaopata madhara zaidi, tunaona katika vyombo vya habari wanapata misaada, lakini hatimayake misaada ile wanashindwa hata kukaa pahala wakawapatia watoto hata maji ya kunywa kutokana na migogoro kama hii.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba tumechoka kutokana na baadhi ya viongozi wa vyama kuchukua sheria mikononi mwao bila ya kufuata sheria za Tume ya Uchaguzi na kutusababishia madhara makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yameshachangiwa, kwa hivyo, kwa hayo machache naomba niunge mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia na sasa umefika wakati wake tuufanyie kazi ipasavyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, kwa michango yako. Lakini na mimi kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kuleta mswada wake huu. Jengine niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia na hata wale waliochangia kwa maandishi. Lakini pia wachangiaji walikuwa ni wengi. Kwa hivyo, niwapongeze wachangiaji wote, inaonekana wazi Mhe. Waziri, huu mswada utaleta manufaa na tija. Kwa hivyo, niwaachie Mhe. Waziri na watendaji wake wakaupitie ili kesho tuweze kufanya majumuisho.

Waheshimiwa Wajumbe, tukijaaliwa kesho ataanza Mhe. Naibu Waziri katika majumuisho hayo, akifuatiwa na Mhe. Waziri muhusika. Waheshimiwa Wajumbe, nawapongezeni sana na nawatakieni kila la kheri, na kikao nimekiahirisha mpaka kesho saa 3:00 asubuhi *In shaa Allah*. *(Makofi)*

(Saa 1:40 usiku kikao kiliahirishwa mpaka
tarehe 16/02/2017 saa 3:00 za asubuhi)